**18 MEI, 2026**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA TATU

**Kikao cha Thelathini na Moja – Tarehe 18 Mei, 2026**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mkutano wa Tatu, Kikao cha Thelathini na Moja.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Katibu.

**18 MEI, 2026**

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI. Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, Mbunge wa Segerea, aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 360

**Ujenzi wa Barabara ya Bima Hadi Mawenzi - Kimanga kwa Kiwango cha Lami**

**MHE. AGNESTA L. KAIZA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Barabara ya Bima hadi Mawenzi – Kimanga kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, Mbunge wa Jimbo la Segerea, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuiboresha kwa awamu Barabara ya Bima – Mawenzi – Kimanga yenye urefu wa kilometa 3.65, ambapo katika mwaka wa fedha 2023/2024 kipande chenye urefu wa meta 200 kimejengwa kwa tabaka la zege *(concrete pavement)* kwa gharama ya shilingi milioni 281 na kipande chenye urefu wa kilometa 0.4 kimejengwa kwa tabaka la lami *(asphalt)* kwa gharama ya shilingi milioni 593, huku ujenzi wa sehemu nyingine ukiendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Serikali imeweka katika mpango ujenzi wa barabara hiyo kwa tabaka la zege Kilometa 0.65 kwa gharama ya shilingi bilioni 1.87.

Aidha, kipande chenye urefu wa kilometa 0.7 kimejengwa kupitia Mradi wa *DMDP II* unaoendelea kutekelezwa katika Wilaya zote za Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutekeleza ujenzi wa barabara hii kwa awamu hadi kukamilika kwake ili kuboresha miundombinu ya usafiri na kurahisisha shughuli za usafirishaji kwa wananchi kwa ujumla. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, ninaomba nitumie nafasi hii kuishukuru na kuipongeza Serikali kwa jinsi ambavyo imeonesha kabisa kwa matendo kuhusiana na hii barabara kwamba hivi sasa ninavyoongea, Mkurugenzi pamoja na *DC* wetu wa wilaya tayari wameshaanza kutekeleza agizo la Serikali la kuhakikisha barabara ile inaanza kupitika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii pia kuwapongeza sana Mkurugenzi wangu pamoja na *DC* kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. Sambamba na hilo, niipongeze Serikali kwa kutenga fedha kiasi cha shilingi bilioni *1.8* kwa ajili ya hii barabara. Sasa maswali yangu ya nyongeza ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kutenga bajeti ni jambo lingine na kupeleka fedha ni jambo lingine, ningependa kufahamu kauli ya Serikali, imejipanga namna gani kuhakikisha fedha hizi zinapelekwa kwa haraka ili barabara hii iweze kujengwa kwa haraka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Barabara ya kutoka Maji Chumvi kupitia Mazda hadi Barakuda - Chang'ombe ni barabara ambayo hivi sasa imesimama kwa sababu Serikali haijalipa fidia. Ningependa kufahamu, ni lini Serikali itakwenda kulipa fidia kwa wananchi wale ili sasa barabara hii iweze kujengwa? Ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninampongeza sana Mheshimiwa Agnesta Lambert, amekuwa mfuatiliaji makini sana kuhakikisha kwamba barabara za Jimbo la Segerea zinajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali hii makini imeendelea kutekeleza kwa vitendo ujenzi wa barabara hizi, naye ni shahidi kwamba wiki iliyopita aliona barabara hii mkandarasi yuko *site*, timu ya *TARURA* ilihamia pale; Mkurugenzi, Mkuu wa Wilaya, na watalaamu wengine ili kuhakikisha kwamba barabara inajengwa na kurejesha usafiri kwa wananchi katika hali nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie kwamba kwa kutambua umuhimu wa barabara hiyo, bajeti ya mwaka ujao tunaoanza Julai mwaka huu imetenga shilingi bilioni 1,870,000,000, kwa ajili ya kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Pia tutahakikisha kwamba fedha hizo zinapelekwa mapema iwezekanavyo ili barabara ijengwe vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili kuhusu fidia kwa wananchi wa Barabara ya Maji Chumvi kwenda Barakuda, tunafahamu kwamba, wako wananchi ambao wana haki ya kupewa fidia na Serikali tayari ilishafanya tathmini ya kujua gharama za fidia zinazohitajika na hivi sasa tuko kwenye taratibu za kibajeti ili kuhakisha kwamba fedha ile inapatikana na kwenda kulipa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi kwamba eneo hilo Serikali italipa fidia ili kuhakikisha kwamba barabara hiyo inajengwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema Mwandabila na Mheshimiwa Patali, niliwaona.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kufahamu Serikali ina mpango gani wa kuiweka lami

barabara ya mchepuko kutoka hii *TANZAM* inayoanzia Mtaa wa Mwakabwangazi Kata ya Katete kuelekea Kata ya Makambini, Tunduma?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kama una majibu ya Tunduma.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko barabara katika miji ikiwemo Mji wa Tunduma ambazo ziko kwenye Mpango wa *TACTIC,* na pia ziko barabara ambazo ziko kwenye mpango wa kawaida wa *TARURA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, ikiwa hicho ni kipaumbele cha Halmashauri ya Mji wa Tunduma, sisi Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI tutahakikisha tunafuatilia kwa karibu ili kujua hali au *status* ya barabara hiyo na kutenga fedha kwa awamu kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo iwe kwa kiwango cha changarawe au lami kwa kadiri ambavyo tutakuwa tunajipanga, lakini muhimu, kuhakikisha kwamba barabara hiyo inatengenezwa na inapitika vizuri, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Patali, swali fupi la nyongeza.

**MHE. PATALI S. PATALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, takribani kata 14 za Jimbo la Mbeya Vijijini miundombinu ya barabara inayosimamiwa na *TARURA* imeharibika sana. Ni nini mpango wa dharura wa Serikali kuhakikisha barabara hizi zinatengenezwa kwa haraka? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Mheshimiwa Patali, Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini amefuatilia mara kadhaa kuhusiana na barabara katika kata zake 14 ambazo ni kweli zimeathirika sana na mvua ambazo zimenyesha na ambazo zinaendelea kunyesha ingawa ziko katika msimu wa mwisho sasa. Serikali inafahamu

kwamba, barabara hizo zimeathirika na mvua na tayari tumeshafanya tathmini kote nchini ikiwemo katika Jimbo la Mbeya Vijijini na tumeshapata taarifa ya gharama ya fedha zinazohitajika kwa ajili ya matengenezo, na kwa ujumla katika nchi nzima mpaka mwezi Aprili mwishoni tulikuwa tunahitaji shilingi 300,000,000,000 kwa ajili ya ukarabati wa barabara zilizoathirika na mafuriko ya mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutahakikisha kwenye bajeti inayofuata na pia kwa fedha za dharura ambazo tayari tunaendelea na utaratibu wa kuziandaa, tunapeleka fedha kurekebisha barabara ziweze kupitika wakati tunajiandaa na matengenezo ya kudumu ya barabara hizo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kadogosa na Mheshimiwa Esther Matiko, niliwaona.

**MHE. MASANJA K. KADOGOSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nikushukuru kwa kunipa fursa hii. Kwanza, tunaishukuru sana Serikali kwa kuanzisha ujenzi wa barabara ya Mji wetu mdogo wa Nkololo na Mji wetu wa Dutwa, lakini hizi barabara zimekuwa zikisuasua sana. Ni lini Serikali itapeleka fedha za kutosha ili ziweze kukamilika? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa kaka yangu, Mheshimiwa Masanja Kadogosa, Mbunge wa Jimbo la Bariadi Vijijini, amefuatilia sana kuhusiana na ujenzi wa barabara katika Mji wa Nkololo na katika eneo la Dutwa ambalo barabara ile inakwenda kwenye Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunafahamu zile barabara mbili zilizopo katika Mji wa Nkololo, na wakandarasi wale watalipwa fedha. Ninajua utekelezaji umeendelea iko moja iko takribani 60% nyingine 40% lakini mpango wa Serikali ni kuhakikisha tunawalipa

*certificates* ambazo wamesha-*apply* ili wakamilishe ujenzi wa barabara zile kwa wakati katika Mji wa Nkololo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya kutoka Dutwa kwenda Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya, mkandarasi hajakidhi matawa ya Serikali haja-*adhere* kwenye mkataba amefanya kazi kwa kusuasua na tayari tuko hatua za mwisho za kuvunja mkataba na kupata mkandarasi mwingine ili aweze kukamilisha ujenzi wa barabara ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali itasimamia kuhakikisha barabara hizo zinakamilika kwa wakati.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko, utamalizia Mheshimiwa Salma Kikwete.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Mji wa Tarime iko kwenye Mpango wa *TACTIC* ambapo imetengewa takribani kilometa 18 za lami na nikataka kujua, ni lini Serikali itaanza utekelezaji wa ujenzi wa barabara za lami kuzunguka Mji wa Tarime ukizingatia uko mpakani na iweze kuchechemua uchumi wa mji ule?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza dada yangu Mheshimiwa Esther Matiko, amefuatilia mara kadhaa, na kwa kweli wananchi wa Halmashauri ya Mji wa Tarime ni kati ya wananchi ambao watanufaika na mpango wa uboreshaji miji wa *TACTIC*. Vilevile Mji wa Tarime uko awamu ya tatu ya utekelezaji wa Mradi huo, na tayari usanifu umefanyika na hatua ambazo zinafuata sasa ni Serikali kuweka mipango ya pamoja na Benki ya Dunia kwa ajili ya kuanza ujenzi wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya kukamilisha taratibu za Serikali ya Tanzania na Benki ya Dunia, mapema iwezekanavyo

tutahakikisha fedha zinakwenda kwa ajili ya kuanza kujenga barabara za lami katika Mji wa Tarime.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salma Kikwete.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na kuwa sichangii hoja, ninauliza swali la nyongeza. Barabara zangu za Mchinga zote zimeharibika na mimi nina tarafa nne, na hakuna kata yoyote unayoweza kutoka kwenye Jimbo la Mchinga kuja makao makuu ya kata pale Mchinga. Je, nini mpango wa Serikali wa kutusaidia ikiwa ni sambamba na yeye mwenyewe kuja kwenye Jimbo la Mchinga kuona hizo barabara? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Jimbo la Mchinga lina hali ya kijiografia ambayo iko *complicated* kidogo, lakini mama yangu, Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete amelisemea mara kadhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimjulishe Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo La Mchinga, kwamba kwanza, Meneja wa *TARURA* wa Mkoa wa Lindi, na Meneja wa *TARURA* Wilaya ya Lindi wameshawasilisha mpango na gharama zinazohitajika baada ya tathmini kwa ajili ya ukarabati wa barabara zote katika Jimbo la Mchinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, nimwelekeze Meneja wa *TARURA* wa Mkoa wa Lindi na Wilaya ya Lindi wafike mara moja ndani ya wiki hii katika Jimbo la Mchinga, wafanye tathmini ya maeneo yaliyoharibika kabisa ambayo yanazuia wananchi wasiweze kusafiri kutoka kwenye kata yao moja kwenda kata nyingine au kwenda makao makuu ya halmashauri, ili hatua za dharura zitumike kurekebisha, na wananchi waendelee kusafiri na kupita wakati tunaendelea na mpango ule wa ukarabati wa barabara zile ambao tayari tumefanya tathmini kwa nchi nzima.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, Mbunge wa Lulindi.

Na. 361

**Wabunge Kuzuiwa Kukagua Miradi**

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA** aliuliza:-

Je, ni sahihi kwa watendaji kuwazuia Wabunge kukagua miradi ya maendeleo na kuwanyima taarifa za utekelezaji katika majimbo yao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, Mbunge wa Jimbo la Lulindi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287 na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288, Mbunge ni Mjumbe wa Baraza la Madiwani, chombo chenye mamlaka ya juu ya maamuzi katika halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wabunge wa majimbo katika halmashauri ni Wajumbe wa Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango. Kwa muktadha huo, ni wajibu wa watendaji kuwashirikisha Wabunge kwa kuwapatia taarifa za utekelezaji wa miradi, na kimsingi Baraza linapaswa kuwa na vikao kila robo mwaka, na moja ya ajenda ni kupokea taarifa za fedha na utekelezaji wa miradi mbalimbali. Hivyo, Mbunge kama Mjumbe anapaswa kupewa kabrasha la kikao kwa kila kikao kinapofanyika na kushiriki ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI imeweka utaratibu wa kuwaandikia Waheshimiwa Wabunge barua za kuwasilisha taarifa za fedha za miradi ya maendeleo na matumizi mengineyo katika halmashauri zao. Hivi karibuni Waheshimiwa Wabunge watapokea barua za taarifa ya fedha za miradi ya maendeleo na matumizi mengineyo kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Januari, 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kusisitiza kuwa ushirikiano kati ya watendaji na Waheshimiwa Wabunge ni muhimu kwa kuimarisha uwajibikaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mbunge kipindi kingi anatumia akiwa hapa Bungeni, lakini ana msaidizi wake ambaye ni Katibu wa Mbunge katika Ofisi, je, Katibu wa anaruhusiwa kwenda kukagua miradi akipata taarifa ya kwamba kuna eneo kuna changamoto ya mradi? Je, Katibu ana jukumu gani kufanya kazi za Mbunge wakati Mbunge hayuko katika eneo lake la kazi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kama una majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana kaka yangu, Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, Mbunge wa Lulindi kwa ufuatiliaji wa karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la msingi sana katika eneo hili kwanza, Waheshimiwa Wabunge ni Wajumbe wa Kamati za Fedha na Mabaraza ya Madiwani katika halmashauri zao na ni maelekezo ya Serikali. Nitumie nafasi hii kusisitiza kwamba ni wajibu wa Mkurugenzi na Watendaji wa Halmashauri kuhakikisha wanawapatia Waheshimiwa Wabunge taarifa kwa wakati kuhusiana na mapokezi ya fedha na miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika maeneo yao. Hili ni suala la lazima kwa

Wakurugenzi kulitekeleza na Ofisi wa Waziri Mkuu TAMISEMI ilishatoa maelekezo mara kadhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikitokea kuna halmashauri ambazo hazitoi taarifa ya mapokezi ya fedha kwa Waheshimiwa Wabunge, ninaomba tuwasilishieni taarifa Ofisi ya Waziri Mkuu, na sisi tutachukua hatua kwa sababu ni takwa la kisheria na kiuongozi na miongozo yetu kwamba, lazima Wabunge wapate taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Makatibu; Katibu ni msaidizi wa Mheshimiwa Mbunge, anaweza kushiriki kwenye Baraza la Madiwani, lakini pia anaweza kushiriki kwenye shughuli za ukaguzi wa miradi pamoja na Kamati husika ambazo zinakagua miradi hiyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecilia Paresso, nilikuona.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kumekuwa na hoja ya muda mrefu ya Wabunge wa Viti Maalum kuruhusiwa kuingia kwenye Kamati za Fedha. Pamoja na kwamba Mbunge wa Viti Maalum ataingia kwenye Kamati nyinginezo, lakini ikifika tu Kamati ya Fedha kwenye halmashauri zetu, Wabunge wa Viti Maalum hatuingii. Nini Kauli ya Serikali kuhusiana na hili?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge Cecilia Paresso amesema, kwa mujibu wa kanuni zetu Waheshimiwa Wabunge wa Viti Maalum ni Wajumbe wa Kamati nyingine na Baraza la Madiwani, lakini sio Wajumbe wa Kamati za Fedha, Uongozi na Mipango za Halmashauri. Sasa hii ni kanuni ambayo hivi sasa bado ipo, lakini ikiwa kuna sababu ya muhimu ya kuiboresha kanuni hiyo, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, iko tayari kuendelea kupokea maoni hayo, kufanya tathmini na kuona ambavyo inafaa, tuweze kuboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa ni Kanuni na ni muhimu tufuate Sheria na Kanuni zetu kwa sababu tumeziweka wenyewe na zinatuongoza. Kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, tumepokea maoni. Tutaendelea kufanya tathmini na kuona namna nzuri ya kuboresha mazingira kama hayo.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Mariam Madalu Nyoka, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 362

**Utaratibu Rahisi wa Kutoa Mikopo - Ruvuma**

**MHE. MARIAM M. NYOKA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaweka utaratibu rahisi wa mikopo kwa wakulima wadogo, hasa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, Mkoa wa Ruvuma?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Madalu Nyoka, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi yote ya mkopo wa 10% yanazingatia utaratibu uliobainishwa katika Kanuni na Mwongozo wa Utoaji na Usimamizi wa Mikopo wa Mwaka 2024. Halmashauri hutakiwa kushughulikia maombi ya mikopo yaliyopokelewa kielektroniki katika kipindi kisichozidi miezi miwili tangu tarehe ya kupokea maombi ya mkopo na kukitaarifu kikundi kupata mkopo ndani ya muda wa siku saba tangu uamuzi wa kukubali maombi kufikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfumo wa WEZESHA unasaidia kurahisisha utoaji wa mikopo kwa wakati, kwani umepunguza udanganyifu wa vikundi vinavyoomba mikopo hiyo. Maombi

hayo ya mkopo yakiridhiwa, halmashauri huingiza kiasi cha mkopo kilichoridhiwa katika akaunti ya kikundi husika baada ya kusaini mkataba na kikundi. Aidha, mikopo ya kilimo inaanza kutolewa kuanzia robo ya pili ya Oktoba hadi Disemba kwa ajili kuhakikisha wakulima wanawahi msimu wa kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025, Mkoa wa Ruvuma umefanikiwa kutoa mikopo ya kilimo na ufugaji kwa wanawake, vijana na wenye ulemavu, ambapo vikundi 105 vya wanawake vyenye wanufaika 1,020 vimepata mkopo wa shilingi bilioni 1.37. Vikundi vya vijana 78 vyenye wanufaika 632 vimepata mikopo ya shilingi bilioni 1.28 na vikundi 19 vya watu wenye ulemavu vyenye wanufaika 53 vimepata mkopo wa shilingi milioni 153.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kutoa elimu ya ujasiriamali na kuwajengea uwezo wakulima na wafugaji wadogo katika Mkoa wa Ruvuma na maeneo mengine nchini, ili waweze kukidhi vigezo vya kupata mikopo itakayowezesha kupata mitaji ya kuanzisha miradi ya kiuchumi na kuinua hali za maisha yao, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam Madalu Nyoka.

**MHE. MARIAM M. NYOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwepo kwa mifumo ya mikopo, bado wakulima wadogo wengi Mkoani Ruvuma wanashindwa kunufaika. Sasa je, lini Serikali itachukua hatua madhubuti katika kurahisisha masharti ili kuondoa urasimu uliopo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Serikali iko tayari kutoa mikopo kwa wakulima wadogo kwa mtu mmoja mmoja na kuondokana na vikundi ambavyo mara nyingi imekuwa na urasimu? Ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Mariam Madalu

Nyoka, Mbunge wa Viti Maalum, amekuwa mfuatiliaji sana wa maslahi ya wananchi; wanawake wa Mkoa wa Ruvuma na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwanza tunafahamu kweli ziko changamoto za baadhi ya wakulima, na hususan wakulima wadogo kukosa mikopo. Serikali imeweka utaratibu mzuri, kwanza kwa kupitia mikopo ya 10%; wakijiunga kwenye vikundi wanaweza kupata mikopo ile, na kama wataomba mapema, kuna upatikanaji wa fedha katika mafungu yale ya 10%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninatumia nafasi hii kuwaelekeza Wakurugenzi wa Halmashauri kuhakikisha wanatenga fedha na kuwapa kipaumbele wakulima pale wanapoomba mikopo wapate fedha hizo kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na 10% tuna Benki ya Kilimo, ambayo pia, inatoa fursa. Pia, kuna vyama vya ushirika katika maeneo mengine, ambavyo vinatoa mikopo kwa wakulima. Kwa hiyo, nawaasa na kuwaomba wananchi wote kuendelea kutumia fursa hiyo ya mikopo ya 10%, Benki ya Kilimo, pamoja na vyama vya ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la…

**MHE. MARIAM M. NYOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mkulima mmoja mmoja aweze kukopesheka.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na mikopo hii ya 10% kukopeshwa kwa mkulima mmoja mmoja, Kanuni zetu za Mikopo zimeeleza kuwa, watu wenye ulemavu wanaweza kupata mkopo mtu mmoja mmoja, lakini kwa wanawake na vijana wanatakiwa kujiunga kwenye vikundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, kumekuwa na ushauri mara nyingi kwamba, tuone uwezekano wa kubadili kanuni na kuwezesha mtu mmoja mmoja kupata mikopo hii ya

10%. Serikali imepokea maoni ya Waheshimiwa Wabunge na wadau wengine, tunaendelea kufanyia tathmini na kuona kama kuna uwezekano wa kubadilisha kanuni zetu na kuweza kukopesha mtu mmoja mmoja, basi Serikali itachukua hatua ili kufikia malengo ya 10%.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Johnston Johansen Mutasingwa, Mbunge wa Bukoba Mjini, aulize swali lake.

Na. 363

**Kujenga Maeneo ya Maegesho ya Bodaboda**

**MHE. ENG. JOHNSTON J. MUTASINGWA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwajengea vijana waendesha pikipiki maeneo ya maegesho?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Johnston Johansen Mutasingwa, Mbunge wa Jimbo la Bukoba Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa kazi ya usafirishaji inayofanywa na vijana maarufu kama bodaboda nchini. Ili kuboresha huduma hiyo, Serikali imetoa maelekezo kwa Wakurugenzi wa Halmashauri zote nchini kuendelea kuwatambua na kutenga bajeti ya kujenga vituo vya madereva badoboda katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetenga maeneo 662 yenye ukubwa wa meta za mraba 5,859,756.18 katika halmashauri 146 kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo wakiwemo madereva bodaboda. Aidha, ujenzi wa ofisi za wafanyabiashara wadogo nchini, wakiwemo bodaboda

unaendelea ili kuboresha na kurahisisha usimamizi, mawasiliano na utekelezaji wa shughuli zao katika kila mkoa, ambapo kiasi cha takribani shilingi milioni 260 zimetolewa katika mikoa 13. Baada ya kutambua na kutoa namba za maeneo hayo, Serikali itaendelea na ujenzi wa maegesho katika vituo vya bodaboda nchini, ikiwemo katika Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Johnston Mutasingwa.

**MHE. ENG. JOHNSTON J. MUTASINGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru Serikali kwa majibu yake mazuri. Nina mambo mawili, na moja ni ushauri. Kwa kuwa, sasa vijana wengi wanalipa fedha ya *parking* kwenye maeneo mengi, hasa maeneo ya Bukoba Mjini, lakini hawana maeneo maalum ya maegesho, ninaishauri Ofisi ya Waziri Mkuu iwahimize na kuwaelekeza Wakurugenzi wawajengee maeneo ya kupaki pikipiki zao, ili wanapolipa *parking* iwe kweli, maeneo yale yametengenezwa hasa kwa utumiaji mzuri wa *road reserve* ya *TARURA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kumekuwa na malalamiko makubwa sana ya hawa madereva bodaboda, hasa kuhusiana na leseni za uendeshaji pikipiki kwamba ni kubwa, shilingi 7,000 sawasawa na gari. Je, Ofisi ya Waziri Mkuu haiwezi kukaa na Ofisi ya Waziri wa Fedha, ili kuona namna ya kuweza kuwapunguzia hawa vijana leseni ya udeva kutoka shilingi 7,000 labda mpaka pungufu ya hapo? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa *Eng,* Johnstone Johansen Mtasingwa, Mbunge wa Jimbo la Bukoba Mjini, kwani amekuwa mfuatiliaji sana wa maslahi ya wananchi. Ninamhakikishia, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, tutaendelea kumpa ushirikiano wa hali na mali kuhakikisha wananchi wa Bukoba Mjini wanapata manufaa ya Serikali yao hii sikivu.

Mheshimiwa mwenyekiti, ni kweli kwamba, tuna changamoto ya *parking* kwa madereva bodaboda. Serikali kwa kulitambua hilo, imechukua hatua mahususi. Tayari katika kipindi cha miaka minne jumla ya mikoa 13 imetoa fedha takribani shilingi milioni 260 na kujenga vituo vya *parking* kwa ajili ya madereva bodaboda na zoezi hili ni endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetoa maelekezo kuhakikisha kwamba, halmashauri zote zinawatambua bodaboda, kutenga maeneo na kuweka namba za vituo vya bodaboda katika maeneo hayo, ili iwe rahisi katika usimamizi na uendeshaji wa shughuli hizo za usafirishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba, tayari wametambua maeneo 39 na wameweka namba kwenye maeneo hayo, lakini bado kujenga vituo vya bodaboda. Kwa hiyo, ninaomba nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, nimsisitize Mkurugenzi wa Manispaa ya Bukoba kuhakikisha kwamba sasa wanaanza ujenzi wa vituo vya bodaboda, kwa ajili ya kuhakikisha kwamba huduma hiyo inaboreshwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, kuhusu leseni za bodaboda kuwa shilingi 7,000, suala hili sisi Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, tutashauriana na wenzetu wa Wizara ya Fedha na wao wataona kwa kadiri inavyowezekana kufanya maboresho, ikiwa inawezekana, lakini sisi tumelichukua kama Serikali, kwa ajili ya kushauriana na kuchukua hatua stahiki kwa kadiri ya mazingira yatakavyoruhusu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sikudhani Chikambo.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kwamba vijana wa bodaboda wanapofanya zile kazi ni kama sehemu ya ajira zao na sisi sote humu ndani tutakuwa mashahidi, hata wakati wa uchaguzi vijana wa bodaboda tunawatumia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amesema kwamba, kuna mikoa ambayo wanakusudia kwenda

kuwajengea maeneo ya maegesho, lakini sisi Tunduru pia tuna hiyo shida. Vijana wetu wengi inyeshe mvua, liwake jua, wenyewe wanakaa kwenye mazingira siyo mazuri. Ninatamani kujua, ni nini sasa mkakati wa Serikali katika hiyo mikoa ambayo ameisema kwenda kuijengea, vipi kuhusu Wilaya yetu ya Tunduru na vijana wale ambao wana shida; wanaegesha magari yao katika maeneo ambayo siyo salama? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninaomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge, ni maelekezo ya Serikali kwamba, halmashauri zote ziwatambue madereva bodaboda, zitambue vituo vyao vya kuegesha bodaboda na kuviwekea namba, na pia, kuendelea kuboresha, kwa maana ya kujenga vivuli *(shades)* na vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninatumia nafasi hii kumwelekeza na kumsisitiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru kuhakikisha pia wanafuata na kutekeleza maelekezo hayo ya Serikali kwa awamu, kadiri ya bajeti zao ili vijana ambao wanafanya biashara hii muhimu ya usafirishaji, waweze kuwa katika mazingira bora, iwezeshe kuratibu vizuri usafiri wa shughuli hizi za bodaboda.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi. Yapo mambo ambayo tunatakiwa Wizara hii ya TAMISEMI iyaangalie; bodaboda na watu wa bajaji wale wanadaiwa *TARURA*, wanadaiwa leseni, wanadaiwa *parking* na wanadaiwa *TRA*. Wale vijana wanakuwa na pikipiki na bajaji za kukodi wanatakiwa kulipa shilingi 10,000 mpaka shilingi 25,000. Hivi kwa haya madai na michango hiyo yote ya Serikali watalipa nini? Kwa nini hatufanyi maamuzi ya kuwasaidia hawa vijana wa bodaboda na bajaji ili wapate nafuu ya maisha?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhamira ya dhati kabisa ya Serikali kuhakikisha kwamba, vijana wa bodaboda wanaboreshewa mazingira yao ya kazi na kuondolewa kero mbalimbali ambazo zinawasibu katika utekelezaji wa shughuli zao za usafirishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea, kwanza kuwatambua, pili kuwatengea na kuwajengea maeneo ya kupaki bodaboda, na pia, kuondoa tozo, ushuru na kodi ambazo hazina ulazima, ili kuwawezesha kufanya shughuli vizuri. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Getere, kwamba tutaendelea, kama Serikali, kupitia na kuona namna ambavyo tutaboresha mazingira ya bodaboda ili waweze kufanya kazi katika mazingira bora zaidi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki, aulize swali lake.

Na. 364

**Ukarabati wa Zahanati ya Kalemawe - Same Mashariki**

**MHE. ANNE K. MALECELA** aliuliza: -

Je, Serikali haioni umuhimu wa kukarabati zahanati ya Kijiji cha Kalemawe kwa kuwa ni chakavu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Jimbo la Same Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya uchambuzi na kuorodhesha jumla ya zahanati kongwe 1,226 kote nchini, ikiwemo zahanati ya Kalemawe, ambazo zinahitaji ukarabati mkubwa. Katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali imetoa fedha ya nyongeza, shilingi milioni 60, pamoja na shilingi milioni 15, Fedha za Mfuko wa Jimbo, kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Zahanati ya Makokane, Kata ya Kalemawe. Aidha, ujenzi wa zahanati hiyo upo hatua ya ukamilishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga fedha, kwa ajili ya ukarabati wa zahanati kongwe nchini, ikiwemo Zahanati ya Kalemawe katika Halmashauri ya Wilaya ya Same, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anne Kilango Malecela.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. Hii Zahanati ya Kalemawe imekuwa ni kimbilio la wananchi wengi; siyo wa Kijiji cha Kalemawe tu, kuna Kijiji cha Kihurio, Kijiji cha Kangokoro na Kijiji cha Karamba kwa sababu, ina daktari mzuri na anatoa huduma vizuri sana. Sasa je, Mheshimiwa Waziri, haoni ni vyema sasa kwa sababu, zahanati ile inakimbiliwa na watu wengi wafanye udharura wa kuikarabati mara moja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Pamoja na kwamba, hii zahanati inakimbiliwa na wananchi wengi kiasi hiki, lakini haina jengo la maabara wala la *OPD*. Je, Serikali, haiwezi ikawasaidia wananchi hawa kwa sababu wanaitegemea sana zahanati hii?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana mamangu, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki, kwa ufuatiliaji mahiri sana wa ustawi wa wananchi wa jimbo hili. Pili, ninampongeza sana daktari wa zahanati hii ya Kalemawe kwa kufanya kazi nzuri na kuwezesha wananchi wengi kufurahia huduma ya zahanati hiyo. Huo ndiyo wito wa Serikali na ndiyo

maelekezo ya Serikali kwamba, madaktari, waganga na watumishi wote wa sekta ya afya katika maeneo yao watoe huduma bora kwa lugha nzuri na kwa ukarimu, kuhakikisha wananchi wanafurahia huduma za afya katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunauona umuhimu wa kufanya ukarabati na upanuzi wa zahanati hii, ndiyo maana tumeiingiza kwenye mpango wa zahanati 1,226 kongwe na tutatoa kipaumbele kwa ajili ya ujenzi wa jengo hilo la *OPD* na maabara kuhakikisha Zahanati ya Kalemawe inakuwa na ubora unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tunafahamu kwamba, kuna changamoto ya zahanati nyingine katika Jimbo la Same na Serikali imeendelea kutenga fedha. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, tutahakikisha katika bajeti zetu zote tunatenga fedha kwa ajili ya kuboresha zahanati hizo katika Jimbo la Same Mashariki.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deo Mwanyika.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa swali. Halmashauri ya Mji wa Njombe, Kata ya Lugenge, tuna zahanati ambayo ni ya zamani sana, lakini kwa sababu ya wingi wa watu imepitwa na wakati na tukaona ni vizuri twende kwenye kituo cha afya. Wananchi wametenga eneo, wameanza michango na mimi nimeingiza katika moja ya vipaumbele. Ni lini sasa kituo hiki cha afya kitajengwa katika Kata ya Lugenge?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kaka yangu, Mheshimiwa Deodatus Mwanyika amefuatilia sana suala la ujenzi wa Kituo cha Afya cha Lugenge. Ni kweli Zahanati ya Lugenge ni kongwe, ya siku nyingi na idadi ya wananchi imeongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa eneo la Lugenge kwamba ni dhamira ya Serikali pale ambapo kuna eneo la kutosha, lakini kuna vigezo vile vingine vya kituo cha afya, kupeleka fedha kwa awamu ili kuunga mkono juhudi za wananchi katika ujenzi wa vituo vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza wananchi wa Lugenge kwa kutenga eneo na kuanza michango. Ninampongeza Mheshimiwa Mbunge, na ninamhakikishia, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, tutaweka utaratibu wa kibajeti kuhakikisha tunaunga mkono ujenzi wa kituo hicho cha afya ikiwa tutajiridhisha tu na vigezo vile ambavyo ni kipaumbele cha kuwa na kituo cha afya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Japhael, nilikuona.

**MHE. JAPHAEL M. LUFUNGIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana. Zahanati ya Nsungwa inalo jengo la mama na mtoto, pamoja na Zahanati ya Imala. Wananchi wamechangishana wamejenga majengo ya mama na mtoto, ili akinamama waweze kujifungua kwa usalama. Je, lini Serikali itaunga mkono juhudi za majengo hayo kuhakikisha yanakamilika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Tunafahamu kwamba, katika Jimbo la Ulyankulu anakotoka Mheshimiwa Mbunge, ziko zahanati ambazo zinahitaji fedha ya Serikali kwa ajili ya ukamilishaji. Katika kila mwaka wa fedha kuanzia mwaka 2021 mpaka sasa 2025/2026, Serikali imekuwa ikitenga fedha, shilingi milioni 50, kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya zahanati na majengo mengine ambayo wananchi wamechangia nguvu zao ili kuhakikisha kwamba, zahanati hizo zinakamilishwa na kuanza kutoa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutahakikisha katika bajeti zetu

ambazo tunatenga fedha kwa ajili ya kumalizia vituo na zahanati hizo, tutapeleka fedha katika Jimbo la Ulyankulu, kwa ajili ya kumalizia zahanati hizo alizozitaja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sumry, nimekuona.

**MHE. HAIDARY H. SUMRY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa, Serikali imekuwa ikijenga vituo vya afya na hospitali kwa gharama zote ambazo zinagharamiwa na Serikali, kwa nini sasa kwenye hizi zahanati Serikali isilete fedha ya kutosha na kuondoa adha kwa wananchi wetu, ile ya kuchangia maboma ambayo inapelekea kuchelewesha miradi ya hizi zahanati kukamilika?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliweka mpango ambao unajulikana kama Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi, ambao mpango huu ni shirikishi, kwa maana ya wananchi ili kuwapa *ownership* ya vituo vyao, na pia Serikali inachangia nguvu za wananchi katika ukamilishaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili tangu mwaka 2017 mpaka sasa limeleta mafanikio makubwa sana kwa wananchi kuanza shughuli za uchangiaji na kujenga maboma mpaka hatua ya lenta na Serikali kuchangia kiasi cha shilingi milioni 50 au zaidi ili kuhakikisha kwamba yale maboma yanakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa, Serikali itaendelea kuhakikisha inajenga hospitali za Halmashauri maeneo ambapo hakuna hospitali, tunakarabati na kujenga vituo vya afya, lakini wananchi tunaendelea kuwatia shime kuendelea kujitolea kuchangia na Serikali itawaunga mkono kukamilisha vituo hivyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge, kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu,

TAMISEMI. Tunaendelea sasa na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Ado Shaibu Ado, Mbunge wa Tunduru Kaskazini, aulize swali lake.

Na. 365

**Ujenzi wa Barabara ya Nachingwea – Tunduru**

**MHE. ADO S. ADO** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa barabara ya lami kutoka Nachingwea hadi Tunduru kupitia Vijiji vya Ngapa na Mindu utaanza na kukamilika?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Ado Shaibu Ado, Mbunge wa Tunduru Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa barabara ya Nachingwea hadi Tunduru ambapo sasa kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Daraja la Ngapa lililopo katika barabara ya Mindu – Ngapa eneo lenye urefu wa kilometa 39.76 imekamilika. Aidha, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii kuanzia Mindu – Ngapa – Kilimarondo hadi Nachingwea yenye urefu wa kilometa 153 inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kukamilika kwa usanifu, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sikudhani Chikambo.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Upembuzi yakinifu ni wa muda mrefu sana. Huu upembuzi ninakumbuka toka nikiwa Mbunge wa Viti Maalum 2015 - 2020 haujakamilika. Nilitamani kujua huu upembuzi yakinifu utakamilika lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Ile barabara ni muhimu sana, ni barabara ambayo inaunganisha Mkoa wa Ruvuma na Mkoa wa Lindi, na kauli ya Serikali ni kuhakikisha barabara hizi ambazo zinaunganisha mikoa zinajengwa kwa kiwango cha lami. Natamani kujua, ni lini sasa hii barabara itakamilika? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa mpango ambao upo, tunategemea hii barabara itakamilika katika mwaka wa fedha ujao kwa maana ya kukamilisha usanifu kwa barabara hii yenye urefu wa kilometa 153. Pia nimkumbushe Mheshimiwa Mbunge kwamba katika hii barabara kuna eneo ambalo lilikuwa ni la *TARURA,* ambalo sasa limepandishwa hadhi kuja *TANROADS*. Kwa hiyo, barabara inasanifiwa yote ili iweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba barabara zote ambazo zinaunganisha mkoa na mkoa zinatakiwa ziwe za lami, lakini tutaendelea kwa awamu kwa sababu ni kweli kwamba bajeti hairuhusu kujenga barabara zote kwa pamoja, lakini tutaenda kwa awamu, na ndiyo maana tumeshaanza kuisanifu ikiwa ni maandalizi ya kuijenga kwa kiwango cha lami, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe na Mheshimiwa Dkt. Christina ajiandae.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Machame - Uswaa, upande wa Kalali - Uswaa, daraja la Kikafu, mkandarasi alishapewa kazi ya kujenga daraja na kumalizia lami pande hizi zote mbili. Akafanya *mobilization,* lakini mpaka sasa hivi hajaonekana *site*. Hali hiyo hiyo iko kwenye daraja la Makoa ambapo Mkandarasi amefanya kazi, lakini hajamalizia kuweka lami pande zote mbili, na sasa linaendelea kuchimbika na kuharibika. Je, lini wakandarasi hawa watarudi *site*?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba huyu mkandarasi alikuwa amesimama, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa Jimbo lake kwamba tayari ameshalipwa fedha yote ambayo alikuwa anaidai Serikali, na tunavyoongea sasa hivi, yupo anafanya *mobilization*, tayari vifaa vyote kwa maana ya daraja la Kikafu viko *yard*, tumekwenda kukagua, anavyo. Kwa hiyo, tuna uhakika hili daraja litakwenda kukamilika ikiwa ni pamoja na zile *approach roads* zake ambazo anatakiwa azijenge, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava atamalizia Mheshimiwa Fadhili Liwaka.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Barabara inayotoka Mwanangwa – Misasi – Salawe - Solwa mpaka Kahama, inaunganisha Mikoa miwili, Mkoa wa Mwanza na Shinyanga; pia inaunganisha Wilaya tatu za Misungwi - Shinyanga na Wilaya ya Kahama; inaunganisha pia majimbo manne. Ni lini itajengwa kwa kiwango cha lami? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii tayari imeshafanyiwa usanifu na tunavyoongea sasa hivi barabara hiyo ina mkandarasi, japo tumeanza kwa awamu, kilometa tatu tumeanza kuzijenga, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fadhili Liwaka.

**MHE. FADHILI A. LIWAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia swali la msingi la Mheshimiwa Ado Shaibu kwa barabara inayotoka Nachingwea kwenda Tunduru, moja kati ya jukumu la barabara hizi ni kuhakikisha kwamba zinapitika wakati wote wakati maandalizi ya kuwa barabara za lami zinaandaliwa. Je, ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba barabara hii inapitika katika kipindi chote?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ninajibu swali la nyongeza la aliyeuliza swali, nilisema hii barabara ni kweli inatoka Mkoa wa Lindi kwenda Mkoa wa Ruvuma, lakini tukumbuke hii barabara ilikuwa inaunganishwa pia kutoka Lindi kwenda Ruvuma, hapo katikati kuna barabara ambayo pia inahudumiwa na wenzetu wa TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi wakati tunaifanyia usanifu, nitumie nafasi hii kumweleza Meneja wa Mkoa wa Lindi na Ruvuma wahakikishe kwamba barabara hizi zinapitika kwa kipindi chote wakati tunaendelea na usanifu, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha tunafanya maandalizi ya kujenga sasa lile daraja la pale Ngapa ambalo usanifu tumeshaukamilisha, ambalo hasa ndiyo changamoto, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge kutoka Wizara ya Ujenzi. Sasa tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo, aulize swali lake.

Na. 366

**Ujenzi wa Skimu za Umwagiliaji**
**Bonde la Umba – Lushoto**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Skimu nne za umwagiliaji katika Bonde la Umba kama ilivyoahidiwa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imekamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Skimu nne za umwagiliaji za Kitivo, Kituani Mwenzae, Kwemgiriti na Mnazi katika Bonde la Umba. Skimu hizo zimejumuishwa kwenye

mpango wa ujenzi wa miradi ya umwagiliaji kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ili kuhakikisha kilimo cha umwagiliaji kinaimarika kwa lengo la kuchangia, kuongeza tija na uzalishaji wa mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mabwawa mawili ya Kitivo na Mnazi umekamilika na wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wamepatikana. Kukamilika kwa miradi hiyo kutanufaisha wakulima zaidi ya 3,000 waliopo vijiji vya Mng'aro, Mazinde na Kikumbi katika Kata ya Mng'aro, Langoni A, Langoni B, Mkongoi, Kiwanja na Kwemkwazu (Mnazi) pamoja na Lunguza na Kivingo eneo la Lunguza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa, Serikali imekamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na wa haya mabwawa mawili ya Kitivo na Mnazi, na Serikali imekiri kwamba wakandarasi wamepatikana, sasa ninataka kufahamu, na pia wananchi wa maeneo husika wanataka kufahamu, ni lini wakandarasi watafika katika maeneo ya mradi na kuanza kazi rasmi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Skimu ya Kituani Mwenzae ujenzi ulianza kwa maana ya kwenye eneo la banio, lakini mifereji ya usafirishaji maji, bado mifereji ya matupio ya maji kwenye mashamba na ilianza kwa fedha ya msaada wa *JICA* kutoka Japani. Ni lini Serikali sasa itamalizia kipande kilichobaki ambacho kimetelekezwa kwa kipindi kirefu?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimpongeze Mheshimiwa Shangazi kwa maswali ya msingi ambayo amekuwa akiyafuatilia katika Jimbo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimthibitishie jambo moja kwamba, katika bwawa la Kitivo na Mnazi, ni kweli tumeshakabidhi wakandarasi. Wanachosubiri sasa hivi ni kwamba tumeshapeleka

maombi ya fedha kwa ajili ya malipo ya awali na tunasubiri baada ya hayo majibu ya fedha za malipo ya awali zitakapokuwa zimefika, wale wakandarasi watafika mara moja katika eneo lako. Kwa hiyo, hiyo ndiyo hatua ambayo tuko mpaka sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Kituani Mwenzae ni kwamba, eneo hili ni kweli lilijengwa kwa msaada wa fedha za *JICA* lakini kutokana na hali ya mafuriko katika lile eneo, Tume ya Umwagiliaji imeamua ku-*redesign* upya ule mradi ili sasa tuweze kukabiliana na ile changamoto iliyopo. Kwa hiyo, tukishamaliza kufanya *design* ya mradi, maana yake hatua inayofuata sasa ni kutafuta mkandarasi ili ajenge kulingana na *standard* za wakati huu uliopo, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, ajiandae Mheshimiwa Asia Halamga, maswali mafupi ya nyongeza.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa, Mkandarasi atakayejenga mradi wa Arusha Chini uliopo kata ya Chawi, mradi ambao utawafaidisha Kata ya Kitaya na Kiromba ameshapatikana, lakini utekelezaji bado haujaanza, je, ni lini mkandarasi huyo ataanza kazi ya ujenzi wa mradi huo?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninampongeza Mheshimiwa Chikota, na bahati nzuri jambo hili alishafika ofisini wiki iliyopita na niwaeleze tu wananchi wake kwamba kama nilivyomjibu Mheshimiwa Shangazi kwamba pamoja na mradi huu wa Arusha Chini ni miongoni mwa miradi ambayo tumeiombea fedha katika Wizara ya Fedha kwa ajili ya yale malipo ya awali, na Wizara ya Fedha bahati nzuri walishatoa *commitmen*t kwetu, nafikiri zile fedha zitakapoingia, mkandarasi yule atalipwa na ataanza ile kazi mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, awathibitishie tu wananchi wake kwamba Serikali itafanyia kazi mradi wake na utakamilika kama ambavyo tumepanga, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asia Halamga, ajiandae Mheshimiwa Nuru Issa Kashakari.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kata ya Endasiwold, Kijiji cha Garbapi, tayari upembuzi yakinifu umeshafanyika. Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa skimu hii ya umwagiliaji yenye umuhimu mkubwa kwa wananchi wa Kata ya Endasiwold pamoja na wananchi wa Jimbo la Hanang?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Vilevile ninampongeza Mheshimiwa Halamga kwa swali lake la msingi. Nimthibitishie tu Mheshimiwa kwamba kwenye kata hiyo ya Endasiwold ni kweli ule mradi *feasibility study* imeshakamilika na ambacho tunakifanya sasa hivi ni *designing* kwa maana ya ku-*design* ule mchoro wa mradi, na baada ya hapo ule mradi utatangazwa kwa ajili ya kupata mkandarasi kwa ajili ya ujenzi, na ndiyo hatua ambayo tuko sasa hivi, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nuru Kashahari atamalizia Mheshimiwa Sylvia Sigula.

**MHE. NURU I. KASHAKARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Wilaya ya Uvinza, ilikuwa na vijiji vitatu ambavyo vilikuwa na skimu, lakini skimu hizi zimekufa na zimechukua mabilioni ya fedha na mpaka sasa hivi skimu hizi hazifanyi kazi. Je, ni lini Serikali itakamilisha skimu hizi ili ziweze kuwasaidia wananchi? Kwa mfano, Skimu ya Kijiji cha Nyanganga, Mgambazi na Kalia, ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba, moja ya maelekezo ambayo Mheshimiwa Rais alitupatia, kuna miradi mingi ambayo ilikuwa inajengwa awali na wakati ule miradi mingi Serikali ilikuwa inapeleka fedha na ilikuwa inasimamiwa katika ngazi za chini, na mingi ilikuwa haina ile

michoro, ama *design* za kisasa. Kwa hiyo, maelekezo ambayo tulipatiwa ni kufanya mapitio upya na kutengeneza michoro upya ili kuhakikisha kwamba ile miradi inakuwa na *standard* za kisasa, yaani sasa hivi tusifanye mambo kwa kukisia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni pamoja na hii miradi ambayo Mheshimiwa Mbunge ameainisha, ikiwemo mradi wa Nyanganga. Ni kwamba ipo katika hiyo hatua ya mapitio kwa ajili ya kutengeneza *design* upya, na baada ya hapo tutangaze kwa ajili ya kupata mkandarasi kwa ajili ya ujenzi. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sylvia Sigula.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Tunaishukuru Serikali kwa kutuletea mradi wa umwagiliaji katika Kata ya Ilemba wenye thamani ya shilingi bilioni 21, lakini mradi ule ulipaswa kuwa umekamilika tangu mwaka 2024, na hivi sasa tunavyoongea, mradi uko 40% tu, na katika hizo shilingi bilioni 21 mpaka sasa tumepokea shilingi bilioni tatu tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Ilemba wamekata tamaa. Je, ni lini hasa fedha zitakuja ili mradi ule ukamilike uweze kuwanufaisha wananchi wa Ilemba?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Sylvia kwa swali la msingi, na bahati nzuri hili swali amekuwa akiliuliza mara kwa mara Bungeni, na tumekuwa tukimjibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya changamoto kubwa ambayo ilikuwa inachelewesha mradi wa Ilemba ilikuwa ni eneo lile kukumbwa na mafuriko hususan wakati wa mvua, kazi nyingi zilikuwa zikisimama. Pili, ni kweli kwamba tunakiri kwamba tulichelewesha kidogo kumlipa fedha, kutokana na changamoto zikiwemo zile za uchaguzi mkuu ambao uliopita, lakini tumemwongezea mkandarasi muda, na fedha atapokea, kwa sababu kuna *commitment* ya Wizara ya Fedha ya kuilipa Tume

shilingi bilioni 25 kila mwezi, ili kuhakikisha ile miradi yote iliyoanza inakwenda kukamilika kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwenye zile *commitment,* tutatoa fedha na tutamsimamia mkandarasi ili aweze kumaliza kwa wakati, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Yagi Maulid Kiaratu, Mbunge wa Singida Mjini.

Na. 367

**Utekelezaji wa Miradi ya Umwagiliaji Katika Jimbo la Singida Mjini**

**MHE. YAGI M. KIARATU** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza kutekeleza miradi ya umwagiliaji katika Jimbo la Singida Mjini ili kuongeza uzalishaji wa kilimo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Yagi Maulid Kiaratu, Mbunge wa Jimbo la Singida Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imetambua maeneo mbalimbali yanayofaa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji katika Halmashauri ya Singida Mjini ikiwemo skimu za Kisasida, Uhamaka na Unyamikumbi ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utambuzi huo, Wataalam wa Tume kwa kushirikiana na wataalam wa Halmashauri na wakulima wamefanya tathmini katika maeneo yanayotarajiwa kuendelezwa yakiwemo Kisasida (hekta 300), Uhamaka (hekta 150) na Unyamikumbi (hekta 96) ili kuainisha mahitaji ya miundombinu inayofaa kwa ajili ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kupitia mpango wa uchimbaji wa visima, Serikali imechimba kisima katika bonde la Uhamaka ili kuwezesha upatikanaji wa maji ya uhakika kwa ajili ya umwagiliaji. Kisima hicho kinanufaisha wakulima zaidi ya 200 katika maeneo ya vitongoji vya Mumbivi na Msimii katika Kata ya Uhamaka pamoja na vitongoji vya Mamise na Nkuku katika Kata jirani ya Mandewa katika bonde hilo la kilimo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yagi Maulid Kiaratu.

**MHE. YAGI M. KIARATU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Waziri ameyatambua maeneo, ameyataja Uhamaka, Kisasida na Unyamikumbi, lakini ninaomba nimwongezee Mpamaa, Mwankoko na Kisaki, nayo yana mabonde mazuri sana. Katika majibu yake, Mheshimiwa Waziri, niungane naye, nakiri kisima kimechimbwa, lakini kisima hicho hakijawekewa miundombinu ya kuweza kufanya kazi mpaka sasa. Je, ni lini Serikali itakamilisha kazi hiyo ikiwemo kuyakumbuka hayo maeneo mengine kwa sababu skimu za umwagiliaji ni chanzo kizuri cha ajira, kukuza uchumi, na kuongeza lishe katika maeneo husika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Katika kijiji alichokitaja cha Kisasida walibahatika kupata mradi mkubwa wa umwagiliaji wenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni 800. Mradi huo ulianza mwaka 2011 na ukakamilika mwaka 2014, lakini jambo la kusikitisha mradi huo wenye thamani ya fedha hizo kwa wakati huo mpaka leo haujaweza kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitamani Mheshimiwa Waziri anipe jibu hapa, ninatamani Mheshimiwa Waziri akubali mimi na yeye twende *site* ili tukaone changamoto za mradi huo apate nafasi nzuri ya kuutathmini na kuutatua ili wananchi wa eneo hilo wapate kufanya kazi. Ninaomba majibu ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo la mwanzo, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimpongeze Mbunge wa Singida Mjini, Mheshimiwa Kiaratu.

Ameeleza vizuri. Jambo moja tu nimthibitishie kwamba maeneo mengi ambayo Tume sasa hivi inachimba visima tumeanza kwa kuchimba. Hatua inayofuata, kwa sababu Tume imeshafanya *procurement* ya vile vifaa kwa ajili ya kumalizia ile miradi, *Procurement* tumeagiza vifaa vingi kutoka nchini India ambavyo ninafikiri viko njiani kufika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, vikishafika maana yake tutakwenda kumalizia katika maeneo yote ambayo tumechimba, hatutasubiri vifaa vifike ndiyo tuanze kuchimba. Kwa hiyo, sasa hivi tulichokifanya ni Tume wanaendelea na uchimbaji maeneo mbalimbali nchini na vile vifaa vikifika maana yake kutakuwa na timu ya pili ambayo itakuwa na kazi ya kuvifunga ili visima vile vianze kusaidia watu katika maeneo hayo kwa ajili ya shughuli za umwagiliaji. Kwa hiyo, hilo lipo katika hatua na litakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la Kisasida niko tayari kufika. Kama sio mimi, atafika Mheshimiwa Waziri wangu kwa sababu alikuwa na ratiba ya kufika katika Mkoa wa Singida. Vile vile, nimthibitishie tu kwamba hii ni sehemu ya ile miradi ambayo Mheshimiwa Rais alituelekeza kufanya mapitio upya na kufanya *designing* mpya ili tuweze kupata gharama halisi na kuirekebisha ili iweze kufanya kazi kwa ajili ya tija kwa wananchi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Christina Mndeme.

**MHE. CHRISTINA S. MNDEME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa Serikali imekuwa ikijenga skimu za umwagiliaji katika maeneo mbalimbali nchini ili kukuza na kuendeleza shughuli za kilimo nchini na kukuza kipato cha mkulima na kuwa na uhakika wa chakula; na kwa kuwa Serikali yetu pendwa imeshatenga fedha za ujenzi wa skimu ya umwagiliaji takribani shilingi bilioni 34 katika Kata ya Goweko iliyopo Wilaya ya Uyui, tunaishukuru na kuipongeza Serikali kwa hatua hii. Je, ni lini ujenzi wa skimu hii utaanza ili mradi huu uweze kuleta tija kwa wananchi wa Kata ya Goweko na viunga vyake?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Christina Mndeme kwa swali la msingi. Mradi wa Goweko ni miongoni mwa miradi mikubwa ambayo Wizara kupitia Tume tunaitekeleza. Ni kweli kwamba mradi wa Goweko una thamani ya shilingi bilioni 34. Tunakiri kwamba tayari tulishapata mkandarasi na tulishamkabidhi *site*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, palikuwa tu na changamoto ile ya kifedha ambayo niliieleza awali, lakini kutokana na hii *commitment* ambayo Wizara ya Fedha walitupatia, ninaamini sasa kwenye mwendelezo wa fedha zile zinazotoka kwenye ile miradi ambayo tumeelekezwa kuhakikisha inakamilika, yote ambayo tulishafikisha wakandarasi *site* ikamilike kwa wakati, mradi huo ni sehemu. Kwa hiyo, tutapeleka fedha ili mkandarasi aanze ule utekelezaji ambao tumekusudia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, nimekuona.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Ujenzi wa bwawa katika Kata ya Nyanzwa Jimbo la Kilolo tunashukuru sana Serikali tayari upembuzi yakinifu umeshafanyika. Je, ni lini sasa ujenzi utaanza, maana wananchi wa Kata ya Nyanzwa wameusubiri mradi huo kwa muda mrefu sana?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tayari tumeshafanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, hatua ambayo tuko sasa hivi Tume kupitia wataalamu wetu wa ndani na *consultant* tunamalizia ule mchoro, kwa maana ya *designing*. Baada ya kumaliza hiyo hatua ya michoro sasa tunakwenda katika hatua inayofuata kwa ajili ya kutangaza na kupata mkandarasi. Kwa hiyo, tupo kwenye hiyo hatua. Ninaamini ndani ya muda tutayamaliza kwa wakati na tutaanza ule mradi. Tunatambua mahitaji ya wananchi na Serikali itatekeleza.

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge kutoka Wizara ya Kilimo. Tunaendelea sasa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Mheshimiwa

Mwita Mwikwabe Waitara, Mbunge wa Tarime Vijijini, aulize swali lake.

Na. 368

**Uanzishwaji wa Minada ya Kimataifa ya Mifugo – Tarime Vijijini**

**MHE. MWITA M. WAITARA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanzisha minada ya Kimataifa ya mifugo katika Jimbo la Tarime Vijijini?

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Mbunge wa Tarime Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa kuboresha minada ya Kimataifa ya mifugo katika maeneo ya kimkakati ikiwemo Tarime Vijijini kutokana na uwepo wa idadi kubwa ya mifugo pamoja na ukaribu wake na mipaka ya nchi jirani, hali inayotoa fursa pana za biashara ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kuboresha mazingira ya biashara ya mifugo na kuhamasisha wafanyabiashara pamoja na wadau wote katika Jimbo la Tarime Vijijini kutumia Mnada wa mpakani wa Magena kama mnada wa Kimataifa kwa kuzingatia kuwa eneo hilo lina sifa stahiki za kijiografia na kibiashara. Katika mwaka wa fedha 2021/2022, jumla ya shilingi milioni 175.65 zilitumika kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu muhimu, ikiwemo mazizi, kipakilio, birika la maji na vyoo, ambapo ujenzi huo ulikamilika kwa 100%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inaendelea kuchukua hatua stahiki za kuimarisha miundobinu muhimu ya mnada huo ikiwemo ujenzi wa ofisi na uzio ili kuongeza ufanisi, usalama na hadhi ya mnada huu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Nimesikiliza majibu ya Serikali, ukweli ni kwamba mnada huu haufanyi kazi kwa muda mrefu na Mheshimiwa Waziri watu wake wamempa majibu ambayo siyo sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumza mifugo ya Kanda ya Ziwa, hapa Mnada wa Magena haufanyi kazi, kule Kenya Maabele wanafanya kazi. Mifugo yote ya Tanzania inapita kwenda Kenya kwa njia za panya, na hivyo tunapoteza mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, hakuna hatua yoyote ya Serikali ya kuchukua yale mazao ya mifugo ili watoto waweze kunufaika. Kwa hiyo, ninaomba kwa heshima tu Mheshimiwa Waziri, labda tufanye utaratibu mwingine kupata majibu mazuri ya eneo hilo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waitara hauna swali, Mheshimiwa Josephine Kapoma.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kumhakikishia Mheshimiwa Waitara kwamba nikitoka hapa tukae tuzungumze, halafu pia niwasiliane na wataalamu wangu tuweze kufuatilia kuhakikisha kwamba mnada huo unafanya kazi kama ilivyokusudiwa. Hatuwezi tukapoteza fedha kiasi hicho halafu taarifa zikawa kwamba mnada haufanyi kazi. Lazima twende kwenye kiini cha tatizo tujue ni kwa nini mnada huo haufanyi kazi? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Josephine Kapoma, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHINE J. KAPOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Morogoro ni kati ya mikoa ambayo ongezeko la mifugo linakua kwa kasi sana, hususan katika Wilaya za Ulanga, Malinyi na Mlimba. Sasa nilitaka kujua ahadi ya Serikali ya uboreshaji wa minada minne katika Wilaya ya Ulanga ya vijiji vya Nakafulu, Mbuga, Ikungua na Milola sambamba na ujenzi wa uzio katika minada ya Mavimba na Mbuga utaanza lini? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ni kweli Mkoa wa Morogoro una mifugo mingi kutokana na uzuri wa hali ya hewa, upatikanaji wa malisho pamoja na maji ukilinganisha na mikoa mingine. Ninapenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imeelekeza sekta zote tutekeleze miradi ambayo tayari tumeshaanza na tuikamilishe kabla ya kuanza minada mipya, na ile ambayo inahitaji maboresho tuzingatie pia upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nitoe taarifa kwamba kuna minada ya aina mbili. Kuna minada ya awali ambayo inajengwa na TAMISEMI na minada ya upili ambayo inajengwa na Wizara ya Mifugo. Kwa hiyo, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba minada hiyo ambayo inatakiwa kufanyiwa kazi chini ya Wizara ya Mifugo iweze kukamilishwa na ile ambayo iko chini ya TAMISEMI nayo pia iweze kukamilishwa. Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bahati Ndingo.

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Tuna mnada mzuri mkubwa ambao Serikali mmeshaanza kuujenga, uko pale Kata ya Utengule, Usangu – Mbarali, lakini mnada ule umesimama kutokana na kwamba bado Wizara haijapeleka fedha. Je, ni lini watakamilisha kupeleka fedha ili wananchi wa pale waanze kutumia mnada ule?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu swali la Mbunge kutoka Morogoro, tunajiandaa kuhakikisha kwamba tunatekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Rais, kwamba tukamilishe miradi yote ambayo tumeshaianza na miradi yote ambayo tumeshaianza iko katika bajeti ambayo Waheshimiwa Wabunge waliipitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Bahati kwamba nitafuatilia nihakikishe kabisa

kwamba mradi huo unakamilika kama ulivyokuwa umepangwa, na kwa mujibu wa maelekezo ya Mheshimiwa Rais.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge na maelezo ya ziada ya mtoa swali la msingi, Mheshimiwa Waitara. Tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Enock Zadock Koola, Mbunge wa Vunjo, aulize swali lake.

Na. 369

**Hitaji la Visima Virefu na Mabwawa – Vunjo**

**MHE. ENOCK Z. KOOLA** aliuliza:-

Je, kwa nini *MUWASA* na *RUWASA* wasichimbe visima virefu na mabwawa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi yanayoathiri wananchi wa Vunjo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Enock Zadock Koola, Mbunge wa Jimbo la Vunjo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kuwa wananchi wote nchini wanafikiwa na huduma ya majisafi na salama kupitia vyanzo vya maji vya uhakika vikiwemo mabwawa na visima virefu. Kwa sasa huduma ya majisafi na salama kwa wananchi wa Jimbo la Vunjo inatolewa kupitia vyanzo vya chemchemi tano pamoja na visima vinne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha zaidi upatikanaji wa maji katika jimbo hilo, Serikali imekamilisha uchimbaji wa visima vitatu vya Uchira, Mabungo Koresa na Miwaleni, ambapo kwa pamoja vina uwezo wa kuzalisha maji lita milioni 3.2 kwa siku. Aidha, katika hatua nyingine Serikali kupitia Bodi ya Maji Bonde la Pangani imetafiti na kupata vyanzo vipya vya chemchemi katika vijiji vya Lyasongoro, Kyerio pamoja na Kilamboro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa Serikali kwa mwaka 2026/2027 ni kujenga miundombinu ya usambazaji maji kwa visima vilivyochimbwa na kupata maji ili kufikisha huduma ya maji safi na salama kwa wananchi wa Jimbo la Vunjo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Enock Zadock Koola.

**MHE. ENOCK Z. KOOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nilikuwa na maswali mawili ya nyongeza. La kwanza, kwa kuwa hicho kisima ambacho kiko Kitongoji cha Miwaleni, Kijiji cha Yamu Makaa, Kata ya *KV* kusini ilikuwa imetengewa fedha shilingi milioni 795 mwaka huu wa fedha lakini mpaka sasa haijafika, je, ni lini Serikali inaweza ikahakikisha kwamba hizo fedha zitaingia ndani ya mwaka huu wa fedha ili kukamilisha huo mradi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa visima vyote ambavyo vimetajwa vipo kwenye kata moja ya Kirua Vunjo Kusini; na kwa kuwa jimbo letu bado tuna Kata za Makuyuni, Kata za Kahe Mashariki na Kahe Magharibi ambazo zina changamoto kubwa ya upatikanaji wa maji, je Serikali ipo tayari kuweza kujenga visima kwenye kata hizo husika?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anayoifanya, hasa kwa kuwatetea akina mama wapate huduma ya majisafi na salama. Ninakumbuka pia nilifanya ziara katika jimbo lake, tuliongea mengi na tayari mengine yameshaanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama katika Jimbo la Vunjo mpaka sasa ni 88.7% na katika vijiji vya Vunjo ambavyo ni 86, tayari wana huduma ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua sera yetu ya mwaka 1991, toleo la mwaka 2002, linasisitiza kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma ya majisafi na salama na ya kutosheleza ndani ya umbali wa meta 400.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipengele cha kutosheleza ndipo ambapo sasa Mheshimiwa Mbunge ninajua anaendelea kufanyia kazi kuhakikisha kwamba maji yawe toshelevu na endelevu. Kwa muktadha huo, kupitia bajeti ya 2026/2027 ambayo tumepitishiwa, tutaenda kutumia programu ya vijiji 1,575 kuhakikisha kwamba tunaenda kuboresha huduma ya majisafi na salama, hasa katika hili eneo la Makuyuni na maeneo mengine ambayo Mheshimiwa Mbunge ametaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika swali la pili, kuhusu mkandarasi, tunafahamu kwamba *RUWASA* wameshaleta mabomba na mkandarasi ameshachimba mitaro, kazi iliyobaki ni mkandarasi kulipwa. Serikali imejizatiti kuendelea kulipa hati za madai za wakandarasi ili kuhakikisha kwamba wanaendelea kukamilisha miradi ili iweze kutoa matokeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, kwenye hili tutasubiri mkandarasi awasilishe hati yake ili tuweze kumlipa na aweze kukamilisha mradi huu. Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana.

**MHE. DKT. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa suala la maji, hususan visima virefu na mabwawa ni suala mtambuka nchi nzima, na bado tunazo shule za msingi, za sekondari, na zahanati ambako watoto wa kike na wakina mama wanajifungua hatuna visima virefu, je, kwa mujibu wa sera, Wizara haioni sasa wakati umefika kuhakikisha suala la visima virefu ni suala ambalo linapatikana katika shule zetu za msingi na zahanati; na haioni kama ipo haja ya kuanzia na Mkoa wa Njombe kwa sababu ndiko vyanzo vya maji vinatoka katika milima ya *Livingstone* hadi tunapeleka *Mwalimu Nyerere hydroelectric power*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali haioni ipo haja ya kuhakikisha shule zote zina visima virefu na zahanati ambako akina mama wanajifungua?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru na nimpongeze Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana, Mbunge kutoka Mkoa wa Njombe kwa kazi nzuri sana na kwa swali zuri ambalo linagusa sera yetu ya maji, ambapo ndiyo maelekezo na uelekeo wa Serikali ya Awamu ya Sita ya kuhakikisha kwamba Watanzania, cha kwanza kabisa maji wayapate katika umbali usiozidi meta 400. Pili, maji yawe safi, salama, toshelevu na endelevu. Tatu, tuhakikishe kwamba wakina mama na watoto hawatumii muda mwingi kwenda kutafuta maji. Watoto waende shule, akina mama wafanye shughuli za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha huo, kwa kubainisha sasa vyanzo vya maji, tunaangalia pale ambapo tunafanya *cost benefit analysis* kuona kama bwawa litafaa ama kisima kitafaa ama kuna chanzo kingine cha mto, *surface water*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukishabaini kwamba njia ipi itakuwa ni rahisi zaidi, Serikali inapeleka fedha na kuwekeza na kuhakikisha kwamba tatizo la upatikanaji wa maji linakuwa limetatuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, Njombe tunaipatia kipaumbele kama ilivyo kwa wananchi wengine katika maeneo mengine, ambayo ni maelekezo na falsafa ya Mheshimiwa Rais ya kumtua mama ndoo kichwani. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yahya Mhata, nilikuona.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Jimbo la Nanyumbu kuna Kata inaitwa Maratani. Tunaishukuru Serikali kwa kutuletea mradi wa maji tangu kipindi kilichopita. Hata hivyo, kwa bahati mbaya sana, mkandarasi amefanya kazi kubwa ili kuhakikisha kwamba vijiji vyote vya Kata ya Maratani vinaunganishwa katika ule mradi mkubwa wa bwawa ambalo liko pale Maratani. Je, ni lini mkandarasi huyu atamaliziwa fedha zake ili arudi *site* na akamilishe mradi ule ambao wananchi wanauhitaji sana?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninamshukuru sana kaka yangu Mheshimiwa Mhata, Mbunge wa Nanyumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakiri kweli kabisa huu mradi umeshaanza kutekelezwa na mkandarasi anasuasua. Pia, ninafahamu kabisa kwamba huu mradi ulikuwa kwenye makaratasi, umetolewa kwenye makaratasi na umeingia kwenye utekelezaji. Tunafahamu kwamba tutaongeza msukumo wa kupeleka fedha na hasa huyu mkandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kumwahidi Mheshimiwa Mbunge, tutamwita mkandarasi na Mheshimiwa Mbunge, tutakaa, tutapanga *milestone* za namna ambavyo tutaanza kumlipa kwa awamu ili ahakikishe kwamba anaendelea kutekeleza kusudi vijiji vyote ambavyo vinaunganishwa katika mradi huu visije kupata changamoto endelevu ya upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama. Tunamwahidi hilo tutalifanyia kazi. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Eng. Chacha Mwita Wambura, Mbunge wa Geita Mjini, aulize swali lake.

Na. 370

**Miradi ya Maji Kata za Geita Mjini**

**MHE. CHACHA M. WAMBURA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha Miradi ya Maji Kata za Bulela, Shiloleli, Bung'wangoko, Nyanguku na Ihanamilo Geita Mjini?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Chacha Mwita Wambura, Mbunge wa Jimbo la Geita Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipaumbele cha Serikali ni kuhakikisha inakamilisha utekelezaji wa miradi ya maji 1,206 inayoendelea nchini kote, mijini na vijijini ikiwemo Jimbo la Geita Mjini katika Mkoa wa Geita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya miundombinu inayojengwa katika miradi inayoendelea katika Kata za Bulela, Shiloleli, Bung'wangoko, Nyanguku na Ihanamilo ni pamoja na ujenzi wa nyumba ya mitambo *(pump house)*, ujenzi wa matanki matatu yenye jumla ya ujazo wa lita 245,000 sanjari na ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 26.49.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hiyo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji ambapo inatarajiwa kukamilika ndani ya mwaka wa fedha 2026/2027. Serikali itaendelea kutoa kipaumbele kwa miradi hiyo kwa kupeleka fedha za utekelezaji kadiri zinavyopatikana ili iweze kukamilika na kuanza kutoa huduma iliyokusudiwa ambapo tunatarajia wananchi wapatao 15,000 wa maeneo hayo watanufaika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Eng.* Chacha Wambura.

**MHE. CHACHA M. WAMBURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuuliza swali la nyongeza, lakini ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Pamoja na majibu yake mazuri, ninaomba kuuliza maswali mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii miradi ambayo tunaizungumzia hapa, ilianza kutajwa kwenye Bajeti ya mwaka 2022/2023, 2023/2024, 2024/2025, na 2025/2026. Miaka yote hii bajeti hii imekuwa ikitajwa, lakini ukiangalia miradi yote hii imekuwa ikisuasua kwa sababu hamna fedha ambayo imekuwa ikiletwa. Fedha ambayo imeletwa ni kiasi kidogo sana, kiasi kwamba imepelekea baadhi ya wakandarasi kutoka *site*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Naibu Waziri atuhakikishie kwamba, miradi hii kweli itatekelezwa? Ukiangalia hizi kata, ni kata ambazo zina changamoto kubwa sana ya maji. Kwa hiyo, tunaomba atuhakikishie hapa, miradi hii itatekelezwa? Pia, ni lini hasa kweli itatekelezwa miradi hii? Hilo swali la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Tunashukuru Serikali kuna mradi mkubwa wa miji 28 ambao unaendelea katika Mji wetu wa Geita, katika Manispaa ya Geita, lakini ukiangalia bajeti ambayo ipo, ni kwa ajili tu ya zile kata za pale mjini, zile kata za pembeni kama Mgusu, Shiloleli na Nyanguku na kata nyingine, bado hiyo bajeti haijawahi kutengwa. Sasa ninaomba kujua, ni lini hasa Serikali itatenga bajeti kwa ajili ya utandazaji wa bomba ili hizi kata na zenyewe ziweze kunufaika na huu mradi mkubwa ambao Serikali inatengeneza? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana kaka yangu kwa kazi kubwa sana na kwa kasi aliyoanza nayo katika Jimbo la Geita Mjini. Anafanya kazi nzuri sana na tunashirikiana naye na tunapoenda kwenye ziara ya kukagua miradi, amekuwa akitupatia ushirikiano mkubwa sana. Tunamshukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaungana na Mheshimiwa Mbunge, suala ambalo ameliongelea kuhusu miradi hii kusuasua, tunao Mradi wa Bung'wangoko ambapo ni kweli kabisa mkandarasi alikuwa ameshalipwa shilingi milioni 264 kati ya shilingi milioni 305, lakini bado mradi ulikuwa 65%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kumjulisha Mheshimiwa Mbunge, Mkandarasi huyu tumeshamfukuza, hayupo *site* na tayari tumechukua jukumu hilo kama Serikali kuhakikisha kwamba mradi huo tunaenda kuutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika Kata za Bulela, Nyaseka pamoja na Shiloleli, mradi huu una gharama ya shilingi milioni 345 ambapo hivi sasa Serikali imeshapeleka shilingi milioni 100 na

mradi uko 35%. Ninakutoa hofu, tutaendelea kuweka msukumo kwa mkandarasi kufanya kazi kwa haraka ili aweze kuleta *certificate* ili tuweze kumlipa ili aweze kuhakikisha kwamba mradi unakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunao mradi wa visima vitano ambapo katika *program* ya visima 900, Jimbo la Geita tulichimba visima vitano, kimoja tukakosa maji, vinne tukapata, viwili tukaendeleza miundombinu na wananchi wanapata huduma ya majisafi na salama. Hivi vingine viwili mkandarasi bado anadai, tukishamalizia fedha na vyenyewe vinakuwa vimekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la miji 28, na kwenye hili ninampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uwekezaji mkubwa sana wa mradi wa miji 28 Geita. Zaidi ya shilingi bilioni 124 imewekezwa katika mradi huo. Ninakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge, pamoja na kwamba mradi umefikia 80%, kuna maeneo ambayo hayakuwa sehemu ya mtandao wa bomba ambapo mradi ukishakamilika kwamba yaweze kupokea. Maeneo hayo ni pamoja na eneo la Mgusu kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amesema, Nyanguku, lakini pia na Ihanamilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya maeneo yote sasa Serikali kupitia Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Geita, wameingia mkataba, wamesaini mkataba na Mtaalamu Mshauri kwa ajili ya kufanya Usanifu katika kata zote ambazo hazina mtandao ikiwemo hizi kata ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja. Ameanza kazi mwezi wa Tatu, na tunatarajia mpaka tarehe 30 Mei, Mtaalamu Mshauri atakuwa amekamilisha kazi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutatafuta fedha kwa ajili ya kuanza sasa kuweka mabomba ili mradi ambao umefikia 80% unapokamilika, na wananchi wawe wanaanza kupata maji, kwa sababu bomba zitakuwa tayari zimeshawekwa. Ninamtoa hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali tunaendelea kuhakikisha kwamba tunaliangalia kwa umakini sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yustina Rahhi nilikuona.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kata ya Dosidosi iliyoko wilayani Kiteto ina changamoto kubwa sana ya upatikanaji wa maji. Je, ni lini Serikali itawasaidia wananchi hao kupata majisafi na salama?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kata hii ina changamoto. Pia, katika Jimbo la Kiteto, ni jimbo ambalo lina ukame na ndiyo maana Serikali inaendelea kufanya kazi ya kutafuta fedha ili tuboreshe zaidi mabwawa ambayo yataweza kutusaidia. Pia, kwenye *program* yetu ya visima kwa vijiji 1,575 katika awamu ya kwanza kuna kata na vijiji vyake tunaenda kuviingiza kwenye bajeti ya mwaka 2026/2027 ili kuhakikisha wanapata huduma ya majisafi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watapataje? Kwa chanzo cha kisima kwa maana ya *underground water,* ama kwa *surface water*, ama kwa mabwawa, hilo tunaliacha kwa wataalamu. Lengo ni kwamba wananchi hawa wapate huduma ya majisafi na salama. Ninamtoa hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaipatia kipaumbele kata hiyo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameielezea.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mfaume, swali fupi la nyongeza.

**MHE. ZUBERI Y. MFAUME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uendelezaji wa miradi ya maji, watu wa vyanzo vya maji katika Jimbo la Morogoro Kusini wamechukua maeneo katika Kata ya Mngazi miaka mitatu sasa, lakini bado hawajawalipa wananchi fidia ili na wao waendelee na kazi ya uchimbaji wa visima virefu pamoja na mabwawa. Je, ni lini sasa fidia hizi zitalipwa kwa wananchi ili miradi hii nayo iweze kuendelea?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miradi ya maji, kwanza ninamshukuru sana Mheshimiwa Mbunge

wa Morogoro Kusini kwa kuligusia hili suala. Tunayo maeneo ambayo huwa tunalipa fidia na tunayo maeneo ambayo tunaomba wananchi tushirikiane nao kwa sababu suala la kupata huduma ya majisafi na salama na ya kupata vyanzo, ni jambo ambalo ni la Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamtoa hofu, nitawasiliana na wataalamu wetu, tuweze kuona katika maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyagusia kama yapo katika yale makundi ya kulipwa fidia ili tuhakikishe tuone kwamba uthamini umeshafanyika. Kama kutakuwa na orodha ya wananchi wanaostahili kulipwa, basi tutahakikisha kwamba wananlipwa, lakini kama ni maeneo ambayo huwa tunayachukua kwa ushirikiano na wananchi, basi tutaendelea kutoa elimu kwa wananchi ili wajue namna ambavyo tunatakiwa kushirikiana na Serikali katika upatikanaji wa vyanzo vya uhakika ili waweze kupata huduma ya majisafi na salama.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge kutoka Wizara ya Maji. Tunamalizia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Tarime Mjini, aulize swali lake.

Na. 371

**Hitaji la Gari la Zimamoto Tarime**

**MHE. ESTHER N. MATIKO** aliuliza:-

Je, lini Wilaya ya Tarime itapata gari la Zimamoto la kisasa?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Tarime Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na jitihada za kuliimarisha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa kulipatia vitendeakazi mbalimbali kwa ajili ya kutoa huduma za uokozi kwa wananchi. Katika Wilaya ya Tarime Mjini, Serikali kupitia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji imeshapeleka gari jipya la zimamoto na uokoaji aina ya *IVECO* 189 lenye ujazo wa maji lita 5,000 na lita 500 za *foam*. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na ninapenda pia kuishukuru Serikali kwa kweli kwa kutuletea gari la kisasa la zimamoto. Kwa kuwa Jeshi la Zimamoto la Tarime, Rorya linahudumia Wilaya sita za Kipolisi, na kwa kuwa hawana ofisi, walipewa jengo tu ambalo lilikuwa la Idara ya Elimu na Halmashauri ya Mji wa Tarime ambalo ni chakavu kabisa, na kwa kuwa sasa hivi Mkurugenzi ameomba wapishe ili waweze kujenga jengo jipya, hawana ofisi, na kwa kuwa wameshapeleka hati Makao Makuu yenye taktibani *square meter* 1,800; ni lini sasa Serikali itaona haja ya kupeleka fedha kwa udharura wake ili Jeshi la Zimamoto liweze kujengewa jengo jipya na lenye hadhi la Kipolisi Tarime, Rorya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kama nilivyosema awali, Jeshi la Zimamoto linahudumia Wilaya sita za Kipolisi kwa maana ya Sirari, Nyamwaga, Kinesi, Ishirati, Utegi na Tarime Mjini, na tunajua kazi ya Jeshi la Zimamoto; pale tuna migodi, tuna Mpaka wa Sirari, kuna miji yetu imekua sasa, majengo mapya ya kisasa kabisa na yana majanga mbalimbali. Sasa inapotokea dharura, Jeshi la Zimamoto linatumia pikipiki kwenda kufanya *service*. Serikali haioni kwamba kuna haja sasa walau kwa kuanzia kupeleka gari moja ambalo litasaidia kutoa huduma kwa wananchi? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutumia fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko kwa jinsi ambavyo anafuatilia kwa karibu na kusimamia wananchi wake kuhakikisha kuwa wapo

salama na hasa kwa ajili ya upatikanaji wa huduma ya zimamoto na uokoaji katika Mkoa wa Mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninakiri kwamba kwa sasa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji katika Wilaya ya Tarime Mjini linatumia ofisi za Halmashauri ya Wilaya. Ninakiri hilo, lakini wakati huo tayari kukiwa na jitihada za kuhakikisha kwamba Serikali inapata kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Zimamoto na Uokoaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hilo, Jeshi limeshapatiwa kiwanja chenye Na. 798 *Block G* chenye ukubwa wa *square meter* 1,896 kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameeleza. Hata hivyo, kwa sasa, kwa upande wa Mkoa wa Mara, tunafahamu kwamba huduma za zimamoto na uokoaji kati ya wilaya sita zilizopo, zinatolewa kwenye wilaya tano tu pekee na wilaya moja ambayo ni Wilaya ya Rorya kwa sasa haina huduma kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada zilizopo kwa upande wa Serikali kupitia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, ni kuhakikisha kwamba tunapeleka Askari wa Zimamoto na Uokoaji pamoja na gari la kuzimia moto katika eneo la Wilaya ya Rorya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi iliyofanywa na Serikali katika nchi nzima ni kubwa, na ni kweli tunakiri kati ya wilaya 139 zilizopo, kwa sasa Serikali imefikisha huduma katika wilaya 133 na wilaya sita hazina huduma kabisa za Zimamoto na Uokoaji. Jitihada zinazoendelea sasa ni kuhakikisha kwamba huduma hiyo inaendelea kutolewa, kwani katika kipindi cha hivi karibuni, Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imefanya kazi kubwa ya kuliwezesha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa kulipatia magari ya kuzima moto 150, lakini magari ya kuzima moto wa kemikali matatu. Vilevile, Serikali imepatia magari 40 ya kubebea majeruhi, magari ya mawasiliano na amri yapo 30, kadhalika kuna boti 23 za uokoaji pamoja na helikopta moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada zote hizi zinalenga kuhakikisha kwamba changamoto ya kuondoa shida ya

kutokuwa na magari au huduma ya uokoaji na zimamoto inaondoka. Ninapenda kumhakikishia Mheshimiwa Esther kwamba, tutahakikisha tunajenga katika eneo lake kwa mujibu wa hali ya kibajeti itakavyojitokeza. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kanoni, nilikuona.

**MHE. EDIFONSI J. KANONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza. Jimbo la Kalambo lina wakazi zaidi ya 350,000. Kijiografia tunapakana na nchi ya Congo na Zambia. Mazingira ya Jeshi la Polisi wanapofanyia kazi siyo rafiki. Ili kuboresha huduma za wananchi na kulinda mipaka yetu, ni lini sasa Serikali itajenga Kituo cha Polisi cha Wilaya katika Jimbo la Kalambo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kanoni itabidi ulete swali la msingi. Tunazungumzia Jeshi la Zimamoto. Mheshimiwa Hawa Mwaifunga.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Pamoja na magari ya zimamoto, lakini bado Mkoa wa Tabora umekuwa na changamoto kubwa ya magari ya doria kwa Askari Polisi wa mkoa huo. Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba wanaongeza magari ya doria ili kuweza kuzuia uhalifu katika Mkoa wa Tabora?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, na hilo ni swali la Jeshi la Polisi kama unayo majibu sawa, lakini kama hakuna, Mheshimiwa Hawa ulilete kama ni swali la msingi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Hawa na ninashukuru pia kwa hoja yake ya msingi ya eneo la Mkoa wa Tabora na magari ya doria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumwarifu Mheshimiwa Hawa kwamba, Serikali kupitia Jeshi la Polisi linaendelea kuimarisha kwa kuwapatia vifaa mbalimbali vikiwemo magari mbalimbali ya doria. Kazi hiyo imefanywa kwa kupatiwa Jeshi la Polisi fedha zaidi ya Dola za Marekani milioni 100 ili kuhakikisha

kwamba linawezeshwa kivifaa vikiwemo magari ya doria, pikipiki na helikopta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kumhakikishia Mheshimiwa Hawa kwamba, tunaendelea kupokea magari na tutaendelea kuliwezesha Jeshi la Polisi ili kuwahakikishia usalama wananchi katika Mkoa wa Tabora na maeneo mengine nchini kwa kuwa na magari ya kutosha ya doria. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, maswali yetu kwa siku ya leo ni hayo. Ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote ambao wanaendelea kujitahidi kuuliza maswali mafupi ya Kibunge na Waheshimiwa Mawaziri ambao wanajibu majibu hayo ya maswali ya nyongeza kwa ufupi.

Ninaamini kabisa na wengine wanaendelea kujifunza na hatimaye tutakuwa na Waheshimiwa Wabunge wote ambao wanaweza kufupisha maswali ya nyongeza na Waheshimiwa Mawaziri kujibu kwa ufupi.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuzungumza hayo, tuna matangazo sasa ya wageni ambao wapo Bungeni asubuhi hii. Kuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Kwanza ni wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji, Mbunge na Waziri wa Maliasili. Hawa ni wadau wa sekta ya utalii nchini. *(Makofi)*

Tunao wageni 83 wa Mheshimiwa Dkt. Kijaji, ambao ni Kikundi kutoka Kituo cha Sanaa na Utamaduni cha Viziwi Tanzania (KISUVITA), karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao waongoza watalii wanawake na wanaume, waongoza watalii, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi kutoka Chuo cha Utalii, Kampasi ya Arusha karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye Mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, huyu ni Ndugu Gasper Manyaki, Katibu wa Jumuiya ya Kolping Tanzania ya Jijini Dodoma, karibu sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Shayo, ambao ni wapigakura wake kutoka Moshi, Mkoani Kilimanjaro, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Yohana Stephen Msita, ni watalamu wa Kata ya Aghondi kutoka Manyoni, Mkoani Singida karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni wageni 36 wa Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, ambao ni Madiwani kutoka Nanyamba, Mkoa wa Mtwara, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Kwanza ni Ndugu Godfrey Mgalla kutoka Jijini Arusha. Karibu sana. *(Makofi)*

Wapo wanafunzi 84 na Walimu sita kutoka Shule ya Msingi Angelico Lipan ya Jijini Arusha, karibuni sana wanafunzi wetu pia kutoka huko Arusha. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge hao ndio wageni wetu kwa leo, karibuni sana wageni wetu wote katika Bunge letu.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano yetu kwa Wizara ya Maliasili na Utalii. Tunaanza na

Mheshimiwa Asia Abdulkarim Halamga, atafuatiwa na Mheshimiwa Haji Amour Haji na Mheshimiwa Mary Daniel Surat ajiandae.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami ya niweze kuchangia katika Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka 2026/2027. Awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, na baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uzima na afya na kuwepo leo hapa, nichukue nafasi hii kupongeza jitihada za dhati za mwongoza utalii namba moja katika nchi yetu ya Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amekuwa ni kielelezo cha mfano wa uzalendo katika nchi yetu ya Tanzania katika kuhakikisha sekta hii ambayo inatuingizia mapato ya fedha za ndani pamoja na fedha za kigeni na ni Wizara ya pili inayotuingizia fedha katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kukupongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji pamoja na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Hamad Chande. Vile vile nampongeza Katibu Mkuu, Dkt. Abbas, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi na watalamu wote wanaotokana na hii Wizara ya Maliasili na Utalii. Tunawapongeza kwa sababu ya kuendelea kuhakikisha wanasimamia rasilimali zetu, wanaziboresha, wanazitangaza na kuhakikisha watalii katika nchi yetu wanaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna kila sababu ya kuwapongeza kwa sababu Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2025 ilikuwa imekadiria kuongeza watalii 5,000,000, lakini Wizara hii imeweza kufanya vizuri, imeongeza watalii zaidi ya 5,936,561. Hii ni hatua kubwa, na hatuna hofu, tuna imani kubwa na mipango ya Serikali lakini kupitia Ilani ya Uchaguzi ambayo inahitaji kufika mwaka 2030 tuwe na watalii 8,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ilani iliyopita ya mwaka 2025, kazi kubwa ambayo imefanyika ya kuwatafuta watalii kwa zaidi

ya 10.7% ni kazi ya kipekee ni kazi ya kizalendo na tuna uhakika na safari inayoendelea ya kufika watalii 8,000,000 mwaka 2030.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuipongeze Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kuendelea kuiwekea heshima nchi yetu, kwa kuendelea kuitangaza Kimataifa, kwa kuendelea kuitangaza huko duniani. Wizara hii tumeona Mheshimiwa Mheshimiwa Rais akipokea tuzo mbalimbali tulizoshinda kwa kuwa nchi ambayo inakua kwa kasi katika sekta ya utalii na pia katika amani, umoja na utulivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna kila sababu ya kuheshimu heshima ambayo tunapewa huko duniani. Tuzo mbalimbali tunazopewa na ni lazima tuhakikishe kwamba tunaungana na Wizara ya Maliasili na Utalii, tunaungana na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuhakikisha hii Wizara inaendelea kututambulisha kidunia, na Wizara hii inaendelea kutuletea pato katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii tunaendelea kuipongeza kwa kuboresha miundombinu. Katika sekta ya anga kumejengwa zaidi ya viwanja vitatu vipya vya ndege. Hii tunaona hatua kubwa ya kimaendeleo, fedha zilizosimamiwa na kutumika kisawasawa, lakini nje ya viwanja vipya vitatu, bado kumefanyika ukarabati mkubwa wa viwanja vingine nane. Natolea mfano kiwanja cha Ruaha, Mikumi na viwanja vingine vya Musoma, Serengeti na viwanja vingine katika nchi yetu. Hii ni hatua kubwa ya mageuzi makubwa katika sekta ya maliasili na utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo niendelee kupongeza kwa jitihada kubwa za kuendelea kuhakikisha Serikali imenunua mitambo ya kisasa kwa ajili ya ujenzi wa barabara. Huu ni ukombozi mkubwa. Tunachokiomba sasa, ili sekta hii iendelee kurahisha huduma mitambo hii, Waziri wa Fedha hapa ni lazima aiangalie sekta hii kwa sababu inatungizia pato, hivyo waongezewe fedha ili miradi na mitambo iweze kufanya kazi na kuhakikisha barabara zetu muda wote zinaweza kupitika kuendelea kutoa ajira kwa vijana wa Kitanzania, wakinamama wa Kitanzania, na wafanyabiashara wa Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiona sekta hii ni namna gani imeendelea kukuza uchumi kwa kila Mtanzania mmoja mmoja. Tunajionea mfano wa wageni wengi katika viwanja vyetu vya Kimataifa, Kiwanja cha *KIA*, Kiwanja cha Dar es Salaam na *Nyerere International Airport* namna watalii wanavyomiminika katika Taifa letu. Hii ni kazi kubwa ya kuipongeza, na sisi Wabunge na Watanzania kuunga mkono juhudi ya nchi yetu kuhakikisha kwamba tunaendelea kuwavutia watalii na kuongeza fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaelekea kwenye *AFCON* mwaka 2027. Jukumu la *AFCON* lipo kwa Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara nyingine zote katika nchi yetu. Sekta zote zinahusika hapa katika kuhakikisha kitu kikubwa hiki kinachokuja kwenye nchi yetu, wageni wanaoweza kuendelea kutumia vivutio vyetu ili waendelee kuitangaza nchi yetu wanaporudi majumbani kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sekta zote; umeme, maji, barabara zinatakiwa ziungane. Wizara ya Michezo, Maliasili na Utalii; na hapa niwapongeze Maliasili na Utalii kwa sababu tumewaona hata katika Bara la Asia wameendelea kufungua soko na kuendelea kufanya matangazo. Tumeona warsha mbalimbali, makongamano mbalimbali, tumewashuhudia nchini Uturuki wakiwa katika kongamano la kuitangaza nchi yetu katika soko la Uturuki na masoko mengine ya Ulaya. Hii ni hatua kubwa, ni hatua ya kihostoria, ni hatua ya kuikomboa sekta ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa lazima tuendelee kumuunga mkono Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo anaendelea kuhakikisha heshima ya wanyama wetu, heshima ya vivutio vyetu tulivyobarikiwa na Mwenyezi Mungu vinaweza kuleta tija katika Taifa letu na kuvitangaza zaidi huko duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze sana Wizara hii kwa kufanya Sensa ya Wanyama. Sensa ya Wanyama huwa inafanyika kila baada ya miaka 10, na niwapongeze kwa sababu ni hatua kubwa katika nchi yetu na ni ya kistoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kwenye wanyama niendelee kuchukua nafasi hii kuwaomba kuongeza jitihada za kuwalinda wanyama dhidi ya wanyama waharibifu wanaotoka nje na kwenda kusababisha madhara huku kwa wananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanyama tunawahitaji, wanatuongezea pato, lakini sasa Wizara ya Fedha lazima iongeze bajeti kwenye Wizara ya Maliasili na Utalii ili tuweze kutengeneza miundombinu mbalimbali ya kuweza kuzuia wanyama wasitoke nje na kufanya uharibifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ninaipongeza Wizara hii kwa hatua madhubuti iliyofanya na kwa kupitia Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuongeza ndege nyuki zinazoweza kusaidia kufukuza wanyama angalau na sasa hapo Wizara ya Fedha bado nasisitiza kuongezwa kwa fedha ili tununue ndege nyuki nyingi, ili tuongeze *electrical fence* kwa ukubwa na kuweza kusababisha tupate pato la Taifa, lakini pia tuhakikishe wananchi wetu wanakuwa salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kupongeza uimarishaji wa soko la asali huko duniani.Ttumezalisha zaidi ya tani 1,596 na tumeingiza fedha za kigeni 19,000,000,000. Ninaiomba Wizara hii, sasa tuna uwezo wa kuzalisha zaidi na kupata fedha zaidi za kigeni na Wizara hii itoe mizinga kwa kila halmashauri ambazo zina uwingi mkubwa wa nyuki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninakaribisha Wizara ya Maliasili ilete mizinga ya kutosha katika Jimbo la Hanang, wananchi wangu wanafuga nyuki, wananchi wangu wana mizinga ya zamani, tunaomba mizinga ya kisasa na maeneo mengine pelekeni mizinga ya kisasa. Hii 19,000,000,000 tunaamini itazaa zaidi ya hapa, wananchi watapata ajira, tutaendelea kupata fedha za kigeni na tutaendelea kuhudumia miundombinu mingine ambayo inatuhitaji katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuendelee kuongeza juhudi za matangazo, kazi kubwa inafanyika lakini lazima tuendelee kuwatafuta *influencer* wa ndani ya nchi na nje ya nchi, na hapa

nipongeze, tumeona jitihada mbalimbali za kuwaleta *influencer* kutoka nje na kutangaza utalii wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu katika kuendelea kutangaza utalii, katika kuendelea kuboresha utalii wetu wa ndani, mimi binafsi ninaomba Serikali ipunguze sasa huko mbele tunapoelekea kutoa leseni za *zoo* kwa sababu mwaka 2019 kipindi cha *Corona* tulipokosa watalii wa nje, watalii wa ndani ndio walioikoa hii sekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukiendelea kutoa vibali vya *zoo* kila mtu akawa ana-*zoo* nyumbani kwake, maana yake sisi wenyewe Watanzania tunajifahamu ni wavivu kutembea. Mtu hawezi kutoka hapa akaenda Serengeti wakati kuna *zoo* iko hapa Dodoma, anaenda na anamlisha mnyama. Kwa hiyo, tuangalie namna ya kudhibiti *zoo*. Ifike mahali tuziweke kwa kiwango ili hifadhi zetu ziendelee kupata tija kwa miaka, kwa kizazi kwa karne na karne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea kuipongeza Wizara hii, ninaendelea kuipongeza Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Wizara hii ni Wizara ya kimkakati, ni Wizara ya kutuletea fedha, kila Mtanzania ana haki na wajibu wa kuhakikisha kwamba Wizara hii wote tunakuwa wazalendo na kuhakikisha inaendelea kutangaza nchi yetu Kimataifa, lakini inaendelea kutoa ajira kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Tena tumechelewa sana, Wizara hii ingekuwa ya kwanza na sasa hivi wawe wamepitishiwa bajeti waende wakafanye kazi, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asia Halamga, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Haji Amour Haji, Mheshimiwa Mary Daniel Surati, Mheshimiwa Njalu Daud Silanga ajiandae.

**MHE. HAJI AMOUR HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nami niweze kukushukuru kwa kuweza kuniona, kuweza kuijadili na kuizungumzia Wizara yetu ya Maliasili na Utalii. Pili,

niweze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuwepo hapa katika kuleta mjadala wa Wizara yetu ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote, nianze kumpongeza au niwapongeze watendaji wote wa hii Wizara ya Maliasili na Utalii hasa mwanauchumi, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji kwamba ni Waziri wa Utalii. Nimpongeze ndugu yangu Mheshimiwa Hamad Chande akiwa kama ni Naibu Waziri, na niwapongeze Watendaji wote wa Wizara hii wakiwemo Katibu Mkuu pamoja na Wakurugenzi wenye kusimamia taasisi za utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu, kwangu mimi hii Wizara ya Maliasili na Utalii ndiyo iliyobeba hiyo maliasili kwa ujumla, na nitazungumza kwa nini ninazungumza hivyo? Nikizungumza hivyo, ni kwamba utalii ndiyo mama na utalii ndiyo uliobeba ngazi zote za hivi vivutio ambavyo tunavyoviita maliasili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila ya maliasili maana yake au hivi vivutio ambavyo vipo, maana yake inawezekana pengine huo utalii wenyewe usingekuwepo. Sasa utalii kwa kweli unategemea, cha kwanza ni hivyo vivutio. Tukizungumzia vivutio ni pamoja na hizo maliasili, zikiwemo mbuga za wanyama, wakiwemo safari *and tours* katika hizo mbuga za wanyama ikiwemo misitu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, utalii unahitaji miundombinu iliyokuwa bora. Bila ya kuwa na miundombinu iliyokuwa bora bado nitasema kwamba utalii wetu utakuwa una mashaka. Nikizungumzia miundombinu bora, maana yake ni vizuri zaidi tukawa na barabara zilizokuwa nzuri zaidi ambazo watalii wetu wanapokuja watakuwa hawapati shida katika kufanya safari zao za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, katika miundombinu maana yake tuwe na viwanja vya ndege ambavyo viko imara na vitakavyoweza kufikika kwa watalii wetu kwa urahisi. Tatu, katika masuala ya miundombinu, maana yake masuala ya mawasiliano yetu yawepo, kama *internet*, na vitu vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili nizungumzie suala la amani na usalama. Bila amani na usalama tuliokuwanao katika nchi yetu, utalii pia utakuwa pengine unalegalega. Mtalii kwa kawaida huwa hapendi kwenda mahali ambapo hapana amani au pengine hapana usalama kwa namna yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la tatu maana yake mbali na miundombinu, amani, huduma za malazi ambazo nazo ni kitu ambacho ni muhimu sana kuwepo katika sehemu ambayo tunakusudia kwamba ni moja ya vivutio vya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nizungumzie suala moja ambalo hata kwenye Kamati walilishauri kidogo kama vile tunalega, nalo ni suala la utamaduni, pamoja na hizi *heritage,* na utamaduni wetu. Maana yake hatujawa vizuri sana kwa upande huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo nizungumzie suala la brandi ya utalii kwa upande wa Tanzania. Hakuna kitu ambacho nitasema ninampongeza Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuleta *Royal Tour. Royal Tour* ni sehemu ya kuweza kutangaza utali, lakini vilevile ni *branding* yetu kwa upande wa Tanzania kwa sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mama Samia Suluhu Hassan alifanya kazi kubwa sana ya kutembelea vivutio vyote kwa upande wa Tanzania. Tukizungumzia Tanzania ili kuweza kuzungumzia utalii wa Tanzania, maana yake ni kuunganisha baina ya Zanzibar na kuunganisha na vile vivutio ambavyo vipo upande wa Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mama Samia Suluhu Hassan katika kuutangaza utalii wa *Royal Tour* alianza tripu zake kuanzia upande wa Zanzibar, kutangaza zile sehemu za *beaches* akaja kwenye mbuga zote ili kuujumuisha utalii wetu wa Tanzania, maana yake kuwa ni utalii mmoja. Kwa kweli niseme kwamba ninampongeza sana Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na jitihada yake kubwa ya kuutanga utalii hasa kwa kupitia *Royal Tour. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba mafanikio makubwa ambayo yamefanyika kwa upande wa Tanzania, ikawa kati ya *top ten* za utalii katika nchi ya Afrika, Tanzania imo kwenye *top ten* na hii imekuja kwa sababu ilipiga hatua kubwa wakati ule tulipoitangaza Tanzania, Mama Samia alipopita kwa kuitangaza *Royal Tour*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha pili, mbali na *Royal Tour,* Tanzania tunakosa kitu ambacho wakati mwingine labda tunajisahau, lakini kuna kitu ambacho tunasema ni *slogan* ya utalii kwa upande wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shida ambayo tuliyokuwanayo kwa upande wa Tanzania hasa kwa upande wa hii *slogan* maana yake tunakuwa kwamba hatuko *consistence* katika hili suala la *slogan*. *Slogan* yetu kila wakati maana yake inabadilikabadilika. Mwanzo tulikuwa na *Tanzania Unforgatable*. Hiyo ndiyo ilikuwa *slogan* yetu, lakini wakati mwingine tunakuwa tunabadilisha aina ya *slogan.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri zaidi kwa upande wa utalii tukawa na *slogan* ambayo ni ya kudumu. Kwa mfano, kama mimi ningeulizwa Tanzania unahitaji iwe na *slogan* ya aina gani? Mimi ningesema tu *slogan* ambayo ni nzuri, ni *The Soul of Africa*. Yaani *Tanzania is the Soul of Africa*, kwa sababu hii ingekuwa inaunganisha vivutio vyetu vyote tulivyokuwa navyo ndani ya Tanzania tukiacha mbuga, tukienda pamoja na *beaches* zetu zote, milima, misitu na kila kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nitoe ushauri, kwa upande wa hii Wizara yetu ya Utalii, ningesema labda ningependa tuchague *slogan* ambayo itadumu na itakayokuwa ni *engine,* itakayoweza kuitangaza Tanzania. Tuwe na *slogan* ya aina moja itakayodumu kwa kipindi kirefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nchi kama *Spain*, *India* na Uturuki, ukizitazama zile *slogan* zao ni *slogan* ambazo zimechukua muda mrefu sana. Ukitazama hasa kiutalii maana yake hizo nchi zinajiuza kwa sababu ya zile *slogans* zao kukaa muda mrefu. Wakati mwingine kuna watalii wanaweza wakakosa *taste* fulani,

maana yake wanahitaji kitu ambacho ni *unique* au pengine ni *antique*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa *slogan* maana yake kwa Tanzania nitasema ni nchi ambayo tumejikusanya kila kitu. Tanzania tuna vivutio vya aina yake, kwa Afrika Tanzania tuko vizuri sana. Kila aina ya kivutio, kwa upande wa Tanzania tunacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha pili ninashauri kwamba, kuwekeza sana kwenye *video documentary* pamoja na *documentary* ambayo ni *quality* kwa upande wa dunia. Ninashauri kitu cha tatu, kutumia *influencers* wa Kimataifa. Ndugu yangu Mheshimiwa Asia alizungumzia kwamba *influencers* wa ndani, lakini kwa vile tunaitangaza Tanzania nje kiutalii, ni vizuri zaidi tukawa na wale *influencers* wa Kimataifa watakaoweza kuitangaza Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, kuunganisha utalii pamoja na *culture* (utamaduni wetu). Tuunganishe utalii na *music* zetu; tuunganishe utalii wetu, pamoja na chakula ambacho tunapika. Ni vigumu sana kwa upande wa Tanzania na watalii, ni sehemu chache utakazoweza kuzikuta maana yake wanatangaza utamaduni wetu hasa kwa upande wa vyakula vyetu, kwa upande wa *music* yetu. Maana yake ni sehemu ambazo ni chache, ambapo ni kitu ambacho kwa upande wa utalii ninapenda kwamba nacho tujaribu kuitangaza Tanzania kwa upande huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutanua *brands* zaidi kwa upande wa safari. Hizi safari ambazo tulikuwa nazo tukatengeneza *brand* ambayo ni *specific* kwa upande wa hizi safari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kigezo kingine cha sita; ni kurahisisha suala la *visa* pamoja na safari za watalii. Maana yake tunaporahisisha *visa* pamoja na safari za watalii, maana yake ni kuifanya Tanzania au kuwafanya wale watalii waione Tanzania ni rahisi kufikika. Tutakavyoweza kufanya hivyo, maana yake tunaweza tukarahisisha shughuli zetu za watalii kuja kwa haraka zaidi na kuja kwa wingi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ninaweza nikaishauri Wizara kuna kitu ambacho wakati mwingine katika haya masuala ya elimu ambazo tunazo mpaka sasa hivi, Tanzania sijaona chuo ambacho kinasomesha masuala ya *Hospitality Management*. Tunasomesha *tourism* pamoja na *heritage*, lakini suala la *Hospitality Management* tunakosa, kama kutoa *degree*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema Wizara ya Utalii wakaandaa kozi za *management* kwa upande wa *degree*. Tunavyozungumzia suala la *Hospitality Management* maana yake ni kuwaandaa *managers* ambao wataweza kusimama kuwahudumia wageni ndani ya hoteli zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho nitakizungumzia ambacho ni muhimu sana, ni suala la *customer care*. Ni vizuri zaidi kuwafundisha watu wetu kuwa na *customer care* itakayoweza kuwafanya wageni wetu waweze kurudi tena. Maana yake ni vizuri zaidi tukawa tunapata *returning* ya wageni ambao wamekuja kuliko kila siku kupata wageni wapya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii ili uweze kujengeka ni vizuri zaidi tukapata wageni wapya na vilevile na wageni ambao wamekuja lakini kutokana na ile kutamani, wanatamani zaidi kuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, nizungumzie kwamba tumekabiliwa na *AFCON* ambayo inakuja, nayo nitasema kwamba ni jumla ya kivutio kipya. Maana yake hii nayo ni jumla ya kivutio kipya. Tunahitaji matayarisho ya kutosha kabisa upande wa *AFCON*. Maana yake *AFCON* nayo tuichukulie kwamba ni moja ya kivutio kitakachosababisha kuja kwa watalii. Sasa, kwenye suala la *AFCON* kunahitajika miundombinu ambayo inashabihiana na utalii. Tuimarishe hoteli zetu, tuimarishe viwanja vyetu vya mipira, tuimarishe barabara zetu, tuimarishe kila kitu ili kiwe katika hali ya ubora ili kuja kuwafanya wageni watakaokuja kutembelea *AFCON* wakute kila kitu kilicho bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Hongera sana Wizara ya Utalii

na Maliasili, wanafanya kazi kubwa sana. Tanzania kwa sasa imekuwa ni bora kwa upande wa utalii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Haji Amour Haji. Nilimtaja Mheshimiwa Mary Daniel Surati; Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga na Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava wajiandae.

**MHE. MARY D. SURATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kutoa mchango wangu katika Wizara hii muhimu na ya msingi sana, hasa kwa sisi watu wa Serengeti. Ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwamba nimepata fursa ya kupata nafasi ya kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanza kabisa ninaomba nitoe pongezi za dhati na shukrani za dhati kwa mhifadhi namba moja, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuheshimu mchango wake wa yeye kuona fursa kubwa inayopatikana katika Wizara hii ya Maliasili na Utalii na akaja na filamu ya *The Royal Tour*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili linaweza likaonekana ni jambo la kawaida, lakini kwa ufahamu wake na yeye kuwa kiongozi mwenye maono aliweza kutambua sisi kama nchi ya Tanzania hapa Afrika ndiyo tunaongoza kwa rasilimali za vivutio, ambapo sisi ni namba moja kwa Afrika na duniani sisi ni namba 12. Kwa hiyo, kwa kuyaona hayo ameona ni jambo jema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kufanya Filamu ya *The Royal Tour*, pia ameenda mbali na kuhakikisha anaboresha minyororo yote ambayo inaelekea kusaidia watalii wetu kufanya utalii bila kupata changamoto zozote. Kwenye hilo eneo ninaomba pia kama mhifadhi na mimi, hasa hasa mimi ni Mbunge wa Jimbo la Serengeti na ninafahamu ni kwa namna gani jinsi ambavyo Hifadhi yetu ya Serengeti, hifadhi bora kabisa Tanzania ilikuwa inakwenda kupata changamoto zinazotokana na usafiri wa watalii wetu kuingia pale na tumekuwa na viwanja vidogo vidogo vya ndege mle ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii imeathiri uzalianaji wa wanyama wetu na baadhi ya wanyama kuhama, lakini akaona ni kitendo cha kiungwana sasa tupate *international airport* ambayo inapatikana nje ya hifadhi, watalii wetu wafike kwa usalama, lakini pia na mle ndani tuendelee kutunza ekolojia yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, ninaomba niwapongeze viongozi wetu wa Wizara kwa kuanza na Mheshimiwa Waziri mwenyewe pamoja na watendaji wake wote. Ninaomba nijikite kwenye maeneo machache ambayo yatakuwa ni matano na kama ambavyo wachangiaji wengine wametangulia, ninakubaliana na hoja zao walizozitoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijikite kwenye kusema kwamba malipo ya *open area* yamekuwa ni changamoto na yamekuwa hayatoki kwa wakati. Ninapongeza jinsi ambavyo malipo ya *WMA* yanatoka kwa wakati, lakini pia ninatumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii. *Weekend* hii nimepokea meseji nyingi kutoka kwa wananchi wangu wakishukuru wamepata zile fedha za kifuta jasho. Ninashukuru sana angalau sasa na mimi ninaweza kuhema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kama ambavyo fedha za kifuta jasho zimefanyiwa kazi kwa wakati, ninaomba na pesa za *open area* zitoke kwa wakati. Kwa sababu, pesa hizi pamoja na kwamba ni za muhimu, lakini ndiyo pesa ambazo zinawalipa watu wetu wa *Village Game Scouts*. Hawa ni watu ambao wanasaidiana na ndugu zetu ambao wanafanya shughuli za uhifadhi kusaidiana kutatua changamoto za ujangili. Fedha hizi za *open area* ni sehemu ya pesa ambazo zinatoa mishahara kwa hawa ndugu zetu. Kwa hiyo, zinapochelewa kutoka inasababisha ulinzi katika yale maeneo unakuwa ni wa kulegalega na pia hifadhi yetu inaweza ikahujumiwa. Ninaomba pesa hizo zitoke kwa wakati kama walivyofanya kwenye pesa za kifuta jasho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninaomba niongelee kuhusiana na uhaba wa vitendea kazi. Kwa hapa kidogo Mheshimiwa Waziri atanisamehe kwa sababu binafsi kama Mbunge wa Jimbo la Serengeti ninaona ni kitu cha aibu sana, kwamba ndugu zangu hawa ambao wanajitahidi sana

kushirikiana na kuhakikisha kama hifadhi tunaendelea kushirikiana na wananchi wetu, lakini mimi tokea mwezi Desemba mpaka leo ninapozungumza pale Kono, Makundusi na Nyichoka, wananchi wangu wanaishi na simba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikikumbukwa kwamba wananchi hao wanaishi karibu na eneo la hifadhi. Kwa hiyo, hata kusema kwamba wanaweza kufanya kilimo au kitu gani hapana. Wengi wao wanategemea mifugo. Hata hivyo, mpaka sasa hivi tokea hiyo mwezi Desemba mpaka tunavyozungumza, simba wale bado hawajatolewa kwa wale wananchi. Simba pekee ambao wameweza kuchukuliwa mpaka muda huu ni simba nane tu ambapo ukiendelea kuhoji na kuuliza wanakwambia Mheshimiwa hatuna dawa, Mheshimiwa tumepungukiwa mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli? Hifadhi ya Serengeti imeliletea Taifa tuzo mara nne mfululizo kama hifadhi bora Afrika na duniani, halafu wananchi wangu wanakaa kuishi na simba? Hatuwezi kuwadhuru kwa sababu na sisi ni wahifadhi, lakini wanawaacha wanatumalizia mifugo yetu, wakijua fika ndicho kitu ambacho tunakiangalia kama kitega uchumi chetu. Tafadhali, ninaomba Mheshimiwa Waziri aniondolee aibu hii kwa sababu sasa hata kwenda kufanya ziara ninashindwa. Simba wapo na wanasumbua wananchi wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia niende kwenye jambo lingine ambalo jambo lenyewe ni kuhusiana na Miradi ya Ujirani Mwema. Hapo awali tumekuwa na miradi hii ambayo imekuwa inatumika katika kuboresha mahusiano yetu, lakini pia katika kuwafanya wananchi wetu waweze kuona umuhimu wa Hifadhi ya Serengeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, miradi hii sielewi ni nini kimetokea lakini ni kama haipo. Kitu ambacho kinapelekea unapokwenda kuzungumza na wananchi wako kuhusiana na namna gani tuendelee kuilinda hifadhi yetu, wanaweza kukuuliza maswali ya hadharani bila kupata wasiwasi, kwamba, Mheshimiwa Mbunge mbona watu ambao wana bahari, wana maziwa, ambao Mungu amewajaalia, mbona wao wanaendelea kuvua mle ndani? Kwa nini na sisi tusiruhusiwe kuendelea kupata

walau vitoweo ndani ya hifadhi hizi? Maswali yale ninawaelewa wananchi wangu. Siyo kwamba hawaelewi umuhimu wa hifadhi yetu. Wanaelewa fika, ila wanaona mbona hatupati ile kunufaika moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwasihi; ile Miradi ya Ujirani Mwema kilikuwa ni kitu kizuri na kilikuwa ni kitu cha msingi na kilikuwa kinasaidia sana katika kuhakikisha wananchi wetu wanapata uelewa wa kutosha, lakini wanayaona manufaa ya moja kwa moja ya hifadhi yetu. Ninaomba miradi hiyo irudi na irudi kwa kasi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo na penyewe lina changamoto na niseme tu wazi ndani ya Bunge lako Tukufu, mimi kama Mbunge wa Jimbo la Serengeti ninapokuwa ninasafiri kama nitapita njia ya Seronera, huwa sipeperushi bendera. Kinachonisababisha nisipeperushe bendera, siyo sipendi, ni kwa sababu hali ya barabara zilizoko hifadhini ni hali ambayo ni mbovu na ya aibu kiasi kwamba ni kitendo cha kawaida kabisa kukuta uko barabarani unawahi usafiri, ukakuta kuna gari ambayo pengine ina mtalii au pengine ya mwananchi mwingine akiwa kwenye shughuli zake imeharibika pale. Wewe kama kiongozi huwezi ukapita kana kwamba huoni ni nini kinaendelea pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni kwa muda gani tutaishi maisha hayo? Ni kwa nini iwe hivyo? Hifadhi hii katika Wizara yetu ya Maliasili na Utalii, sisi Serengeti tunachangia zaidi ya 50% ya mapato yote. Ni kwa nini watuachie barabara kuwa za aina ile? Ni kwa nini barabara zifanane na namna ile? Kutokana na barabara hizo baadhi ya watalii wanapokuja kwetu hawarudi. Kwa sababu gani? Barabara zile zina-*risk* maisha yao. Tumeona tukio baya kabisa hivi karibuni tumejikuta baadhi ya magari yakisombwa na ni magari ya watalii wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, pamoja na mema na mazuri yote ambayo ameyapanga, tafadhali jambo hili lisijitokeze. Ninajua kwenye ripoti yao nimesikia wakiongelea kwamba imetokana na mvua. Hapana. Pamoja na mvua, lakini jambo hili, hali hii ya barabara

hizi imekuwa ni ya muda mrefu. Imekuwa ni ya muda mrefu kabisa. Kwa hiyo, ninaomba hilo lichukuliwe kwa uzito wake, kwa umaalum na kwa msingi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapongeza hela ya *emergency* ambayo imetolewa ambayo ni takribani shilingi bilioni 8.1, lakini ninaomba iongezwe kwa sababu haiendani na uhitaji. Ukizingatia barabara zenyewe bado tuna madaraja yanayohitaji kuunganishwa, bado tuna barabara ambazo tunahitaji ziinuliwe. Kwa hiyo, ninaomba paangaliwe kwa umakini mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia ninaomba pia Mheshimiwa Waziri atusaidie na pengine anapokuja kupitishiwa bajeti yake atufafanulie wazi. Kumekuwa na hii changamoto ya magugu vamizi, ambapo kwa kule kwetu sisi Ukuryani tunayaita *machabongo*, lakini nimeambiwa kwa jina la kitaalamu yanaitwa *Chromolaena odorata*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya magugu vamizi sambamba na kwamba tunapambana kama Wanaserengeti kuhakikisha wananchi wetu wanapata malisho katika maeneo yetu ya makazi, lakini magugu haya yamekuwa yanaenda moja kwa moja kushambulia malisho yetu na kutengeneza vichaka vya wanyama wakali kama simba na fisi. Mpaka sasa tunavyozungumza, bado hatujaona ni juhudi gani za dhati za kumaliza jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia ninaunga mkono hoja kwa asilimia zote. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mary Surati. Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava na Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri ajiandae.

**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba hii muhimu sana kwa nchi. Ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa maono yake mazuri na ninawapongeza sana watumishi wa Maliasili na Utalii wakiongozwa na Waziri mwenye dhamana

pamoja na Katibu Mkuu na wote tu kwa ujumla, taasisi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea kushukuru kwamba, Wizara ya Maliasili na Utalii imeweza kufanya kazi kubwa kwenye maeneo yetu. Kwanza imetupatia fedha kwa ajili ya vikundi zaidi ya vijiji tisa. Tunawapongeza sana, zaidi ya shilingi 154,000,000 kwa ajili ya kujipatia kipato wananchi wa eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na haya yote tunayoyazungumzia katika Bunge lako Tukufu, uhifadhi tunauhitaji sana lakini na wananchi tunawahitaji sana. Tunahitaji mshikamano wa haya yote mawili ili yafanikiwe kwa pamoja. Kwenye maeneo sisi tunayotoka mpakani mwa Serengeti – *Maswa Game Reserve* tunazo changamoto kubwa sana na ni nzito sana. Ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri na taasisi yake. Kwanza tunawashukuru wameajiri vijana wa kufukuza wale tembo na wametufungulia vituo vya kudhibiti wanyama wakali. Ni jambo la kuwapongeza Serikali kwa kazi kubwa na nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na haya, ni vyema sana hawa vijana (maaskari) wakawafundisha jinsi ya kuishi na raia kwenye maeneo hayo. Kumekuwa na changamoto kubwa sana. Katika akili ya kawaida yawezekana baada ya kupewa nafasi ya kuwa askari akaamini akienda kwenye hifadhi ukiona raia, kazi yako ni kushughulika na raia bila kutoa elimu kwenye eneo husika. Sisi tunapohitaji umoja, tunapohitaji ujamaa, ni pamoja na kushirikiana na wananchi waliotuamini tukaja katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tembo wanapokuja kuharibu mazao yetu tunakuwa na kifuta machozi. Ni jambo kubwa sana. Mheshimiwa Waziri ametuandikia kwenye hotuba yake, badala ya kuchukua miezi miwili mpaka mitano mpaka mwaka, umeweka siku saba hadi siku 14. Ni jambo la kuwapongeza Wizara, wamejipanga vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa ushauri; kama ng'ombe wetu wanapoingia kwenye hifadhi wanakamatwa, wanawekwa kwenye zizi, wanapigwa faini na mpaka mwenye ng'ombe alipe

ndiyo watoke. Kwani tembo hawa wanapoingia kwenye maeneo yetu, kwa nini na sisi tusiwe na mazizi tukawazuia watulipe ndiyo watoke huko ili kusudi tuelewane pamoja pale? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, tembo hawa wanapodhuru mahindi kwenye kipindi cha kiangazi, sheria yetu au sheria ya wahifadhi inawataka wasilipe kwa sababu yameliwa nje ya kilometa sijui tano. Tayari hapo tunapozungumza ajira, tunapozungumza maisha ya wananchi tunatengeneza mgogoro kwenye jamii ambayo inaamini kabisa kwamba ilichokipata itakuja kujihudumia. Hawa tembo tena wanarudishwa kwa *escort* na barabara zenyewe hazipo za kupitisha hao tembo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba kama Serikali ilitazame jambo hili kwa umakini wa hali ya juu sana. Wananchi hawawezi wakawa wanatupa nguvu zao, wakulima nao, wafugaji nao, inapofika sehemu tunaanza kugombana zaidi ya miaka mitano. Mahakama imeamua warudishiwe mali zao, ng'ombe hawapo walishakwishauzwa. Kwa hiyo, jambo hili kwa kweli wakati mwingine huwa tunajiuliza, hivi kati ya wanyama na binadamu nani mwenye haki zaidi ya kuishi? Hata hivyo, wote tunawahitaji, ni jambo ambalo ni la msingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, tunayo hifadhi yetu kule *Maswa Game Reserve* na kuhusu barabara, Mheshimiwa Mbunge wa Serengeti amezungumza vizuri sana. Sisi tuna barabara na mna mitambo mizuri imetajwa kwenye hotuba ya Waziri, kutoka Serengeti kwenda Kibondo mle ndani mwa hifadhi kuna hoteli moja ya *Sopa Lodge* na mle ndani kuna watalii wanapita; ni aibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, atakapomaliza kupitisha bajeti yake na Bunge likiisha, afanye ziara kwenye maeneo yale kwenda kuona zile hoteli zilizoko mle kwenye hifadhi. Ni hoteli kubwa lakini barabara hazipo na huku kila siku tunazungumza tunahitaji fedha kwa ajili ya kupata watalii. Jambo hili kidogo nimwombe sana atusaidie katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, watu wa *TAWA*; wamefanya kazi kubwa ya kushirikiana na wananchi kuzuia hao wanyama waharibifu. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana, ikiwezekana vile vijiji vinavyopakana, vilivyo kandokando, basi na wao wapate nafasi au kama sheria inaruhusu waweze kuandaliwa mazingira ya kuwa wanaingia kwenye hifadhi kule kwenye *buffer zone* kujua maana ya utalii ni nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo utalii tunaouzungumzia hapa ni wa Kimataifa, lakini watu wetu wa ndani hawajui kama kuna utalii na faida yake hawaijui. Kama kutakuwa na watu na kama Wizara itajitolea kuwa inatoa elimu kwenye maeneo hayo husika, ninaamini kabisa jambo hili litapokelewa na mambo yatakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Mtanzania anapopita tu kwenye hifadhi, akikamatwa, kipigo chake ni cha hali ya hatari sana, lakini wale wanaokuja kutembea kwenye hifadhi kwa magari wao hawana shida yoyote. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana, umefika wakati sasa wa kwenda kuboresha sheria zetu na kuboresha mahusiano yetu na jamii inayozunguka kwenye eneo husika, wajue maana ya uhifadhi ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua wanatuletea fedha hizo walizozipata kwenye vijiji vya kandokando, ni jambo kubwa na zuri zaidi wakijua maana ya uhifadhi, ninaamini kabisa migongano itaanza kupungua. Tunajitahidi sana tunaoishi kandokando mwa hifadhi, tukiamua kuyasema yanayotokea kule, nchi inahamia kule yote, ni mambo ya kusikitisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba sana wahifadhi, kupitia taasisi zenu hizo ambazo wameziweka za maaskari ili kusudi wawape elimu ya kutosha, wasiwe maadui, wawe ni watu wa kushirikiana nao kumaliza matatizo. Tunapochukua kwamba, ni maadui nao ni binadamu, wakiamua linakuwa ni jambo zito sana. Bahati nzuri sana, vituo vya uhifadhi tumevijenga kwenye maeneo yetu, tunahitaji hawa watu washirikiane ili wafanye kazi nzuri ya kuhakikisha wanalinda uhifadhi na wanyama wakali

wanaoingia kwenye maeneo yetu. Jambo hilo likichukuliwa, ninaamini kabisa tutafanya vizuri na vilevile itaonesha utayari kwenye maeneo yetu na wananchi wanaotuzunguka kwenye maeneo hayo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili. Wametupatia magari, kulingana na hali ilivyo na haya majeshi, wakati mwingine ninajiuliza, sijui tunawapa kazi ya kuwatesa au kwa sababu, tu ni afisa ndiyo maana inatokea haya mambo yanakuwa ni magumu sana! Watu wanafanya *harassment* angalau kujiokoa katika maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hela inayotoka ni ndogo sana, shilingi 1,000,000 kwa mwezi mzima, mtu hawezi kuendesha ofisi huku anapambana na majangili, anapambana na wanyama wakali, haiwezekani. Umefika wakati hawa binadamu tuliowapa dhamana kwenye maeneo haya ya kulinda hifadhi zetu, basi Mheshimiwa Waziri aangalie namna gani ya kuwasaidia, ili kusudi mambo yaende vizuri na malalamiko yasiwepo katika maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri, pamoja na watendaji wake, Itilima tunayo Hoteli ya *Sopa Lodge,* ipo Barabara inayotoka Kata ya Mwaswale, Kitongoji cha Mwakubija, ni kilometa 120, kuja Mkoani Simiyu, lakini watu waliopo *Sopa Lodge* inabidi waondoke kwenda Arusha, zaidi ya kilometa 420.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifanya ziara wakati ninaomba kura, nilienda mpaka mle porini, nikakuta malalamiko ya wananchi; walisema na mimi niliona kweli, mazingira yaliyopo pale na mitandao ya simu ni changamoto. Ninamwomba Waziri mwenye dhamana kushirikiana na Waziri mwenye dhamana ya mawasiliano ili kuwawekea watu hao mawasiliano. Sisi wakitufungulia pale Simiyu maana yake ni kwamba, mji wetu na utalii vitakua, watu watakuwa wanatoka nje wanaingia kuja huku. Tutaanza kujua kwamba, sasa utalii faida yake ni hii hapa, kama tunavyoizungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wametuletea fedha shilingi 150,000,000, wametuletea mizinga kwenye maeneo yetu, wametupa pikipiki; mambo haya yote yanawezekana, lakini yanahitaji ushirikishwaji. Tuachane na mambo ya kuwa tunaelea juu juu, tushuke chini, wafanye ziara, wazungumze na watu, ili wananchi na viongozi wa ngazi za chini waelewe maana ya utalii, tuondokane na haya malalamiko yanayoendelea kwenye maeneo yetu, haya ambayo tunayasimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea kuwapongeza sana kwa kuendelea kupokea kero na kutatua changamoto. Mheshimiwa Waziri na Naibu wake wanafanya vizuri sana, ninawashukuru sana. Pamoja na hayo yote, ninaunga mkono hoja ya Wizara hii muhimu sana. Ninawashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga.

Nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava. Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri na Mheshimiwa Ali Haidar Madeweyya wajiandae.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii ya Maliasili na Utalii. Kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata kibali cha kusimama kwenye Bunge lako Tukufu kuweza kuchangia, lakini pili, ninamshukuru sana Mhifadhi namba moja, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambayo anaifanya kuhakikisha kwamba nchi yetu inazidi kupaa Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru sana na kuwapongeza viongozi wote wa Wizara hii ya Maliasili na Utalii, nikianza na Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii, Naibu Waziri na Watendaji wa sekta zote ambazo zinahusiana na Maliasili na Utalii. Kwa nini tunawapongeza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka miaka mitano iliyopita Wizara hii ya Maliasili na Utalii inapowasilisha bajeti yake, huwa panakuwa pamoto sana kwa sababu, kulikuwa kuna changamoto nyingi sana. Kwa kiasi kikubwa Wizara hii imeweza

kutatua baadhi ya changamoto ambazo zilikuwa ni kero kwa wananchi na Wabunge kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta hii ya Utalii tumeona inafanya vizuri. Ukiangalia mapato ambayo inaingizia Taifa letu, ni ya pili ikitanguliwa na Wizara ya Madini, kwa hiyo, Wizara hii imekuwa ikifanya kazi nzuri, tunawapongeza sana. Ukiangalia hadi kufikia Disemba, 2025 mapato yameongezeka, kutoka dola za Kimarekani bilioni 3.9 mpaka 4.4. Ndiyo maana tunasema kwamba, Wizara hii kwa sasa hivi kwa kweli, inafanya vizuri, lakini fedha hizi ambazo Wizara hii imekuwa inakusanya zinakwenda moja kwa moja kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapendekeza, kwa sababu hawa watu wana majukumu makubwa, hii Wizara ina mambo makubwa ya kufanya, fedha hizi zingekuwa zinabaki, ili waweze kupanga mipango yao, ili waweze kutimiza yale ambayo Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakiyasema hapa. Fedha ambayo inarudishwa inakuwa haikidhi mahitaji, wana bajeti, wana taasisi nyingi ndani yake, kuna kazi kubwa ya kulinda hawa wanyama wakali ambao wanaingia katika makazi ya wananchi, ninaomba hili liweze kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitu kingine ambacho kinasikitisha sana, kila Mbunge anayesimama anazungumza kuhusu tembo, simba, mamba na tunaposafiri, *let's say,* kama unakwenda Iringa, ukifika Mikumi wamekuwekea kabisa bango, ukigonga tembo utalipa shilingi ngapi, ukigonga swala utalipa shilingi ngapi, lakini hawahawa tembo, na simba wanawaua wananchi wetu. Fidia inayolipwa ni ndogo na hailipwi kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia takwimu katika taarifa niliyokuwa ninaisoma, madai ni takribani 62,446, sawasawa na shilingi bilioni 18.6. Madai yaliyolipwa ni 15,000, madai 47,000 hayajalipwa kwa zaidi ya miaka miwili. Tukumbuke hawa walioathirika ni binadamu, wengine wamepoteza maisha, wameacha watoto, wameacha familia, kwa nini Serikali hailipi kwa wakati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kidogo, faini ni ndogo sana, ile fidia ni ndogo sana, lakini hailipwi kwa wakati, inakatisha tamaa. Hebu gonga tembo sasa au twiga pale, swala amekatiza mgonge, hatua 10 hutembei umekamatwa, umezingirwa, unatakiwa ulipe faini. Serikali yangu Tukufu, tunaomba waliangalie hili, tuwafute machozi wale wanaopata athari kwa wakati. Thamani ya mwanadamu ni kubwa sana hailinganishwi na ile fidia ambayo analipwa, kama kifuta jasho tunavyokiita, basi wafutwe hilo jasho, wafutwe hayo machozi kwa wakati ili waweze kusahau. Miaka miwili mtu anafikiria, kila siku anakwenda kwenye ofisi, kwa ajili ya yale madai hapati, tatizo ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Mheshimiwa Waziri anapokuja ku-*wind up* hapa, atuambie ni lini zile fidia ambazo wananchi wanadai kwa miaka miwili watazilipa na tujue ni kwa nini hawalipwi kwa wakati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha. Wabunge ambao wanatoka kwenye sehemu za uhifadhi wanapata changamoto kubwa sana, kama alivyosema ndugu yangu hapa Mheshimiwa Mary, hatembei na bendera kwa sababu, ataulizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuboreshe na miundombinu yetu; unakwenda *Ngorongoro Crater* kule chini, kuangalia wanyama, unaporudi kama mvua imenyesha gari linazama. Wale watalii badala ya kuangalia simba wanaanza kupiga picha kuangalia ubovu ule wa barabara, baada ya muda unaona kwenye mitandao. Tunaomba hata miundombinu ya kwenye hifadhi zetu iweze kuboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru kwa jitihada ambazo zinafanyika, tunaona kuna viwanja vya ndege ndani ya hifadhi na nje ya hifadhi, tunaomba hata barabara ambazo zinaingia na kutoka kwenye hifadhi ziweze kufanyiwa matengenezo. Nchi yetu imepata bahati sana, tumepata heshima ya kuwa wenyeji wa Mashindano ya *AFCON;* je, kama Wizara, tunadhani mpaka sasa hivi tunavyofanya tumejipanga vya kutosha kuhakikisha kwamba, tunaitangaza nchi yetu kwa vivutio vilivyopo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekwenda Arusha, Kamati ya Utamaduni na Michezo, ukiwauliza wale wananchi ambao wapo pembezoni pale, wengine wanaona kweli, kuna uwanja unatengenezwa, lakini hawajui nini kinaendelea? Wengine wanafahamu kuna *AFCON,* ninachotaka kusema ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji kutangaza utalii wetu katika vipindi vya *television* zote ambazo zinarushwa hapa Tanzania, Wizara iweke *documentary* nzuri ya kuonesha kwamba, nchi yetu inakwenda kufaidika na kitu gani? Kama Sekta ya Utalii, tumejipanga vipi? Hoteli katika Mji wa Arusha, Moshi, Tanga, Manyara na sehemu zote ambazo zinazunguka Arusha zimejipanga vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tujipange, ili tuweze kupata watalii wengi. Tutumie ma-*influencer* wakubwa wa Tanzania na wa nje ya nchi kutangaza. Wenzetu wa nchi ya jirani wanatangaza sana, kuna kipindi hata Mlima Kilimanjaro ulikuwa unasemekana upo nchi ya jirani, kumbe upo Tanzania.  Kwa hiyo, tuendelee kutangaza utalii wetu. Sisi tunawatia moyo, kazi wanayofanya ni kubwa, kinachotakiwa ni kuongeza *speed,* ili kila Mtanzania, kila mwananchi, kila jirani aone kwamba, Tanzania kuna kitu ambacho kinafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu, Wizara hii imekuwa ikifanya vizuri kwa kipindi hiki, sina mengi ya kusema. Ninaunga mkono hoja na kuwaomba waendelee kutangaza utalii, tuendelee kupata watalii wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, lakini siyo kwa umuhimu, ninawapongeza sana Wizara ya Maliasili na Utalii kwa tuzo ambazo wamezipata, tuzo kubwa ya *World Travel Award*. Tukio ambalo limefanyika Jiji la Manama, Nchini Bahrain. Tuendelee kuwapongeza kwa tuzo mbalimbali, hasa Serengeti wamekuwa wakifanya vizuri mfululizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine, ni Waheshimiwa Wabunge, katika Mabanda yale ya Maliasili na Utalii ukienda pale, chukua simu yako piga kura; kuwa mzalendo, pigia kura vivutio vyetu vya utalii vilivyopo Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava. Nilimtaja Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri; Mheshimiwa Ali Haidar Madeweyya na Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko wajiandae.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti hii ya Maliasili na Utalii. Kwanza ninaanza kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutufikisha siku ya leo tukiwa na afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaanza kwa kumpongeza Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayofanya kuitangaza Tanzania katika Sekta ya Utalii. Watanzania wote tumeona jitihada kubwa ambayo imefanyika, tumeona idadi ya watalii ambayo imeongezeka na tumeona jinsi gani tumezidi kupata fedha za kigeni kutokana na utalii. Ninampongeza Waziri, Mheshimiwa Ashatu, Naibu Waziri, Mheshimiwa Chande, Katibu Mkuu na Watumishi wote wanaofanya kazi katika Wizara hii ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaanza kuongelea Hifadhi ya Kilimanjaro na ninaongelea kuhusu Mlima Kilimanjaro. Mlima Kilimanjaro theluji yake imepungua sana ukilinganisha na huko nyuma tulipotoka. Barafu inayoonekana pale juu sasa hivi inazidi kupungua siku hadi siku. Hili ni jambo ambalo linatudhoofisha sisi Watanzania, tukitambua kwamba, Mlima Kilimanjaro ni wa pili duniani, wa kwanza Afrika na ndiyo unaotupa jina la Tanzania, hasa ukiwa katika mataifa mengine, ukisema Kilimanjaro, inamaanisha umetoka Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachotaka kusema ni kwamba, theluji hii imepungua na zipo tafiti ambazo zilifanyika. Mnamo mwaka 2012 zilifanyika tafiti kuangalia ni kwa nini mlima huu theluji yake inapungua, tafiti moja ilionesha kwamba, ifikapo karne ya 20 na 21 barafu itakuwa imekwisha kabisa, jambo ambalo lilishtua sana wale ambao waliiangalia tafiti ile na jinsi

ilivyosomeka. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu sana, mpaka leo barafu haijakwisha, bado tunaiona, japo imepungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naiomba Serikali iangalie kwa makini sana, ifanye tafiti za kina kuangalia kwamba, ni nini kinachofanya ile theluji ipungue, ili ihakikishe kwamba, inafanya kila liwezekanalo theluji irudie uasili wake. Baada ya kusema kuhusu Mlima huo wa Kilimanjaro, zipo changamoto chache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mlima Kilimanjaro umezungukwa na wilaya tano; Wilaya ya kwanza ikiwa ni Rombo, ya pili Moshi Vijijini, ya tatu Siha, ya nne Hai na ya tano ni Longido, lakini vijiji hivi vinavyozunguka ule mlima, kwa maana ya ule msitu, hawajawahi kupata *CSR* kwa zaidi ya miaka mitano. Ni jambo ambalo linasikitisha kidogo, tunatambua *CSR* hizi zinawasaidia wale wananchi wanaolinda ule msitu kufanya shughuli za maendeleo katika maeneo yao. Ninaiomba Serikali yangu sikivu ijitahidi sana tunapopokea watalii, tunapopata fedha za kigeni, tuwaangalie na wale wanaolinda ule msitu, wanaoangalia ule msitu, wale ndiyo wenzetu watakaotuambia leo msitu umelalaje na leo msitu umeamkaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hilo, ninarudi kuchangia katika Wilaya ya Same. Hifadhi ya Mkomazi inaongoza kuwa na faru weusi na pale kuna Mradi wa Faru Weusi. Katika Mbuga ya Wanyama Serengeti na kwingine, hakuna ambayo unaweza ukamwona faru mweusi kwa karibu kama Mkomazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hifadhi ile imeleta watalii sana kwa huyo faru mweusi na wametengeneza utaratibu, mimi ni shuhuda namba moja, ambaye nimekwenda pale kipindi cha kiangazi, wametengeneza matenki ya maji, wametengeneza na maeneo ya kunywea maji; wale wanaishi kwa ratiba. Tulipofika pale wakatuambia subirini ifike saa tisa mtawaona wengi wanakuja kunywa maji. Ni kweli, tulienda na magari, tuka-*park* pembeni, imefika saa tisa wakaja wakiwa wanakimbia kunywa maji. Ni fahari kwa Mtanzania na ni fahari kwa watalii. Ni nini ninataka kusema?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini ninataka kusema, historia inaonesha huko nyuma, mnyama huyu alikuwa hatarini kupotea, lakini Serikali ilifanya jitihada mpaka ikahakikisha kwamba inatengeneza mazingira ya mnyama huyu kuzaliana. Basi, Serikali hii iendelee kutengeneza mazingira mengine katika hifadhi zingine ili mnyama huyu anayependwa na watalii aendelee kuwepo Tanzania kwa wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipo vivutio vingine vingi sana katika Mkoa wa Kilimanjaro ndani ya Wilaya ya Same. Upo Mlima wa Shengena, upo pia Mlima wa Kidenge. Mlima huu kwanza ni mrefu sana na ni mlima ambao una kona nyingi, wenyewe huu mlima ni utalii tosha. Kwenye mlima huu wa Kidenge kuna pango moja katikati ya milima, ukiingia ndani utaona maajabu ya Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko ndani kwenye pango hilo utakutana na ng'ombe, utakutana na mbuzi, utakutana na punda ambao hawana mwenyewe na wanyama hao wanajiongoza wenyewe. Ukifika wakati wa jioni utaona wanyama hao wamejitenga hata maeneo yao ya kulala. Ndama zinalala kivyake na wakubwa wanalala kivyao na wakirudi asubuhi, wanapotoka asubuhi wanaanza watoto ndiyo waje wakubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani utanipa dakika zangu za kukohoa, ninakohoa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiingia katika pango hilo watalii zaidi ya mia nane wameenda kuona lile pango, hicho ni kivutio kizuri sana na hata Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mheshimiwa Angellah Kairuki ameshafika huko, ni shuhuda na akina Mzee Malechela walienda ku-*visit* baadhi ya maeneo huko, wako na viongozi wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali ihakikishe kwamba vivutio kama hivi wavitangaze na kutengeneza mazingira mazuri ya watalii kufika ili kuongeza mapato, kwanza kwa Wanasame wenyewe na kwa Taifa kwa ujumla, niiombe sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongea kuhusu tembo, mimi nimezaliwa katika Kata ya Maore. Ninavyoongea sasa hivi hapa, Diwani wa Kata husika yuko kwenye kikao cha wananchi kupanga utaratibu wa watu kwenda kuhakikisha kwamba wanapambana na tembo. Tembo wameingia usiku wa jana katika Vijiji vya Kadando, Muheza na Kizerui hapafai! Ndege nyuki zimetusaidia ila naona sasa wameshazoea ndege nyuki, sijui Serikali tutatumia utaratibu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Serikali, hii Kata ya Maore imejengewa mpaka Kituo cha Wanyamapori, lakini hali halisi ya tembo inaonekana kule porini hawapati maji na wakikosa maji ndiyo pale wanapoingia katika mashamba ya wananchi na kuanza kuharibu mazao ya wananchi. Ninaomba sana Serikali iangalie hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho tunasikitika sana, baada ya Waziri Mkuu kufanya ziara yake kule, zilitoka hoja za watu kutolipwa stahiki zao za vifuta jasho na kwa wale waliofariki, lakini inasemekana kwa taarifa niliyopewa na Diwani husika, fedha zile zilitolewa kipindi kifupi Waziri Mkuu aliposema, lakini sasa hivi zoezi limesitishwa. Ninaomba Serikali iwasaidie wananchi, hawana pengine na wala hawana maisha mengine zaidi ya kilimo. Serikali iwape vifuta jasho vyao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niseme ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, nikiamini kwamba changamoto za wananchi Serikali itazifanyia kazi kwa karibu sana. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Zuena Bushiri. Nilimtaja Mheshimiwa Ali Haidar Madeweyya, Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko na Mheshimiwa *Engineer* Kija Ntemi ajiandae.

**MHE. ALI HAIDAR MADEWEYYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii asubuhi ya leo ili kuchangia katika Wizara muhimu sana ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maono yake makubwa sana katika kuongoza

Taifa hili, lakini pia yeye ni *champion* namba moja katika masuala yetu ya utalii. Sisi kama Wabunge, katika kitu cha msingi sana kwenye utalii ni *brand* na *marketing*. Hii Wizara inaongozwa na *brand* pamoja na *marketing*, lazima Wizara kupitia taasisi zake ilione hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajielekeza moja kwa moja katika *retention fund.* Tunashuhudia *TANAPA* na Ngorongoro jinsi gani inavyopambana katika kukuza mapato ya kiutalii, lakini cha ajabu, *TANAPA* na Ngorongoro hizi fedha zinakwenda moja kwa moja wanakusanya *TRA*. Hili ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANAPA* na Ngorongoro wakishakusanya, hizi pesa zinakatwa kodi 18%. Pesa hizi hizi zinazokusanywa na *TANAPA* na Ngorongoro zinakatwa asilimia sita ya *Tourism Development Levy*. Pesa hizi zinakatwa asilimia tatu ya *Tanzania Wildlife Protection*. Sasa kinachobaki ni 50% kwa 50%, pasu kwa pasu. Kufanya hivi tutaziua hizi taasisi. Wanajitahidi kufanya kazi, lakini tufahamu kama nilivyozungumza mwanzo, tunapozungumza Wizara ya Utalii ni *brand* pamoja na *marketing*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu nchi jirani sitawaogopa kutaja kwa sababu juzi Rais wao alikuja Kenya, kupitia *Kenya Wildlife Service* mapato yote wanayokusanya wanaachiwa wenyewe. Niombe sana Serikali sikivu ya Mama Samia na Waziri wangu wa Fedha, waliangalie hili. Tunashindana na mtu ambaye ni *giant*. Maana yake hizi fedha wanazokusanya waachiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kenya wameenda mbali zaidi, ukiondoa mapato wanayokusanya kuachiwa, wanatoa ruzuku ya 10%. Tunalifahamu hilo, sasa tunakwenda kushindana na mtu ambaye ana *full support,* nini kinachokuja kutokea, athari ya *TRA* kuendelea kuzihodhi hizi pesa, kwanza wanapozirejesha ndiyo makato yale niliyoyataja, wanarejesha kwa kuchelewa au wanarejesha kwa pungufu na wanagawa nusu kwa nusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kweli tutegemee miundombinu na *infrastructure* ya hifadhi zetu kweli? Tutakuwa kila siku tunakuja hapa tunapiga kelele hakuna hicho kitu. Kama kweli tumeamua

kwa makusudi tufanye maamuzi magumu, hakikisha haya mapato si ya kikodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema wanachaji *VAT*, ufanye uzalishaji ubadilishe thamani ya kitu kama ni kilimo umelima, matunda unatengeneza *juice*, unakwenda ku-*impose tax* pale, haya siyo mapato ya kikodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana pia ndugu yangu *Commissioner General* Mwenda akaona akiyaachia haya mapato inawezekana, ika-*reflect* athari ya mapato au ukusanyaji wake kule *TRA*, atafute mbinu mbadala na wala si aibu, aseme mapato yake anayokusanya yeye kama yeye na haya ambayo yanayokusanywa na *TANAPA* na Ngorongoro. Ku-*declare* hili, wala si aibu, asichukue majukumu mengine ya taasisi nyingine. Langu lilikuwa ni hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine katika *issue* ya *TFS*. Muda sasa umefika *TFS*, *(Tanzania Forest Service)* ijiendeshe kibiashara. Leo tunawaambia tu hifadhini, hifadhini. Tukishahifadhi tunafanya nini? Mfano mzuri sisi tumezaliwa na wazee, tumekua, tukasema tunataka kuoa na kuolewa. Maana yake tunda likiiva liliwe, *TFS* wakati umefika watafakari kwa kina wajiendeshe kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaposema mali unaiona ile pale hifadhi tu ataitumia nani? Pia *TFS* wana tatizo, wakati mwingine wanawaruhusu wananchi wetu kulima kilimo kile cha muda mfupi. Waziri akitoa maelekezo bwana wee tunakuja kufanya operesheni au *TANAPA*, unakuta kilimo kama cha mahindi *just* kinahitaji miezi mitatu au mitano, wawavumilie wavune kisha wazuie. Unakuta wanawakamata bodaboda kwa kupakia mkaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa ambao walioenda kuchoma huu msitu *TFS* walikuwepo wapi? Si kitu kizuri. Hivi karibuni tulishuhudia pale Mbarali, mazao ya mpunga umeshachipua unakaribia kuvunwa, wameenda kumwagia madawa magugu maji. Hii nchi ni yetu sote. Niwaombeni sana *TANAPA*, *TFS* na Wizara kwa ujumla. Waziri atakapokuja ku-*wind* hapa, mimi ninamheshimu sana dada yangu pamoja na kaka yangu

Chande, sina *interest* ya kuzuia shilingi, lakini basi watujibu vizuri, ubinadamu wakati mwingine utumike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda umefika kwa Wizara pamoja na tuzo alizotusomea hapa mama yangu, Mheshimiwa Waziri ni nzuri, lakini wenzetu Rwanda wanasema pale *Visit Rwanda*. Hebu na sisi tutafute kitu kitakachokuwa *branded* kama nilivyozungumza awali. Hii ni wizara ya *marketing,* lakini vilevile ni Wizara ya *brand*. Tuweke watoto wadogo pale wa kike wengine maradhi yao ni hayo, kwa maana hiyo tutafute kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu Rwanda wamesema *Visit Rwanda*, wanaingiza hela nyingi *to be honest*, sasa na sisi Tanzania tunaweza tukasema *Visit TANAPA*, tujipange, tutafute hao ma-*tycoon* huko duniani tuingie nao mikataba kuwa na *special*. Tunaweza tukasema *Visit Royal Tour,* yaani tuangalie *something special,* wakati umefika sasa tusijifungie ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho si kwa umuhimu, nipende sana kuishauri Wizara yangu ya Maliasili na Utalii katika suala la mpango wa matumizi ya ardhi. Kweli kuna kero za wanakijiji pamoja na hifadhi, lakini hebu tu-*review* upya mipango yetu ya kijiji. Tunaweza tukapunguza hizi changamoto za ugomvi baina ya wananchi wetu pamoja na hifadhi. Unaweza ukakuta kuna hifadhi nyumba iko hapa nyingine iko mbali *scattered* lakini hebu tufanye *review*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Uzini walionituma kuja kuwawakilisha, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ali Haidar Madeweyya. Nilimtaja Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko; Mheshimiwa *Engineer* Kija Limbu Ntemi na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere wajiandae.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia fursa kuchangia Wizara ya Maliasili na Utalii. Wizara ambayo ni muhimu sana kwa uchumi wa Taifa letu, Wizara

ambayo tukiwekeza kwa kiwango kikubwa sana tutakwenda kuongeza fedha za kigeni nyingi na kukuza uchumi na pato la Mtanzania mmoja mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wa Wizara husika kwa jinsi ambavyo wamekuwa wakijitahidi kuhakikisha kwamba Wizara hii inaweza kuwa moja ya chanzo si tu cha kuitangaza nchi yetu na vivutio vilivyopo, lakini pia kuhakikisha kwamba tunakuza utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nimpongeze Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwenye hotuba wamemweka kama mhifadhi namba moja na mwongoza utalii namba moja. Ni dhahiri kabisa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uongozi wake thabiti kabisa, uthubutu, ujasiri na ubunifu alikuja na *Royal Tour* na wote hapa tumesimama tunachangia tunai-*praise Royal Tour* kwa sababu tumeona matokeo chanya ambayo ameleta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi kile ameanzisha *Royal Tour* iliweza kufufua sekta ya utalii. Wote tunajua baada ya *pandemic* ya *COVID-19* utalii uliyumbayumba kidogo ,lakini *through Royal Tour* walau tena tukarudi kwenye mstari na utalii ukaja na mapato yakaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aliweza pia kutumia *Royal Tour* kuhakikisha kwamba anatangaza vivutio vyetu vya utalii, lakini kuelezea mambo mbalimbali ambayo yako ndani ya nchi yetu ya Tanzania ambapo mtalii akija anajua kabisa nikienda Tanzania nitakutana na mambo mbalimbali. Kupitia *Royal Tour* tuliona Dkt. Samia Suluhu Hassan aliweza kukutana na wawekezaji wakubwa wa mahoteli na wengine ambao wanaweza kuongeza mnyororo wa thamani kwenye sekta ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya utalii ni kubwa sana na ni sekta muhimu sana kwenye ukuaji wa uchumi, kama ambavyo ameeleza kwamba inachangia 17% kwenye *GDP* lakini pia 25% kwenye fedha za kigeni. Ukweli wa mambo ni kwamba tukiweza kuongeza kwenye thamani ya mnyororo wa utalii, sekta ya utalii ina uwezo wa kuchangia na ikawa ya kwanza, ikachangia hata

zaidi ya 60% ya fedha za kigeni ambazo zinakuja ndani ya Taifa letu, lakini pia inaweza ikachangia zaidi ya 17% inayochangia leo kwenye *GDP* ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa yale ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameyafanya katika *Royal Tour* ni wajibu sasa wa Wizara hii kwa kushirikiana na watendaji kuhakikisha kwamba kwanza inalinda yale mafanikio yote ya *Royal Tour* ambayo yalipatikana, ili tuendelee kuona tunaongeza kufikia hiyo ambayo tumejiwekea ya watalii 8,000,000 *by* 2030. Pia iendeleze mafanikio haya kwa kuhakikisha kwamba inaongeza matumizi ya miundombinu iliyopo kwa maana ya *occupancy rate* na *utilization rate* walau ifikie 100% ya hoteli ambazo tunazo zote Tanzania kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona pia hapa wamesema viwanja mbalimbali vimejengwa basi viwanja hivi vyote viwe *busy by 100%.* Pia tuhakikishe mbuga na vivutio vingine vya asili tulivyonavyo vinatumika *to the maximum* ambapo sasa itaenda kuongeza pia na kutoa fursa ya kuhakikisha kwamba tunakuza pato letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ihakikishe kwamba inafufua miundombinu yote iliyolala. Katika Taifa letu hapa ninavyoongea na katika uwekezaji tunajua ni mahoteli na miundombinu, barabara, viwanja vya ndege na *the like*. Ninavyoongea sasa hivi kuna mahoteli ambayo yametelekezwa ninaweza nikasema na hapa kwa kweli Serikali ione kabisa kwamba ni wajibu na tumebarikiwa kuja na *AFCON*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, hoteli kama ile ya *Embassy* ambayo iko pale Dar es Salaam, *Motel Agip*. Zote hizi zimetelekezwa. Ni *high time* sasa Serikali iweze kuona kama kuna mgogoro wowote unamalizika na inafufuliwa. Ni hoteli ambayo ina hadhi ya kutengenezwa kuwa hoteli ya nyota tano, lakini tumeitelekeza miaka mingi pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna mashirika yetu haya, *NSSF* na *TANAPA*, walikuja na uwekezaji wa mahoteli ya nyota tano, kule Mwanza na Mzizima *Tower* kule Dar es Salaam, takribani ni

miaka 10 mahoteli yale hayakamiliki wala ku-*take off*. Hapa sasa tunakuwa tunafifisha. Wizara ya Maliasili na Utalii ishirikiane na Wizara husika kuhakikisha kwamba inaendelea kuongeza mnyororo wa thamani kwenye sekta ya utalii na kuweza kukuza utalii wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamezungumza hapa na kweli tunajipongeza. Tumeongeza thamani, tumeongeza watalii. Tunakuwa tuko namba sita kwa Afrika, namba 11 kidunia, lakini uhalisia ambao tunaweza tukaongea kutoka kwenye mioyo yetu kwa jinsi tulivyobarikiwa vivutio vya asili, tukijilinganisha na mataifa mengine bado hatufanyi vizuri. Nikajaribu kurejea takwimu *Royal Tour* imetu-*boost* mpaka tumefika takribani bilioni 2.5 kwa mwaka 2025, tukilinganisha na wenzetu kutoka nchi za Afrika Mashariki, mathalan Kenya, wenyewe 2025 walikuwa na watalii, ninazungumzia wa nje hata hawa wa ndani hapa na-*quote figures* za nje, walikuwa na watalii milioni 7.9.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda upande wa *SADC* walikuwa na watalii milioni 10.5, ukienda Misri kule na Morocco 10,000,000 zaidi *every year* wanakuwa na watalii. Kiafrika kwa mwaka 2025 kulikuwa na watalii 81,000,000. Sasa sisi vivutio vyote tulivyonavyo, watalii milioni 2.5, ukilinganisha tunachangia vipi katika wale watalii 81,000,000 wanaokuja Afrika utaona kwamba ni kwa asilimia 2.8 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii tunaona Amiri Jeshi Mkuu amejitolea kutangaza vivutio, watendaji wa Wizara husika ya Maliasili na Utalii *it is high time* wahakikishe wana-*exhaust* vivutio vyote vya asili ambavyo tumepewa na Mwenyezi Mungu, tunavitangaza na tunawekeza vya kutosha, tunaenda mbali kuwa na vivutio vya kutengeneza, *artificial attractions*, ambazo pia tumeona mataifa mengine wana-*capitalize* huko waki-*supplement* na vile vivutio vya asili tulivyonavyo, wanaongeza idadi kubwa ya watalii wa kigeni kuja kwenye nchi husika na kuongeza mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mathalan, ukiangalia Tanzania, kwa mwaka jana 2025 kwa vivutio hivi vya kutengeneza kwa maana ya makumbusho tuliingiza watalii 25,570, lakini ukijaribu

kulinganisha na mataifa mengine wenyewe wana vivutio vingi, *cultural heritages* za kutosha, *I mean heritage tourism,* kwa mfano ukienda Misri na Morocco wana *pyramid*, wana *medinas,* wengine wana *theme park*, tunazo *theme park* lakini siyo zile kubwa za Kimataifa kuweza kuvutia watalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende kwenye *digital hubs* pia, tuhakikishe tunawekeza huko. Tuwe na *virtual reality;* yaani mtu hata kama hawezi kuja kwa mfano kwa *pandemic,* kupitia *VR tourism,* wanaweza wakawa wapo huko wamekaa kwenye nchi mbalimbali, lakini wana-*view* vivutio tulivyonavyo halafu wanalipa *through digital, digital marketing* kwa kutumia hiyo *VR*. Pia tunaweza tukatumia *augmented reality tourism*. Mtu anaweza akawa amekuja hapa lakini akaangalia, kwa mfano yuko *Stone Town,* siyo lazima aingie kule ndani, anatumia hiyo na kuweza kupata. Tu-*exhaust* kama mataifa mengine ambavyo wanafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi, pamoja na kwamba tunapongeza lakini bado, *we need to do more*. Kama Mheshimiwa Rais amefanya hivyo na watendaji wahakikishe wanafanya zaidi kuhakikisha kwamba tunaletea Taifa letu mapato zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Serikali na pia ninaipongeza zaidi Wizara ya Uchukuzi. Ndiyo maana ninasema kwamba wale wanaohusika na mambo ya hoteli, uchukuzi, ujenzi, na miundombinu ya barabara wafungamane. Tumeona uchukuzi wanakuja kujenga viwanja vya kisasa na vya kimataifa ikiwemo Njombe, Bukoba na kule kwetu Serengeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza kwa sababu hivi ilivyo sasa hivi; ninatambua wakati wa uchukuzi kulikuwa na *debate* kubwa sana; lakini niliwaambia Watanzania kupitia Bunge hili Tukufu: Mbuga ya Serengeti, achilia mbali kwamba inachangia sana kwenye mapato ya Taifa letu, lakini pia ukijaribu kuangalia miruko ya ndege kwenye Mbuga ya Serengeti; nilikuwa ninajaribu kupitia baada ya *debate* kubwa; tulikuwa na jumla ya miruko ya ndege 52,593 kwa mwaka uliopita. Kwa maana ndege zile za wakati wa mchana 20,262; za usiku zinazotua 4,691; na zile ambazo zinapita kwenye anga 27,640.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi pia ninatoka Kanda ya Ziwa, na ninautamani sana uwanja wa Mwanza pia ujengwe katika hadhi ya kimataifa, lile jengo na kwingineko. Sasa vyote vina thamani. Ukiangalia miruko ya ndege kwa uwanja wa Mwanza ilikuwa wakati wa mchana 9,830; usiku 1,063 na ile *overflight* ilikuwa 5,000, jumla ni 15,000. Sasa nikija kwa uwanja wa Serengeti wenye miruko 52,000, inaonesha dhahiri kwamba uko *busy* sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni uwanja ambao tukiujenga kuwa uwanja wa kimataifa; wenzetu upande wa pili wa Maasai Mara wanajenga uwanja wa kimataifa na sisi Tanzania tujenge uwanja wa kimataifa ili tuongeze mapato ambayo yatatumika kujenga miundombinu mingine, ikiwemo barabara na viwanja vingine kote Tanzania. Kwa hiyo, niiombe sana wizara, ihakikishe inatekeleza hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kengele imegonga, nilikuwa bado nina *points* za *AFCON* na kuhusu kupeleka fedha, zikikusanywa zisiende kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina, wabakishiwe hawa watu ili waweze kuboresha miundombinu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimalizie, kwenye *AFCON* tunapata neema kubwa sana. Tukitumia vizuri na wizara wamekiri kwamba watapata zaidi ya dola bilioni mbili. Hata hivyo, ukweli wa mambo ni kwamba, hatuna hoteli toshelezi zenye hadhi za kuweza ku-*host* wale wageni wanaokuja. Wamesema wanaoingia viwanjani ni milioni 1.8, lakini hata tukisema tuna wageni 300,000 wa kuweza kuwalaza, hoteli tulizonazo hazitoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliuliza swali Bungeni wakaniambia, wananchi wanaweza wakafanya *Airbnb*. Tujiulize, mwananchi wa kawaida akifanya *Airbnb* atakuwa na ile hadhi ya kuweza ku-*host* hao wageni wa kimataifa wanaokuja? Kwa hiyo, kuna kazi kubwa ya kufanya kuhakikisha kwamba tunaweka miundombinu, hasa ya malazi ili tusije tukawa-*dissapoint* baada ya *AFCON* tukajikuta tunakosa watalii ambao wanakuja Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaomba nikushukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Esther Matiko. Tunaendelea na Mheshimiwa Festo Sanga, Mheshimiwa *Engineer* Kija Ntemi, Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere ajiandae.

Mheshimiwa Festo hayupo, Mheshimiwa *Engineer* Kija Ntemi na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere ajiandae.

Mheshimiwa *Engineer* Kija pia hayupo! Mheshimiwa Mwita Getere, kama hayupo Mheshimiwa Kija.

Ninamwita Mheshimiwa Mwita Getere kwa sababu nimeona Mheshimiwa Kija sijamsikia.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Kwanza, ninawashukuru sana viongozi wa Wizara, tukianza na Waziri wake Mheshimiwa Ashatu, Naibu Waziri wake Mheshimiwa Chande, Katibu Mkuu Ndugu Abbas na Naibu wake na watendaji wote wa wizara. Pia niwashukuru Makamishna wote, Kamishna wa *TAWA*, Kamishna wa *TANAPA*, Kamishna wa *TFS* na wasaidizi wao wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nimshukuru Mheshimiwa Rais. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa sababu amefanya maamuzi ya dhati ya kujenga Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Utalii Serengeti. Amefanya kazi nzuri sana, amefanya urithi mkubwa sana kwenye wilaya yetu na hasa Mkoa wetu wa Mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninamtazama sana hapa Mbunge wa Serengeti, Mheshimiwa Mary, hadi ninamhurumia. Leo ni miaka 75 ukianzia 1959, Serengeti ilipojitenga kutoka Ngorongoro, lakini ukienda pale Serengeti wilayani, ni wilaya pekee ninadhani kwenye Nchi ya Tanzania ambayo haina barabara ya lami inayotoka kwenye wilaya hiyo. Ni wilaya ambayo leo hata ukiingia halmashauri, huoni kama kuna halmashauri; miaka 75, lakini Serengeti ni hifadhi yenye ubora duniani na imepata tuzo kila mahali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, kwa kweli nilikuwa ninamwomba mama, Mheshimiwa Mbunge wa Serengeti, hasa wakati wanajenga lile jengo, atafute sanamu kubwa sana aweke

pale, halafu aandike sanamu ya Mama Samia. Hii ni kwa sababu sasa Serengeti itapanuka; lakini hata sisi ambao tulikuwa na barabara zimekwama; Barabara ya Sanzate – Natta – Mugumu itakuwepo na barabara zingine za kutoka Tarime zitakuwepo. Ninamshukuru sana mama, ametushika kwenye jambo hilo.

Mheshimiwa Mweynekiti, kingine ambacho amefanya kikubwa ni kutoa takribani shilingi 45,000,000,000 za kwenda kujenga Uwanja wa Ndege wa Mwanza. Kwa hiyo kanda nzima yote itakuwa imesheheni miradi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninaona Waheshimiwa Wabunge humu ndani, wengi tu, ooh sijui Wizara ya Maliasili, ooh tulinde tembo, ooh tujenge miundombinu, ooh tulipwe sijui ujirani mwema, ooh tulipwe nini; watatoa wapi fedha? Watatoa wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imeanza mwaka 1961. Awamu ya kwanza ya Baba wa Taifa ni miaka 24; awamu ya pili ya mzee wetu Mheshimiwa Mwinyi ilikuwa miaka 10; hiyo inakuwa miaka 34. Awamu ya tatu ilikuwa ya Mheshimiwa Mkapa, miaka 10; inakuwa miaka 44. Awamu ya nne ya Mheshimiwa Jakaya miaka 10; miaka 54. Ukiacha hii ya mzee Magufuli na wa sasa tuliyenaye, Awamu ya Tano na Awamu ya Sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka 54 Serikali haijawahi kuchukua fedha za hifadhi. Wanajua urithi pekee tulionao Tanzania ni mambo ya hifadhi za Taifa, maana ardhi tunaweza kuishi ikaisha yote. Hifadhi ambazo tunazo fedha zake, kama za *TANAPA, TAWA, TFS* tumezikatalia. Huko nyuma uchumi wetu ulikuwa uko chini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo *GDP* ya Tanzania inaelekea kuwa dola 100,000,000,000. Tuna vyanzo vingi vya mapato, ni kwa nini hatutoi fedha za *TANAPA, TAWA* na *TFS?* Kwa nini? Tulishatoa azimio humu ndani kwamba fedha ziende. Wanaendaje kufanya kazi? Wanaendaje kuimarisha vivutio? Wanaendaje kufanya kazi ya mama, ambaye anaifanya ya *Royal Tour*? Wanaendaje kuifanya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Rais, kwa sababu kwa Waheshimiwa Mawaziri tumesema, inaonekana hawakubaliani, Waziri wa Fedha na *TRA* wanazikatalia fedha hizi zote. Mama aingilie kati, watu wapewe fedha watutengenezee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo katika Jimbo langu la Bunda tembo wako kila mahali. Jana tembo wamezaa watatu, wako hapa, watu hawapiti, wanazalia kwenye nyumba za watu. Wataendaje kuwatoa ikiwa fedha hamna? Hakuna fedha. Sasa, tumwombe Mheshimiwa Rais aingilie kati jambo hili, vinginevyo watu wetu watakufa, kila kitu hakitafanyika, utalii wetu utarudi nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tuna *AFCON;* na niipongeze sana *Azam TV*. Leo wamepewa kuonesha mechi 104 za Kombe la Dunia. Hii ni sifa kubwa sana kwa Tanzania. Sasa kazi ya watu wa utalii ni kupeleka matangazo pale, waende wakasaidie yale matangazo ili *AFCON* yetu sasa ipendeze na utalii wetu kupitia humu ndani uweze kuwa mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo si lazima tu tufanye kazi ya uwindaji au ya utalii mchana. Nchi nyingine, nimeona South Africa, Botswana, Thailand na Australia wanafanya kazi ya utalii usiku. Sasa mama akishatoa hela *TANAPA,* warudi na hela zao na *TFS* na watu wa *TAWA*, aende *Royal Tour* ya pili sasa. *Samia Royal Tour Phase II,* aende akaanzishe utalii wa usiku, aende *Speke Bay* ya Nyatwali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Nyatwali imechukua eneo, tusipoangalia itabaki pori tu pale. Kwa hiyo, waende kwenye Ziwa Victoria ambalo sasa limekamilisha maajabu ya Hifadhi ya Serengeti. Mama aende pale afungue utalii wa ziwani kule ndani, watu wale na mitumbwi, wafanye kazi zao. Mama aende kwenye eneo lile la uhamiaji, akaone nyumbu wale ambao wanavuka usiku na mchana wakiwa na wapambe wao, swala na pundamilia; aende pale ashuhudie. Sasa hiyo, baada ya kuifanya hiyo awe ametoa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna wanyama wametuzunguka sana. Kampuni ya *VIP* ambayo ni *Grumeti* imekubali kujenga *fence*. Serikali hawajakubali wajenge. Wapewe ruhusa ili watujengee *fence* ya kuzuia wanyama. *Fence* ile nishaona matunda kwenye maeneo mbalimbali, wenzetu wa Kenya, Botswana, South Africa wameweka. Waweke *fence,* vinginevyo Jimbo la Bunda watuambie sasa kwa mwaka wanatulipa shilingi ngapi? Maana tembo wapo, kila siku wanazaliana pale. Nimesema jana watatu wamezaa pale, lakini juzi waliua mtu mmoja anapeleka mwanafunzi. Kwa hiyo, tuombe kwamba sasa tuwekewe *fence.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri pamoja na Katibu wake wanaweza. Mwekezaji wa *VIP* wa *Grumeti* amekuja pale miaka ya karibuni tu, akazuia watu kuwinda, tulikuwa tunapewa nyama. Hifadhi ya *Grumeti* ilikuwa inachukuliwa kama *open area* ya watu wa Bunda, Serikali ikaichukua ikasema itakuwa inawalipa. Wakaja na mtindo wa kutupa nyama kwenye *quota.* Wakaja *Grumeti* wakasema kwamba jamani waacheni hawa wanyama, tutawalipa fedha. Wakaanza na shilingi milioni mbili, wakaja na shilingi milioni nne. Sasa juzi wamekataa hawalipi, wanasema Serikali imewazuia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niseme tu, tafadhali waende wakawaambie watulipe fedha, hii vita hawaiwezi. Hatuwezi kunyimwa fedha halafu tena watu wetu wanakufa kila siku, haiwezekani. Wawaambie wakatulipe, vinginevyo hii vita hawawezi. Hii ligi ni ngumu sana. Waende watulipe hela zao walizokuwa wanatulipa, kwa sababu sisi ni majirani zao. Mungu hakuwa mjinga alivyosema mpende jirani yako kama unavyojipenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere. Tunaendelea na Mheshimiwa Fadhili Ngajilo; Mheshimiwa Alan Thomas Mvano na Mheshimiwa Kijakazi Yunus Mohamed wajiandae.

**MHE. FADHILI F. NGAJILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa nafasi hii, lakini pia niwashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Iringa Mjini kwa kuniamini na kunipa kura nyingi sana ambazo ninawahakikishia kwamba nitaendelea kuwatumikia kama mtumishi wao mwaminifu kabisa. Nichukue nafasi hii pia kumshukuru sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri na maono yake mazuri juu ya utalii na maliasili ya Nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kabla sijaanza kuchangia bajeti yetu, niombe leo Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii aniwie radhi; kwamba atakutana na wageni wametoka Mkoa wa Iringa. Nimewaleta wageni hawa wanahitaji kusikia sauti yake. Hawa ni Chama cha Wawindaji Mkoa wa Iringa. Kuna malalamiko juu ya ugawaji wa maeneo ya uwindaji Mkoa wa Iringa. Hawa ni wenyeji pale Mkoa wa Iringa, wamelalamika tangu mwaka 2024 na ushahidi ninao hapa, lakini hawasikilizwi. Mimi mwenyewe nimejaribu kuingia kwenye vyombo kuulizia, kwa nini hawapewi nafasi ya kuwinda kama ilivyokuwa asili ya Wanairinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka mingi sana Wanairinga shughuli yetu imekuwa ni ya wawindaji, lakini hawa hawapewi maeneo ya uwindaji na wakiuliza wanambiwa maeneo yamepewa wawekezaji. Sasa haiwezekani, rasilimali iko ndani ya Mkoa wa Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tulidhani kipaumbele ni kwa wananchi wa Mkoa wa Iringa halafu mwekezaji aje kwa maeneo ambayo sisi tumeshindwa kuwinda. Kwa hiyo, leo nina wageni ambao wako hapa wakiongozwa na viongozi wao akina mzee Kiponza pamoja na Askofu Mpeli wako hapa kwa ajili ya kusikia kauli yake, yeye mwenyewe Mheshimiwa Waziri, kwa sababu kama ni ngazi zingine wameshapita sana. Mimi Mbunge pia nimekwishaulizia nikaona kule tayari kuna jiwe na hilo jiwe anaweza akalisukuma yeye tu ninavyoliona. Kwa hiyo, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri atusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nijikite kwenye mchango na mchango wangu utakuwa sehemu moja tu, kwenye idara ya mambo ya kale.  Idara ya Mambo ya Kale pale kwa maoni yangu; katika utajiri wa nchi hii, kwenye vivutio vya nchi hii, mambo ya kale tuna vivutio vingi sana, tena hata kupita sehemu nyingine, lakini havitangazwi. Ninadhani kwamba hata tunapozungumzia *AFCON* hawa wageni ambao watakuja wangeipenda sana wapate ile *package* ya vivutio vya mambo ya kale. Hii itaongezea vivutio tulivyonavyo na wao waje washuhudie vivutio ambavyo tunavyo katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna vivutio katika maeneo; tuna mawe ya kale, chuma, ceramics *(vyungu),* shanga za zamani, vyuma ambavyo ni *iron tools* ambazo zinapatikana hapa hapa Tanzania na mambo mengine mengi mengi. Vilevile kuna mapango na kadhalika, kama walivyozungumza wazungumzaji wengine. Kikubwa kinachotakiwa ni kutangaza hivi vivutio na kuvifanya kuwa *package* ambayo itaongeza *value* ya utalii na hivyo kumfanya mtalii aongeze siku za kukaa hapa Tanzania. Kama amekwenda kuona wanyama basi apate muda pia wa kuona vivutio hivi vingine vya malikale, ambavyo vipo vingi sana ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wizara wana uwezo wa kujiongeza, wakaongeza *product* nyingine kwenye eneo la malikale. Wenzetu wa *Korea* wamewekeza sana kwenye hilo eneo la historia na malikale. Wameamua kuwekeza sana kwenye filamu kwa mfano. Yaani wamefungamanisha malikale na filamu. Kwa hiyo, wanatengeneza hizi picha na wanauza nyingi sana. Ukiingia kwenye mitandao ya *Netflix* utaona picha zinauzwa nyingi sana za Wakorea za kihistoria. Utaona kwa mfano wale waangaliaji wazuri wa picha za Kikorea, unaona picha inaitwa *Goguryeo*, *Baekje*, *Shilla.* Hizi zote ni picha za Kikorea ambazo zinauza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Gazeti la *Oxford Economics,* mwaka jana tu 2025, wameingiza *US Dollars* 19,000,000,000 ambazo ukizigeuza kwa hela ya Kitanzania *almost* shilingi 41,000,000,000,000. Wameingiza hizo fedha mwaka jana kwenye hilo eneo tu, wamefungamanisha tu filamu na historia yao na mambo yao ya kale na unaona wanauza sana hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninataka kuishawishi wizara, kwamba ijiongeze kwa kuweka *products* zaidi kwa ajili ya kuongeza ajira zaidi. Kwa mfano, Wakorea mwaka jana pekee wameingiza ajira zaidi ya 211,000 katika eneo la historia na mambo kale tu, kwa mujibu wa hili gazeti la kimataifa la *Oxford Economics.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka hapa niongezee kwa kusema, idara hii ya mambo kale ipewe sauti zaidi, iwe na sauti, iwe na uwezo wa kusikika. Ninaamini kwamba wangekuwepo maafisa mawasiliano wazuri pale kwenye Idara ya Mambo Kale, wangeweza kuwa wanazungumzia habari ya mambo kale na Watanzania wakajua na dunia ikajua kwamba Tanzania kuna malikale hii na utajiri huu mkubwa ambao uko ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna dhana potofu, kwa mfano hizi ambazo zinasema binadamu ni sokwe. Tungekuwa na idara ya mambo kale ambayo iko *active,* hapa ndipo mahali pa kufuta dhana za namna hiyo. Kuwaeleza Watanzania kwamba hakuna mambo ya kusema kwamba binadamu eti ni sokwe, kwa sababu wao wana ushahidi, watu wa mambo kale wana ushahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Elimu wao wanafundisha lakini watu wa Wizara ya Maliasili na Utalii wao ndiyo wenye ushahidi, inaeleweka, kwamba hakuna kitu cha namna hiyo; kwamba binadamu ni binadamu, sokwe ni sokwe na binadamu ana *lineage* yake kutokea enzi za *australopithecus, zinjanthropus* sijui *australopithecus afarensis, australopithecus boisei,* baadaye *homo habilis,* baadaye *homo erectus*, baadaye unampata *homo ergaster.* Hizo zote ni kuonesha kwamba, binadamu ana *lineage* yake, binadamu hajawahi kuwa sokwe, hajawahi kuwa sokwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo dhana zitaondolewa kama tuna *active department* ya mambo ya kale, ingeweza kuwa inazungumza mambo ya namna hii. Ninaomba sana hili eneo la mambo ya kale lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale kwangu Iringa ninamshukuru Waziri ameendeleza baadhi ya maeneo ambayo ni ya kihistoria na mambo ya kale ameweka fedha. Ninamshukuru kuna maeneo

kwa mfano Mtaa wa Legezamwendo - Kitanzini wamefanya jambo. Ninaomba waendelee kufanya jambo kubwa zaidi kwa kuliendeleza na kulitangaza pamoja na Jiwe la Gangilonga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe maeneo mengine pia wayape kipaumbele. Kwa mfano, tuna michoro kule Igeleke, Mtwivila, tuna Mapango ya Igumbilo, tuna *pillars* zile za Msisina kule Nduli, tuna maeneo mengine mengi katika Manispaa yetu ya Iringa, yako katika kata mbalimbali ambayo ni ya vivutio vya utalii. Tunaomba viendelee kutangazwa na kuwekwa katika vyombo vya utalii ili viweze kujulikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe pia Wizara ya Utalii, kuna hii dhana (ilikuwa ni mchango tu); ninafikiri utalii unatupatia faida nyingi, lakini tungeweza kuongeza faida zaidi kwa hawa watalii. Mtalii anapokuja nchini kwetu tuongeze faida zaidi, wako *professionals* ambao tunaweza tukatumia taaluma zao wakija nchini tukazitumia hizo taaluma zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshapata changamoto ya kupata wanataaluma wamekuja hapa kama watalii, tumeomba tuwatumie, lakini wakazuiwa kwa sababu hawana vibali au vibali vyao havijielezi pale. Ninafikiri tungewapa *platform*, tutengeneze utaratibu mzuri wa kuruhusu hawa watalii wanapokuja pia wakiwa wataalamu wana mchango wao, tuwape *platform* za kutoa mawazo yao na kuchangia katika nchi yetu na hasa eneo la utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi na ninaunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fabian Ngajilo, ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Japhael Masanja, Mheshimiwa Kijakazi Yunus Mohamed na Mheshimiwa Margaret Simwanza wajiandae.

**MHE. JAPHAEL M. LUFUNGIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi. Awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kunipa kibali pia siku ya leo kuweza kuchangia hotuba ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutangaza *Royal Tour* na kuwa mtalii namba moja nchini. Pia, niwashukuru na kuwapongeza Waziri na Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu ninataka ujikite kwenye masuala ya uhifadhi. Suala la kwanza la uhifadhi ni suala muhimu ni suala linalohitaji kupewa kipaumbele sana. Uhifadhi tunatunza rasilimali zetu, lakini uhifadhi unachochea vitu vingi hasa ukuzaji wa uchumi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuishukuru Serikali kwa kufanya maamuzi mazuri mwaka 2022 na 2023 kupitia Baraza la Mawaziri kwa kukubali vijiji 22 kuendelea kuishi katika eneo la *Igombe River* lililokuwa chini ya *TFS* ambako sasa mgogoro uliokuwepo kwa muda mrefu wa ndani ya Jimbo la Ulyankulu umekwisha kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niweke maombi machache kwenye eneo la vijiji kadhaa na kata kadhaa. Wakati Baraza la Mawaziri linafanya uamuzi wa kuruhusu wananchi wakae kwenye eneo hilo, yako maeneo yalibaki, yaliachwa nje kama kwenye Kata ya Mwongozo. Kipo Kijiji cha Mwanduti ambacho kuna mgogoro mdogo wa wananchi pale katika Kitongoji cha Kipendamoyo Mashariki, eneo hilo liliachwa nje na bado wananchi pale wanalalamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Wizara iweze kuona namna kwa kushirikiana na Wizara zote kuhakikisha kwamba, eneo hilo dogo la kilometa kadhaa liweze kufanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kata ya Nhwande vipo vitongoji viwili viliachwa nje vina mgogoro mkubwa ambavyo ni Kitongoji cha Kabanga, Kasandalala pamoja na Isozi. Kijiji hicho kilibaki na Vitongoji viwili ambavyo ni vizima kwa maana ya Ntwigu, Kalama pamoja na Didia ambayo ilimegwa upande.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kijiji cha Asasu kipo Kitongoji cha Ibilingo ambacho mara nyingi kilikuwa kinafanya uchaguzi na wananchi pale walijenga pakawepo na shule, lakini wakati wanafanya marekebisho kitongoji cha Ibilingo kiliachwa nje. Niiombe Serikali yangu, Serikali pendwa ifanye marekebisho madogo hapo ili kuendelea kuondoa migogoro isiyo ya lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kata ya Ilege kipo kitongoji na eneo la Mtakuja ambalo liliachwa nje. Wananchi wameishi pale zaidi ya miaka 30, lakini wakati wanafanya marekebisho katika vile vitongoji, maeneo hayo yaliachwa nje. Niiombe Serikali yangu pendwa iweze kufanya marekebisho ili waendelee na maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo tunao mgogoro mkubwa ambao kwa *level* ya mkoa na wilaya tuliushindwa, marekebisho ya mgogoro wa mpaka baina ya Wilaya ya Kaliua na Wilaya ya Kahama kwenye Halmashauri ya Ushetu. Mpaka huo umeleta mgogoro kwa muda mrefu na mgogoro huo tuliuleta Wizarani kwa maana unatatuliwa ngazi ya Wizara. Tuiombe Serikali iweze kuutatua mgogoro huo ili kuhakikisha kwamba Wilaya ya Kahama pamoja na Kaliua tunamaliza tatizo ambalo liko upande wa Msitu wa Kigosi, Muyowosi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijikite kwenye eneo la wilaya kwa ujumla. Wilaya ya Kaliua ina kilometa za mraba 14,050, lakini eneo linalofanya shughuli za kibinadamu ni 11% tu, 89% sawa na *square meter* za mraba 12,504.50, ni eneo la msitu na mapori yaliyohifadhiwa. Eneo linalotumika kwa shughuli zote za kilimo na ufugaji ni *square meter* za mraba 1,545, lakini idadi ya watu tulionao kwa sensa ya mwisho iliyofanyika, wakaaji wa Wilaya ya Kaliua wapo 753,998. Pia, tuna idadi ya mifugo 564,836 hapo tunawazungumzia ng'ombe, lakini wako mbuzi na kondoo. Mahitaji yao eneo wanalolisha tunazo ekari 182,000 tu zinazotumika kwa ajili ya malisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwa hesabu za kitaalamu kwamba eneo la ng'ombe mmoja anahitaji kutumia eneo la hekta 2.5. Kwa hiyo, uhitaji wa malisho tu peke yake ni ekari 1,412. Kwa hiyo, tuone namna ambavyo Wilaya ya Kaliua

imebanwa. Si hivyo tu, eneo la Kaliua tuna vijiji na limebanwa kwenye maeneo yote. Tuna Kata za Ukumbi Siganga, Zugi Mlole na maeneo mengine yote yamebanwa na uhifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Tabora kwa historia ni mkoa wa nyuki, ulikuwa unafanya shughuli za nyuki, lakini pia ni mkoa ambao ulikuwa na shughuli za uvunaji wa mazao ya misitu. Kwa sasa baada ya mabadiliko ambayo yalifanyika hapo katikati, yalifanyika bila kuwashirikisha wananchi. Jambo hili limesababisha mgogoro mkubwa sana kwa wananchi wetu na limesababisha kuichonganisha Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali yangu kwamba mchakato huu wa uanzishwaji wa mapori ufuate taratibu za kisheria kwamba utangazwe, wananchi na wadau wengine waweze kushirikishwa, lakini yako mapori ambayo yalianzishwa, Mapori ya Luganzo – Tongwe ambayo yalichukua Misitu ya *Mpanda Line*, lakini pia Tongwe Magharibi kwa maana ya Katavi, Msato na Uvinza. Maeneo haya yanaleta changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hivyo tu, nimekuwa Mwenyekiti wa Halmashauri mwaka 2023, Hayati Lukuvi akiwa Waziri wa Nyumba na Maendeleo ya Makazi alikuja wilayani Kaliua na alifanya mikutano katika Kata ya Ukumbi Siganga, akawaeleza kwamba mama yetu mpendwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameruhusu vijiji kuendelea kuishi vikiwemo Vijiji vya Usinga pamoja na Kakonko. Wananchi walishangilia na wakaelezwa kwamba, eneo hilo litawekewa mipaka na bado wananchi waendelee na maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huo huo 2023 akiwa Waziri wa Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ndugu yangu Mheshimiwa Jerry Silaa alikuja tena, alirudi akasema eneo hilo limefutwa, wananchi wa eneo hilo wajiandae, wataondoka katika maeneo hayo. Kwa hiyo, ndani ya mwaka mmoja kukawa na kauli mbili zinazowachanganya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali kwamba, eneo hilo wananchi wengi wamekaa, lakini ndiyo eneo pekee linalozalisha mazao mengi katika Wilaya ya Kaliua zaidi ya mabehewa 50 ya

mazao yanayotoka kwa mwezi. Kwa hiyo, Kaliua haina mahali pa kupumulia. Niiombe Serikali kwamba ione namna ya kulirejea zoezi hili ili ikiwezekana mapori yaliyokuwa chini ya *TFS* yabadilishwe yaende *TAWA* na yaliyokuwa ya *TAWA,* yarudi *TAWA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajiuliza uzalishaji wa *TANAPA* aliyeko huko, mimi ninaamini kwanza huwezi kumtalii simba kwenye msitu mnene. Msitu wetu wa Kaliua ni msitu mnene wenye vichaka vingi lakini na nyasi ndefu. Niiombe Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan iweze kuona namna ambavyo inaweza ikaifanya Kaliua na yenyewe iweze kupumua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Japhael Masanja, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Kijakazi Yunus Mohamed, Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta na Mheshimiwa Pascal Lucas Lutandula wajiandae.

**MHE. JAPHAEL M. LUFUNGIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. KIJAKAZI Y. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye bajeti ya Wizara hii muhimu sana hususan katika pato la Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa sana ambayo ameifanya kuhakikisha kwamba utalii wa Tanzania unaendelea kukua ambapo unaendelea kuongeza pato la Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi hapa wamezungumza kuhusiana na filamu ya *Royal Tour* na niungane nao kumpongeza Mheshimiwa Rais kwenye hili. Tumeona tija yake kubwa ambapo tunafahamu wakati Mheshimiwa Rais anaingia alikuta watalii ambao wanatembelea Tanzania takribani watalii 900,000, lakini leo tunapozungumza tunao watalii wa nje zaidi ya 2,200,000. Hii ni

hatua kubwa sana na hao ni watalii wa nje, lakini ukijumlisha pamoja na watalii wa ndani tunao zaidi ya watalii 5,000,000 ambao wanatembelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunafahamu kwamba hapo nyuma sisi Watanzania ilikuwa siyo utamaduni wetu kutembelea vivutio vya utalii. Tulikuwa tukiamini utalii ni kwa ajili ya watalii ambao wanatoka nje ya Tanzania. Ni hatua kubwa sana ambayo tumeipiga na hii ni jitihada kubwa za Mheshimiwa Rais mwenyewe, lakini kwa kushirikiana na watendaji wake hususan watendaji wa Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Rais anaingia tulikuwa tunapata mapato takriban dola milioni 1.3 sawa na *almost* shilingi trilioni 2.5. Leo tunapozungumza tunapata zaidi ya dola bilioni 4.4 sawa na takriban shilingi 11,000,000,000,000. Kubwa zaidi tuna vijana wetu wa Kitanzania zaidi ya 3,000,000 ambao wanaendelea kupata ajira kutokana tu na utalii. Hii yote ni kutokana na kazi kubwa ambayo Mheshimiwa Rais ameifanya ya filamu ya *Royal Tour Season One*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo ninaomba nichukue nafasi hii kuipongeza sana Wizara kuanzia Mheshimiwa Waziri, dada yangu Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji kwa muda mfupi ambao amekuwepo kwenye Wizara hii, tunaona tija yake, tunaona kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya. Pia, kaka yangu Dkt. Abbas, Katibu Mkuu ambaye amehudumu Wizara hii zaidi ya miaka mitatu sasa, kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya na yeye tumpongeze zaidi kwa sababu tutakumbuka wakati filamu ya *Royal Tour,* yeye ndiye alikuwa mratibu wa filamu ile. Kazi ile kubwa ambayo imefanyika ni jitihada za Mheshimiwa Rais, lakini yeye kwenye kuratibu jambo lile alifanya kazi kubwa; tuendelee kumpongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika eneo hili tulipata taarifa kwamba itakuwepo filamu ya *Royal Tour Season Two*. Ningetamani sana Mheshimiwa Waziri wakati anakuja ku-*wind up* atueleze filamu hii itaanza lini. Kwa sababu kama tumepata tija kubwa kwa kiasi hiki kwenye filamu ya *Royal Tour Season One,*

nina imani kwamba tutakapokuja kwenye filamu ya *Royal Tour Season Two,* basi matokeo yatakuwa makubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi changamoto nyingi ambazo tumekuwa tukizungumza hapa Bungeni katika maeneo tunayotoka tuna imani kwamba changamoto zitaendelea kupungua kwa ukubwa. Kwa hiyo ningetamani sana Mheshimiwa Waziri atuambie lini filamu hii itaanza kurekodiwa ili tujiandae.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili ningetamani kushauri. Tumeona sasa hivi tunapozungumza utalii hata ukimuuliza Mtanzania wa kawaida utalii, yeye kichwani kwake anafahamu utalii kwa Kanda ya Kaskazini, lakini Taifa la Tanzania tumebarikiwa. Tuna vivutio vya utalii kila kanda ya Tanzania, tena vivutio vya asili kabisa. Kwa hiyo ningeshauri, kwenye filamu ya *Royal Tour* itakayofuata, tunaomba Mheshimiwa Rais ajielekeze kwenye kanda nyinginezo kama vile Kanda ya Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukienda Kanda ya Kusini kuna vivutio vingi sana ambavyo tukiendelea kuvitangaza tutaongeza idadi kubwa ya watalii Tanzania. Ninatamani kutoa ushuhuda tu wa filamu ya *Royal Tour Season One*. Mimi ni mmoja kati ya Watanzania ambao wanapenda kusafiri katika maeneo mbalimbali. Nimewahi kukutana na watalii wazungu kundi la watalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipowauliza walifahamu vipi kuhusu Tanzania, waliniambia walifahamu kupitia filamu ya *Royal Tour*. Kwa hiyo tunaona umuhimu mkubwa. Kwa hiyo, ningetamani tuweke msukumo wa kuleta filamu ya *Royal Tour Season Two* ili tuendelee kuona mafanikio makubwa ambayo yataendelea kupatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nikiongelea utalii wa Kusini ninafahamu kwamba Wizara imeendelea na jitihada za kuhakikisha kwamba wanaenda kuvitangaza vituo vya utalii na wameweka jitihada. Tumeona ukienda Hifadhi ya Ruaha pale, ukienda Hifadhi ya Nyerere wameweka viwanja vya ndege vipya. Nina imani kwamba tija itaendelea kupatikana kwa kuwekwa viwanja hivi vya ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kule kwetu Kilwa Kisiwani kuna watalii ambao wanakuja pale kwa kutumia boti, lakini inatumika boti ndogo. Ningeomba sasa Wizara watuwekee gati kubwa ambalo litaweza kupokea meli kubwa ili tuendelee kupata watalii wengi zaidi pale Kilwa Kisiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kule Kilwa Kipatimu kila mtu hapa anafahamu kuhusiana na Vita vya Maji Maji. Leo ukizungumza Vita vya Maji Maji wengi wanafahamu kule vita vilipoishia Songea, lakini vita hivi vilianzia kwetu Kilwa Kipatimu pale ambapo kwa muda mrefu tumekuwa tuki-*struggle* Watanzania wafahamu kuhusiana na pale vita vilipoanzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana hapa tulitaka kufanya maadhimisho mwezi Agosti, lakini tulishindwa hatukufanikiwa. Sasa niombe Wizara mwaka huu tuko kwenye mipango ya kuhakikisha kwamba tunakuwa na maadhimisho ya Vita vya Maji Maji Kilwa Kipatimu. Niombe Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na Wizara kwa ujumla twende wakatuunge mkono ili tuweze kufanikisha maadhimisho ya Vita vya Maji Maji tuendelee kutangaza vivutio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale ukienda Kipatimu utakuta yako pale katika Mapango ambapo wakati wa Vita vya Maji Maji akina mama walikuwa wanaficha watoto wao kwenye yale mapango pale. Ni sehemu nzuri ya vivutio vya utalii, ambavyo tukivitangaza tutaendelea kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Lindi na Kusini kwa ujumla ukienda Mtwara tuna *beach* safi kabisa. Leo hii unaenda Lindi, huna hoteli ya kufikia, unaenda Mtwara wageni wetu wanakosa pa kufikia kwa sababu hakuna hoteli, lakini tuna *beach plots* nzuri ambazo tunaweza tukajenga hoteli pale tukaendelea kuongeza idadi ya wageni ambao wataendelea kutupatia mapato katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na tija kubwa inayotokana na utalii tunazo changamoto. Moja ya changamoto kubwa ambayo tunakabiliana nayo, wengi wameeleza hapa changamoto ya tembo kule kwetu tunaita ndovu na ningependa nitumie jina ndovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukienda Mkoa mzima wa Lindi utakuta tunakabiliana na changamoto ya ndovu. Nami binafsi ninatambua sana umuhimu wa ndovu, ninatambua tija yake kwenye kutuletea mapato kwenye Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, tunafahamu kwamba, hakuna kitu muhimu kama uhai wa wananchi wetu. Kwa hiyo, ninaomba sana twende tukaone namna ya kukabiliana na changamoto hii ya ndovu, kwa sababu watu wengi wanapoteza maisha, watu wanajeruhiwa, lakini mali zinapotea, kwa maana ya mashamba ambayo ndovu hawa wamekuwa wakiathiri mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapo hapo tunafahamu kwamba, Wizara au Serikali imekuwa ikitoa fidia ya kifuta jasho na kifuta machozi, lakini kuanzia mwaka 2023, wapo watu zaidi ya 3,000 wanaodai katika Mkoa wa Lindi, mpaka leo bado hawajalipwa. Mara ya mwisho malipo yalitoka mwaka 2024 na malipo yale yalikuwa kwa wale wanaodai kifuta jasho cha miaka ya nyuma, lakini mpaka leo bado hawajalipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua sana jitihada za Serikali. Tumeletewa ndege nyuki sita kutokana na ahadi ya Mheshimiwa Rais, ambayo aliahidi wakati wa kampeni alipokuja Lindi, lakini ndege nyuki sita hazitoshi, tungetamani tuendelee kuongezewa nguvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais pia alituahidi kutuletea Maafisa Wanyamapori, kwa maana ya kuandaa vijana katika maeneo husika ambao watakwenda kusaidia Maafisa Wanyamapori. Tunao takribani vijana 30, lakini bado hawajapatiwa mikataba, kwa hiyo, bado tija yao haionekani. Ingawa pia, hawatoshi tungetamani tuendelee kuongezewa vijana wengine, ambao watakwenda kuongeza tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana Serikali, ninajua zipo jitihada mbalimbali za kudhibiti tembo, tumeona kwenye baadhi ya maeneo zimejengwa *electric fence,* tunaona njia ya asili ya kutumia pilipili, ambazo zinafanyika huko kwetu na nyinginezo, lakini bado njia hizi hazijaleta tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningetamani Wizara iendelee kufanya tafiti, kwa sababu tembo hawapo Tanzania pekee yake. Nchi mbalimbali wapo ndovu. Wajue wenzetu wanafanyaje ili twende tukakabiliane na changamoto hii ambayo akina mama wanashindwa kwenda mashambani na kwenda kuchota maji alfajiri, kwa sababu wanakwenda kukutana na ndovu na kuathiri maisha yao. Ninaomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa atuambie mipango ya Serikali kuhakikisha kwamba inaendelea kufanya tafiti za kuzuia ndovu kuathiri wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitembelea Kata moja ya Rutamba kwenye jimbo la mama yangu Mheshimiwa Mama Salma Kikwete. Niliwekewa maji ninywe yako kwenye jagi. Nikauliza hiki ni nini, baada ya kukaribishwa chakula, kwa sababu Rutamba ndipo kijijini ninapotoka. Baada ya kula ninapewa maji, nikauliza haya maji ya togwa, nikaambiwa haya ni maji na hii ndiyo athari ya ndovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndovu wamekwenda kwenye vyanzo vya maji, wanaenda kutifuatifua maji, kiasi kwamba maji yanatoka bombani ukiyakinga, ukiyatazama yale maji yaani unaweza kuelewa ni nini ambacho tunazungumza. Kwa hiyo, changamoto ni kubwa wanaharibu mashamba sawa, lakini mpaka kwenye vyanzo vya maji wananchi wetu wanashindwa kunywa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuhitimisha, inawezekana Mheshimiwa Waziri haelewi, japo ninajua anaelewa, lakini ili apate picha halisi ninayozungumza ningetamani baada ya Bunge hili, twende akatembelee aone tunapozungumza athari za ndovu tunazungumza kitu gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi na niendelee kuipongeza Wizara, wanafanya kazi nzuri, niwatie moyo, ingawa changamoto ni nyingi, lakini tuendelee kupambana nazo. Ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kijakazi Yunus Mohamed. Waheshimiwa Wabunge, pengine tukiwaita ndovu

kwa jina hilo wanaweza wakaacha kuja kutuvamia kwenye makazi yetu. Ninafikiri ni neno zuri zaidi pengine ninavyofikiria. Kwa hiyo, tukiita ndovu basi inawezekana ikawa tija kwetu.

Tunaendelea na Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta na Mheshimiwa Pascal Lucas Lutandula ajiandae.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nichangie hoja iliyoko mezani. Kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai. Pili, ninawashukuru sana wananchi wa Urambo kwa kunipa ushirikiano. Zaidi ya yote ninamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa aliyofanya ya kutangaza utalii wa nchi yetu kwa kupitia *Royal Tour*. Mwenyezi Mungu ambariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru sana wafanyakazi wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii, kuanzia Mheshimiwa Waziri mwenyewe, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote, Makamishna kwa kazi kubwa wanayofanya, Mwenyezi Mungu awape nguvu zaidi ya kufanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru Wizara kama nilivyosema hapo awali, kwa kutambua kwamba wananchi wa Urambo nao wanategemea asali kama zao lao la kiuchumi. Ninawashukuru zaidi kwa kutambua hivyo, wametusaidia kutupa kiwanda cha kuchenjua asali, kwa hiyo, karibu na sisi tutaanza kuuza asali ya Urambo, Mwenyezi Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa pamoja na kuwashukuru, ninaomba tu niwakumbushe kwamba, ili tupate asali nyingi zaidi ya kuweza kusafirisha mpaka nje, tunahitaji eneo la kufugia. Maana yake ni kwamba, tunahitaji mizinga zaidi, tunahitaji eneo la kuweka mizinga mingi zaidi, ili tuweze kupata asali nyingi ya kuweza kuchanjua katika kiwanda ambacho Mwenyezi Mungu ametusaidia kupata kwa kupitia kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninarudia ombi langu, kwa niaba ya wananchi wa Urambo kwamba, nimeshafika

mpaka kwenye vikao vya Kamati husika. Wizara ninaamini kabisa inatambua chini ya Mawaziri mbalimbali waliopita huko, kwamba bado tunaomba elimu kwa wananchi wale ambao eneo lao lilichukuliwa likaingizwa katika Msitu wa Hifadhi wa Mto Ugalla. Bado wanahitaji elimu, kwamba tunataka ushirikiano nao kwa aina gani na wao watanufaika vipi msitu wa uhifadhi ukiendelea kudumu kwa ajili ya vizazi vya sasa na vijavyo. Kwa hiyo, bado tunaomba elimu kwa wananchi ili wajue kusudio la Serikali na wao watanufaika vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika Wilaya ya Urambo au Jimbo la Urambo tuna kata nne, ambazo ni Ukondamoyo, Nsenda, Kasisi na Ugala, ambao wote wanahusika katika maeneo ambayo yamechangia katika kupata Hifadhi ya Msitu wa Mto Ugalla. Wao wote wangependa kushiriki kama nilivyosema kupewa elimu, lakini zaidi ya hayo nao wana changamoto kama nilivyosikia kwa Waheshimiwa Wabunge waliotangulia kuongea na sisi tuna wanyama wakali; simba na tembo, sisi tumezoea kusema tembo, ambao pia wanatuathiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakumbuka wakati fulani nikiwa Urambo tulikwenda kukagua maeneo ambayo wananchi wa Kata ya Nsenda, waliona miguu ya simba na kweli baadaye tukafuatilia nami mwenyewe, tukakuta walishambulia ng'ombe. Kwa hiyo, tunachoomba sasa, kwa kuwa tunathamini msitu huo, lakini pia tunathamini maisha ya binadamu, tunaomba katika maeneo manne ambayo wanyama ni wengi wawekewe kambi, ili wanyama wanaposhambulia binadamu au mifugo, wao waende kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tungeomba sasa, kuna eneo Utenge, Horongo, Lunyeta wao tungeomba katikati ya hizi kata za Izengabatogilwe, katika maeneo haya niliyotaja manne kuwe na kambi ambayo itasaidia kuwalinda hasa wanapopata kuvamiwa na wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itawasaidia sana pale ambako ataona Serikali yao pendwa inawajali wao pia, inawajali wanyama, lakini inawajali wao ili tupate huduma kwa haraka

pale wanyama wanapotushambulia. Kwa hiyo, tunaomba sana kambi ya maaskari husika wawepo pale watusaidie kulinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwamba sisi Urambo kama walivyo wenzetu, majirani zetu Kaliua tunapata watalii, lakini sisi kwa upande wa Urambo hatuna lango la kuingilia watalii. Kwa heshima na taadhima, tunamwomba Mheshimiwa Waziri na wahusika wote katika wizara hiyo, watusaidie na sisi Urambo tupate lango la kuingilia watalii. Kuna wakati tulipata matumaini mpaka tukajenga nyumba ile ambayo watakuwa wanapitia watalii wanapokwenda porini kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, bahati mbaya nyumba hiyo imekaa, mwisho tumeruhusu wafanyakazi katika idara zingine wakae, baada ya kuona bado sisi kama Urambo hatujapata lango la kuingilia watalii kwetu. Kwa hiyo, ninaomba sana kwa heshima na taadhima watuletee lango ili na sisi tupate watalii, tuingize fedha kwa ajili ya kuendeleza maisha yetu Wanaurambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo niliona ni la msingi sana, ni matangazo, nami ni mmojawapo wa watu wanaopenda sana kuangalia ligi zote; La Liga, *Premier League* zote ninaangalia na ukiniambia mashindano ya jana matokeo nitakuambia tu *Manchester* walipata nini na washindani wao walipata nini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachoniumiza moyo wangu mimi, sioni *Visit* Tanzania ya kiuhakika. Roho inaniuma sitaki kutaja nchi za wenzetu, unakuta timu kama Arsenal, wanavaa mikanda *visit*, mimi sitaki kutaja nchi za watu. Sasa kwa nini na sisi hatuna timu kubwa ya Manchester City huko na Barcelona wakavaa huku mikanda ambayo inaonyesha *visit* Tanzania au *visit* Serengeti. Serengeti kama tulivyosikia na mbuga zingine za wanyama zinaongoza duniani. Kwa nini, hatuoni *visit* Serengeti kwenye timu kubwa kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tusisahau Barcelona Waziri, wakawaombe huko na *Manchester United* na wengineo. Wavae mikanda ambayo inasema *visit* Serengeti, *visit*

Ngorongoro, *visit* Manyara ambako simba wanapanda kwenye miti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, yangu yalikuwa ni hayo, lakini nirudie tena kuwashukuru sana Wizara husika, kwamba Urambo na sisi tunahitaji elimu, tunahitaji maeneo ya kuweka mizinga na tunahitaji lango kama nilivyosema la watalii kuingia. Zaidi ya yote tujenge mahusiano na wananchi kwa kuja kuwapa elimu; kile wanachokifanya kina manufaa gani kwa, na kina manufaa gani kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta. Nilimtaja Mheshimiwa Pascal Lucas Lutandula.

**MHE. PASCAL L. LUTANDULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nikushukuru sana kwa kunipa kibali hiki nami niwe mchangiaji katika Wizara hii ya Maliasili na Utalii. Nianze kwa kuwashukuru sana wananchi wangu wa Chato Kusini, kwa namna ambavyo wameendelea kunipa ushirikiano. Nimshukuru sana Waziri wa Maliasili na Utalii pamoja na Naibu wake, kwa kweli, watu hawa wanafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwangu Jimbo la Chato Kusini wamenijengea zahanati mbili, wamenijengea shule moja zaidi ya madarasa saba pamoja na vyoo vyake. Kwa kweli, watu hawa Mungu wa Mbinguni awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwashukuru wao pamoja na wataalamu wao, nimshukuru sana Meneja wa Shamba la Silayo. Kule Chato Kusini tuna Shamba la Silayo kwenye hifadhi yetu ya *TFS*, watu hawa wamekuja na teknolojia mpya wanapanda miti. Kwa hiyo, tunaona mabadiliko yanayoenda kuleta tija kwenye Jimbo langu la Chato Kusini. Baada ya muda kidogo wananchi wangu wataanza kuona matunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Meneja huyu Juma Mwita, sijui kama Wakurya wote kama akina Mheshimiwa Getere wapo kama huyu mtu, ni mtu mwema anafanya kazi nzuri, kwa kweli ninampongeza sana mhifadhi huyu, pamoja na watumishi wake wanaokaa kwenye ofisi yake. Wananipa ushirikiano mimi kama Mbunge pamoja na wananchi wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto yangu sasa, ninaomba Mheshimiwa Waziri, dada yangu. sasa atulie vizuri anisikilize, ninaleta hoja ya wananchi wangu wema wa Chato Kusini. Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan alipokuja Chato, mimi Mbunge wao nikiwa ninaomba kura na yeye akiomba kura, mimi mtoto wa mama ntilie nilisimama nikamwambia, kwamba wananchi wangu wa Bwanga, wa Buziku, kule Nyalutefya kule Ipembe la Ng'ombe, Mchangani kule Matabe wana changamoto ya maeneo ya kufugia na kulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais aliposimama alinijibu vizuri na wananchi wangu wakawa na imani nami, ndiyo maana wakanipa kura. Akasema baada ya kuteua tu Baraza la Mawaziri atatuma ile Tume ya Mawaziri Nane, waje wapitie hii mipaka ili wahakikishe hii migogoro yote ya wakulima na wafugaji na alinihakikishia haitakuwepo tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimesubiri zile siku 100, kwamba hawa Mawaziri labda hawajakumbuka au wamesahau. Sasa ninashindwa kujua wamesahau Mawaziri kwamba, Mheshimiwa Rais alisema baada ya kuwateua tu mje ili waainishe mipaka vizuri, wawape watu wangu wa kule Nyakayondo waliobanana zaidi ya wakazi laki mbili, hawana mahali pa kulima. Wamesahau kuja kuokoa tatizo hili la wananchi wangu? Mimi ninawakumbusha tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini inaniumiza moyo kuwa nina watu hawana mahali pa kulima, lakini Mungu amewapa eneo zuri kule. Ninawaomba sana ndugu zangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, tuliomba eneo la Matabe, hekta zaidi ya 2,860. Watu wa shamba na watu wa *TFS* wamesharidhia kutupa eneo hilo. Nimwombe Mheshimiwa Waziri

anapokuja kuhitimisha leo hotuba yake hapa, limebaki tangazo la Serikali, hili nalo ni la kuchukua maelezo muda mrefu? Ninaomba Waziri anisaidie kuwaambia sasa, kwamba wametangaza leo, sisi kule Matabe kimekuwa kijiji na tuendelee kulima na kufuga, hili nalo linachukua muda? Kama hawa watu wa shamba wameshakubali, nimwombe sana Mheshimiwa dada yangu, ninampigia magoti, ninaomba leo akija hapa awaambie wananchi wangu wa Matabe ili mioyo yao ipone.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa la mwisho kwa sababu ya muda, ninadhani linaweza likawa la mwisho. Mimi kwa kweli, Waheshimiwa Wabunge sina changamoto na watu wa utalii, neno linaloitwa utalii sina changamoto nalo. Ombi langu wapunguze safari za kwenda nje kutangaza, wanatumia fedha za Serikali ovyo, utangazaji huu si umeshakuwa ni wa kwenye mtandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa fedha 2022/2023 walichukua bilioni nane za Serikali, wote wameenda nazo safari, 2024/2025, wamechukua bilioni 15 zote wanasafiri tu. Kweli Waheshimiwa Wabunge tutakuwa tunapitisha hela za watu kusafiri? Watangaze kidijiti, dunia imebadilika, dunia iko kwenye kiganja, Bodi ya Utalii kama hakuna watu wenye uwezo mimi mtoto wa mama nitilie nipo. *(Makofi)*

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nilitaka tu kumpa taarifa mchangiaji kwamba, ili upate hela unahitaji kuitumia hela. Kidijiti tuna uwezo wa kutangaza, lakini hatuna uwezo, pia wenzetu wa mataifa mengine wanakwenda huko na wanafanya makongamano makubwa. Kwa hiyo, tuendelee kuamini kwamba *CAG* yupo na kama kuna ubadhirifu wowote, basi atauona. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa unaipokea taarifa hiyo ya Mheshimiwa Asia.

**MHE. PASCAL L. LUTANDULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea kwa mikono miwili. Huyu ni MNEC, nami ni mtu mdogo sana kwake. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni kupunguza gharama za safari. Nimepokea taarifa yake nadhani ujumbe umefika. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda nieleze la mwisho, mimi kwenye utalii sina shida. Shida yangu sasa kwenye Serikali ni kwenye maliasili, niulize tu, humu kwenye hifadhi, kwa mfano mimi ninatoka kule Kigosi, hizi nyasi zinaoteshwa na Mungu kila mwaka, Mungu anawaletea maji, wanatunzwa mpaka wanakauka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Biblia inasema watu wangu wanaangamia kwa kukosa maarifa, haya ni maarifa mabovu. Haiwezekani Mungu akaotesha nyasi, tukazuia ng'ombe hawa wa watoto wa maskini kwenda kuchunga wale ng'ombe wale na kunenepa. Tukawasubiri tena Mungu akawaambia kaukeni nyasi. Haya ni matumizi kweli? mpaka Mungu ninadhani huwa anatushangaa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri, watengeneze mpango wa kuwasaidia wafugaji, siyo kuwafanya wafugaji wa Tanzania kuwa maskini. Nami ushauri wangu kwa Wabunge, ninaomba wanielewe, hili tatizo ili tulimalize wasipige kelele humu ndani. Nimemsikia Mbunge wa Serengeti na ndugu zangu wote wa Bunda wanalalamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuja na suluhisho, hii Wizara ya Maliasili na Utalii, Utalii ujitegemee na Maliasili nayo ijitegemee. Nikiwa na maana gani, maliasili na uvuvi na mifugo ziunganishwe, ili lile fungu la Biblia liungane, kwamba mtoto wako akikuomba mkate unampa jiwe? Kama wakiunganishwa kwenye mifugo hapa hawa watu watatupa nyasi sisi wafugaji tutafugia ng'ombe zetu kwenye yale mapori. Kwa sababu, ng'ombe hawezi kukata

mti, ng'ombe hawezi kupambana na simba, sisi tutawalinda hata hao wanyama, kuliko watu wanaoingia na kukata miti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaokata miti ndiyo wanaharibu. Sisi ng'ombe wanaenda kula nyasi tu. Kwa hiyo, nimwombe sana, mimi hili ndilo suluhisho langu, kama awamu hii ni kwa sababu ninawashauri hawatalipokea, awamu ijayo nitashikilia shilingi na wala sitaachia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Waheshimiwa Wabunge huyo ni mchangiaji wetu wa mwisho kwa mchana huu. Ninawashukuru wote kwa michango yenu na ushauri kwa Serikali.

Kabla hatujasitisha shughuli za Bunge, tuna wachangiaji wa mwanzo watakaoanza jioni. Tuna Mheshimiwa Nassriya Nassir Ali, Mheshimiwa Mgore Miraji Kigera, Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mheshimiwa Bakari Bakari Shingo na Mheshimiwa Rashid Mtima, wataanza wakati wa jioni.

Tuna tangazo la wageni ambao wapo ukumbini muda huu. Tuna wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji, Waziri wetu wa Maliasili, hao ni Wadau wa Sekta ya Utalii nchini. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Tunao wageni sita wa Mheshimiwa Fadhili Fabian Ngajilo. Hawa ni viongozi wa Chama cha Wawindaji kutoka Mkoa wa Iringa. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Tunao wageni ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, tuna wanafunzi 100 na walimu nane, kutoka Shule ya Awali na Msingi Canossa ya Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana wanafunzi wetu na wageni wetu wote ambao mmetutembelea katika Bunge letu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, ninawatakia mchana mwema na ninasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.59 mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Deodatus P. Mwanyika) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. MKUTA MASOLI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea na majadiliano ya hoja iliyo mbele yetu. Tutaanza na wachangiaji wafuatao; Mheshimiwa Nassriya Nassir Ali, atafuatiwa na Mheshimiwa Mgore Miraji Kigera na Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga ajiandae. Ninadhani Mheshimiwa Nassriya yuko upande ule.

*(Hapa Mhe. Nassriya Nassir Ali alichangia kupitia mtaalamu wa lugha ya alama)*

**MHE. NASSRIYA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nishukuru kwa kupata nafasi hii ya kuchangia, lakini pia nimshukuru Mwenyezi Mungu na nimesimama tena mara nyingine kwa kuwa nimepata kibali cha kuweza kuchangia hapa. Kwanza nipongeze Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kazi kubwa ambayo wamekuwa wakiifanya ndani ya nchi hii. Wizara hii ni Wizara ambayo inachangia sana pato la Taifa, ninadhani inashindana na Wizara nyingi kubwa katika kuchangia pato la Taifa na mimi ni mdau wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kwanza kusema ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania kwa kuhakikisha kwamba anahamasisha utalii. Ndiyo maana aliweza kurekodi ile filamu fupi ya *Royal Tour*. Kwa maana hiyo watalii wengi wamekuja Tanzania kwa ajili hiyo. Kwa hiyo nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuunga mkono suala zima la utalii na maliasili hapa nchini kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu mimi mwenyewe nilishawahi kushiriki kwa ajili ya kuhamasisha utalii kwenye nchi za wenzetu. Niliwahi kwenda Urusi na baada ya hapo tulipata wageni wengi sana wenye ulemavu wakiwemo viziwi, walikuja Tanzania kwa ajili ya kufanya utalii. Kwa hiyo, niiombe sana Wizara hii; kwanza kabisa nimshukuru Dkt. Abbas ambaye ni Katibu Mkuu kwa kazi kubwa ambayo amekuwa akiifanya. Niseme wazi Dkt. Abbas ni mbunifu sana amekuwa akitumia muda mwingi sana kujaribu kufanya ubunifu katika kuikuza Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikishirikiana naye kwenye masuala mengi hata kabla, huko nyuma. Kiukweli anasaidia sana kukuza utamaduni wetu hapa nchini na kuweza kukuza utalii wetu hapa nchini. Niseme tu isingekuwa yeye kwa sisi watu wenye ulemavu ingekuwa ni changamoto kwa sababu ni mtu ambaye ni mwepesi sana kumfikia. Kwa hiyo, nimshukuru sana Dkt. Abbas kwa kazi kubwa na ngumu ambayo anaifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee pia angalau kuhusu Wizara yetu iweze kuandaa matamasha mbalimbali ya kitamaduni ambayo yanakuza utamaduni wetu na asili yetu na hii niombe sana Wizara iongezewe bajeti ili kufanya hivi kwa sababu tukifanya haya matamasha kwa maana hiyo tunaitangaza nchi yetu, tunatangaza tamaduni zetu na kuelimisha watu na watoto wetu kuweza kujua tamaduni zetu. Kwa hiyo, Wizara hii inahitaji pia kuwa na ubunifu katika masuala mbalimbali, tena ubunifu wa hali ya juu. Kwa sababu tukiweza kutangaza nchi yetu sisi kama Tanzania kwa maana hiyo tutaweza kukuza pato la Taifa. Hatuwezi kuliachia hili jambo Wizara peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nipo tayari, mimi ni balozi mzuri sana wa masuala ya utalii na Tanzania Mungu ametupa rasilimali za kutosha kuhusiana na masuala mazima ya utalii, tuna milima kadha wa kadha, tuna mbuga za wanyama, tuna mito,

tuna kila kitu ambacho kinaweza kutangaza utalii wetu. Kwa hiyo, niombe sana mabalozi ambao wako huko kwenye maeneo yao ya kazi kwenye nchi mbalimbali wasikae tu kufikiri kazi ni kuwakilisha tu Tanzania kule, watangaze utalii. Watangaze utalii wetu, watumie ubunifu kutangaza utalii wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ya Maliasili na Utamaduni pia ni Wizara ambayo tunahitaji kukuza tamaduni zetu kama ambavyo nimesema. Kwa mfano, Zanzibar kule kuna tamaduni mbalimbali ambazo zinavutia, Songea huko Wangoni wana ngoma zao nzuri tu tunaweza tukazihamasisha kukuza utamaduni wetu, watu wakatujua kwa tamaduni zetu. Pia, tunafahamu kwamba Wazungu wakiwa wanakuja kwenye nchi za wenzetu hizi au wanakuja kwenye nchi zetu kabla hawajafika wanakuwa tayari wameshafanya *research* kwamba hii nchi ina vitu gani vya kuvutia ili aweze kufika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama hatuna tamaduni za kuvutia au vitu vya kuwavutia watajifunza nini wakija huku? Lazima tuoneshe tunakula nini vyakula vyetu vya asili, tamaduni zetu ngoma zetu na kadhalika. Pia, kama ambavyo nimesema kuhusiana na suala zima la utalii niombe sana Wizara yetu iboreshe miundombinu ili iweze kuwa jumuishi, kwa nini? Kule Afrika Kusini Cape Town kuna mlima unaitwa *Table Mountain*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Table Mountain* kule tunaambiwa kwamba watu wenye ulemavu wana uwezo wa kufika kule, wanaweza kutumia *wheel chair* zao kufika kule, viziwi wanaweza kuwasiliana wakiwa kule. Kwa maana hiyo hata huku tunaweza kufanya hivyo kukuza utajiri wetu kwa sababu wapo watu wenye ulemavu ambao ni matajiri wanahitaji kufika huko kutembea, kuona namna ambavyo nchi mbalimbali zilivyo. Kwa hiyo, niombe sana tuweze kuboresha miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana na nimwombe Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, hili ni ombi ambalo linakuja kwa unyenyekevu mkubwa. Niombe sana kama ambavyo nimesema suala zima la matamasha; hili suala tulichukulie kwa umaanani, kwa sababu bila matamasha haya watu hawawezi kuelewa nini Tanzania tunafanya, tuna tamaduni

gani, tuna mambo gani ambayo ni ya kuvutia. Pia, niombe sana wasituchoke sisi, tupo kutangaza utalii katika maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa utayari wake na ninajua Mheshimiwa Rais anapenda sana masuala mazima ya utalii na amekuza sana utalii hapa nchini. Tusikae tu kudhani kwamba wageni watakuja hivi hivi lazima tujitangaze, tuongeze *promotion*. Tuongeze matangazo, tutafute watu ambao wanaweza ku-*influence* watu waweze kuja kutalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa, niombe sana kuunga mkono hoja. Mungu ibariki Tanzania, Mungu mbariki Mheshimiwa Rais wa Tanzania yetu. Mungu mbariki Mheshimiwa Spika wa Bunge letu wa Tanzania. Mungu wabariki Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Mawaziri wote wa Tanzania. Amina. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Nassriya Nassir Ali kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Mgore Miraji Kigera, atafuatiwa na Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga na Mheshimiwa Bakari Bakari Shingo ajiandae.

**MHE. MGORE M. KIGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza kabisa ninapenda kuipongeza Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia Waziri wetu Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii wakiwepo Wakurugenzi wa *TANAPA*, Ngorongoro na *TAWA* kwa kazi nzuri na kubwa wanazozifanya kwa kupitia mazingira ambayo ni magumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alifanya kazi kubwa sana ya kuhakikisha Wizara hii ya Utalii inaweza kukua na kupata watalii wengi hapa nchini. Kupitia filamu yake ya *Royal Tour* mapato yaliongezeka kwa kiasi kikubwa sana katika Wizara hii. Hata hivyo, ni jambo la kusikitisha sana watumishi wetu wa *TANAPA*, Ngorongoro na TAWA wamekuwa wakipitia changamoto kubwa sana hasa katika upatikanaji wa stahiki zao kutokana na pesa kuchelewa kuwafikia kwa wakati. Hii ni baada ya fedha za *TANAPA*, Ngorongoro na *TAWA* kuwa

zinakusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania na kuzirudisha kwenye hizi taasisi inachukua muda mrefu. Kwa hiyo, tunafikia hatua ya kuwakatisha tamaa hawa watu wakati Wizara hii ndiyo Wizara inayofanya vizuri katika *collection* zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mwaka uliopita wamekusanya takriban shilingi 500,000,000,000. Hivyo nimwombe Mheshimiwa Waziri akishirikiana na mamlaka husika waendelee kuishauri Serikali na ninaishauri Serikali *collection* ya maliasili ambapo ni *TANAPA*, Ngorongoro na TAWA wazifanye wenyewe na huku Serikalini lirudishwe gawio la 15% kama ambavyo ilielekezwa na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatokea Mkoa wa Mara, hivi karibuni tumepata changamoto kubwa sana, Mbuga ya wanyama Serengeti miundombinu yake imekuwa ni mibaya hairidhishi na watalii walipata changamoto kubwa sana. Tunategemea sekta ya utalii kukuza pato la nchi yetu, lakini miundombinu ni mibaya mibaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa *TANAPA* wakiwezeshwa wakaendelea na *collection* zao wenyewe wakawa wanatoa fedha kwa ajili ya kutengeneza *infrastructures* hizi, nadhani tutafikia hatua nzuri ya kuongeza watalii. Kama ilani yetu inavyoelekeza kwa Mkoa wa Mara watalii wa ndani wafikie 15,124 na watalii wa nje wafikie 126,138. Bila kuboresha miundombinu hili lengo halitoweza kutimia na tutakuwa tunamkwamisha Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANAPA* wana kampuni yao ambayo ni kampuni ya ujenzi, nadhani dhamira ya kufungua kampuni hiyo ilikuwa ni kupunguza kutumia wakandarasi ambao wana *charges* kubwa, lakini kampuni hiyo kutokana na kwamba *TANAPA* wanashindwa kuwa na pesa imeshindwa pia kufanya kazi ipasavyo. Hivyo barabara zinaharibika, viwanja vya ndege vinaharibika, lakini wanashindwa kuendelea kwa sababu hawana fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali ilizingatie hili; fedha za maliasili na utalii kwa hizi *institutes* wakusanye wenyewe na

warudishe lile gawio la 15% kwenye Serikali, kwa sababu bila kufanya hivyo changamoto hii haitokwisha na mwisho wa siku tunakwenda kupoteza hii sekta yetu ya utalii ambayo ndiyo tunu ya Taifa letu na tumekuwa tukipata tuzo nyingi sana kutokana na utalii nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichangie kwenye upande wa kuongeza *products* za *TANAPA*, *TANAPA* wana *products* tano. Niwaombe waongeze na *product* nyingine ya sita ya utalii wa fukwe. Watalii wanapokuja wakishapita wakapanda Mlima Kilimanjaro, wakaingia Serengeti kuona wanyama kinachofuata ni nini? Wanahitaji kubarizi kwenye fukwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Musoma mjini pale tuna fukwe nzuri na kuna *sunset* za maana sana. Niiombe Wizara ya Maliasili na Utalii wahakikishe wanaingiza hii *product* na utalii wa fukwe uweze kufanyika katika Ziwa Victoria. Watalii wakifika Musoma Mjini wakatalii wakapita wakatembea mpaka kwenda Nyatwari sasa hivi tembo wanavuka wanakunywa maji wakiangalia hicho kitu wanafurahi sana. Kwa hiyo, niiombe pia Wizara ya Maliasili na Utalii iweze kuongeza hii *product* na hili jambo liweze kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niendelee kuwasisitiza Wizara ya Maliasili na Utalii hapo nyuma kuna barabara ilikuwa inatoka Kigoma inaenda Mahale. Hiyo barabara haikuwahi kupitika toka uhuru, ilikuja kufunguliwa mwaka 2013 na watu wa *TANAPA* wenyewe na watalii wengi sana walianza kuelekea Mahale kwa ajili ya kwenda kufanya utalii wa *chimpanzee*. Kwa hiyo, niendelee kusisitiza na kuomba Wizara hii iangaliwe kwa jicho la tatu kwa sababu sisi ndiyo tunaoitegemea kwenye Taifa hili kwenye mapato ya ndani kwa kupitia watalii wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais ameonesha jitihada za dhati sana za kuhakikisha hii Wizara ya Maliasili na Utalii inakua na kufikia kukusanya *above 500,000,000,000,* hili jambo lilikuwa halijawahi kutokea. Ninaomba pia niendelee kumshauri Waziri wa Maliasili na Utalii na niishauri Serikali, watalii wanapokuja nchini wanahitaji kupata vivutio vingi hivyo sisi tuwe wa kwanza kuendelea kufanya *promotions* na *advertisements* ili watu waweze kujua Tanzania inafanya nini.

Maana tangu Mheshimiwa Rais amefanya *Royal Tour* hakuna kitu kingine ambacho Wizara iliguswa kufanya ili kuendelea kuchochea utalii katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuwapongeza na niombe Serikali ilizingatie hili la kuhakikisha Wizara ya Maliasili na Utalii inaendelea kufanya *collection* zake wenyewe na warudishe gawio Serikalini la 15% ili Wizara hii iendelee kukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mgore Kigera, ahsante sana kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga atafuatiwa na Mheshimiwa Bakari Bakari Shingo na Mheshimiwa Rashid Mtima ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipatia nafasi hii. Nianze kwa kuunga mkono hoja na nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote waliopo kwenye Wizara lakini pia niwapongeze viongozi wote wa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kazi nzuri ambazo kwa kweli wanaendelea kuzifanya na wamefanya. Tumeona nchi yetu sasa kwa mwaka jana imepata tuzo ya kuwa kwenye *Safari destination*, Tanzania imeongoza kwa kupata tuzo. Kwa kweli tunawapongeza sana. Hiyo inatokana na kazi kubwa ambayo wameifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hapo, tumeona Hifadhi ya Serengeti imeendelea kuongoza na imepata tuzo kuwa hifadhi bora duniani, kwa kweli hiyo ni kazi nzuri ambayo wameifanya, tunawapongeza sana. Pia, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa ubunifu wake kwa kuja na ile *Royal Tour* ambayo aliifanya ambayo imetu-*promote* sana duniani na imetusaidia sana kuleta watalii wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli mpaka sasa hivi tunajivunia pamoja na kwamba tunahitaji kuongeza zaidi lakini tunajivunia kwa hapa tulipofika ambapo kwa kweli kuna

mchango mkubwa sana wa filamu ile ya *Royal Tour*. Tunaona idadi ya watalii sasa imefika 5,955,361, haijawahi kutokea katika nchi yetu. Idadi kubwa kama hiyo haijawahi kufikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa cha kuvutia zaidi tunaona watalii wa ndani wameongezeka sana sasa hivi. Tumepata watalii wa ndani milioni 3,641,066 hao ni watalii wa ndani ina maana Watanzania sasa wamejua umuhimu wa kwenda kula maisha na kwenda kutembelea hifadhi zetu. Kwa kweli ninawapongeza sana, ni kazi kubwa ambayo ameifanya mpaka tumefikia hapo. Watalii wa nje tumepata milioni 2,294,495, si haba ni watalii wengi lakini tunahitaji kuongeza nguvu zaidi ili tupate watalii wengi zaidi na tuweze kupata mapato makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine, haijawahi kutokea kwenye nchi yetu, sasa kwenye mapato yatokanayo na utalii, tumepata dola bilioni 4.4. Kwa kweli hizi ni jitihada kubwa sana ambazo tumefikia na hizi ukiziweka kwenye *Tanzanian Shilings* tunapata zaidi ya 11,000,000,000,000 tumeweza kuzipata, kwa hiyo, hili ni jambo la kujipongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia utalii jinsi ulivyo na nchi zingine zinavyofanya kazi, kwa kweli Tanzania ni moja ya nchi yenye vivutio vingi vya asili. Hapo nyuma Tanzania ilikuwa ni nchi ya pili duniani kwa vivutio vizuri, japo hapo katikati tumetetereka kidogo kwenye uhifadhi. Tumeshuka kwenye nafasi ya pili, sasa sijui tuko nafasi ya ngapi kati ya saba au ya nane duniani, lakini tulikuwa tunashika nafasi ya pili. Sasa nchi zingine ambazo hazina hata vivutio vizuri sana zinafanya vizuri sana kwenye maeneo ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Ufaransa kwa mwaka jana wamepata watalii zaidi ya milioni 103, lakini wamefuatiwa na Spain wana milioni 93.8; Marekani wana milioni 73.4; Uturuki wana milioni 60.6; Italy wana milioni 57.7; Mexico wana milioni 45; *UK* wana milioni 41.8; Japani wana milioni 37.5; na Ujerumani wana milioni 37.5. Tutaona nchi hizi za wenzetu zinapata mapato makubwa sana kutokana na idadi kubwa ya utalii ambao unafanyika kule kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa na sisi tufike mahali katika vivutio tulivyo navyo, hatuwezi kusema kwamba tutaendelea kupata watalii wengi kama vivutio vitabaki kama vilivyo. Tunahitaji kuongeza thamani ya vivutio vyetu, kuongeza *value* vitu mbalimbali ambavyo vitaweza kuvutia watalii wengi zaidi kuweza kuja katika nchi yetu na kuweza kukaa muda mrefu na nchi yetu ikaweza kupata mapato makubwa yanayotokana na masuala ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya utalii ni sekta mtambuka, ni sekta ambayo inahitaji ushirikishwaji na ushirikiano wa sekta mbalimbali zichangie kwenye utalii. Kwa mfano, pamoja na nchi yetu kuwa na vivutio vingi vya utalii, lakini tunahitaji kuongeza utalii wa fukwe. Nchi yetu imebahatika kuwa na fukwe nyingi, tuna bahari, maziwa na mito, ile lazima tuitumie kama rasilimali ya kuongeza. Sasa ili tuwavutie tutengeneze mazingira wezeshi kwenye fukwe zetu ili angalau sasa watu wengi wavutiwe kwenda ku-*enjoy* katika maeneo hayo ya fukwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tuna utaratibu, baadhi ya fukwe nyingi zinamilikiwa na watu binafsi, watu wanachukua. Ninafikiri tungeiga mfano wa nchi nyingine, maeneo ya fukwe lazima yatengwe mita kadhaa zibaki kuwa ni maeneo ya utalii wa ujumla, yasimilikiwe na mtu mmoja. Hiyo itasaidia sana katika kutengeneza na kuongeza kuvutia watalii mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuongeze utalii wa matibabu. Nchi yetu ninaipongeza sana, sasa hivi tumeboresha sana huduma za hospitali, tunaongeza ujenzi, kwa kweli si tu kwamba, tunatoa huduma za afya, lakini tunataka na watalii wanaokuja kupata matibabu nchini, waje hapa kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, utalii wa matibabu ni muhimu sana, ambao ni lazima tuendelee kushirikiana na Wizara nyingine, ili waongezeke, tupate hela nyingi sana. Tupate watalii kutoka nchi mbalimbali, labda watoke huko Zambia, Congo au sehemu nyingine, waje kwenye matibabu na wale wanaokuja nao sisi wote tunawahesabu kwamba, ni watalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuongeze pia utalii wa mikutano. Nchi yetu kwa jinsi tulivyo, tunahitaji kuongeza kumbi za kisasa za mikutano ya Kimataifa na hoteli za Kimataifa. Hoteli nyingi ziongezeke kujengwa, ili kuweza kuvutia watu mbalimbali kuja kufanya mikutano hapa. Wakija kufanya mikutano hapa, ndipo sisi tunawahesabu wote hao ni watalii, watatuletea fedha nyingi na nchi yetu itaweza kunufaika zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji utalii wa michezo. Ninafurahi na ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa jitihada zake mpaka Tanzania sasa tunakwenda ku-*host* mashindano ya michezo ya Afrika yale, kwa kweli ule ni utalii mkubwa. Sasa ni wajibu wetu sisi sote kujipanga namna tutakavyonufaika na hii michezo inayokwenda kufanyika. Hii ni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji michezo mbalimbali ya Kimataifa ifanyike. Nimeona kwamba, hata wale walimbwende, wale wazuri, tunategemea miaka ijayo tunaenda ku-*host* duniani, hiyo yote ni utalii. Kwa kweli, ninawapongeza sana kwa jitihada hizo, ni mambo mazuri sana ambayo tunayahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji utalii wa utamaduni. Utamaduni wa nchi yetu tunao mwingi. Tuna utamaduni wa malikale; malikale tunazo nyingi hapa, nchi yetu imebahatika kuwa nayo. Tunahitaji tuongeze utalii katika maeneo yote hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji utalii wa misitu na tunahitaji kujenga hoteli na huduma mbalimbali, ili tuweze kuhudumia watu wote wa namna hiyo. Ninasema kwamba, tukiongeza ujenzi wa hoteli nzuri na tunaweka kumbi za kisasa watu mbalimbali watakuja, watatembelea mbuga zetu, misitu yetu na fukwe zetu, watatuachia fedha nyingi sana ya utalii na nchi yetu itanufaika na hizi rasilimali zilizopo za utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufikia haya yote tuendelee kuimarisha uhifadhi wa hifadhi zetu. Tanzania ni nchi ambayo hapo nyuma tulikuwa tuna hifadhi *one third,* theluthi moja ya nchi yetu ilikuwa imehifadhiwa, 33%, tulikuwa tumehifadhi. Sasa hivi kumekuwa na chokochoko nyingi, wafugaji, mara wakulima wanavamia hifadhi, tunazidi kupunguza, lakini ninasema uhifadhi

nao ni muhimu. Wanyama ni muhimu kama sisi tulivyo muhimu, sote tuliumbwa na Mungu, tunatakiwa tuhifadhi na sisi sasa tutumie hizo hifadhi ili zituletee utajiri na zituletee fedha za kigeni, ili tuweze kuendelea kwa hiyo, ni lazima tuendeleze uhifadhi, hilo ni la msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, tunataka fedha zinazotokana na utalii ziongezeke na zitaongezeka iwapo tutatoa huduma nzuri kwa watalii wanaokuja. Tunataka wakija leo wakawashawishi na wengine waje, wakae muda mrefu zaidi na ili wakae muda mrefu zaidi ni, kama pale niliposema kwamba, tuongeze *value* ya vitu tunavyovitoa kwa watalii mbalimbali, waweze kuacha fedha nyingi sana. Tunaona mchango wa sekta hii kwenye upande wa fedha ni mna tutapata fedha nyingi za kigeni zinazotokana na utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana mimi kwenye mchango wa juzi nimesisitiza tununue ndege nyingi kwenye shirika letu la ndege ili likalete watalii mbalimbali kutoka duniani, waje hapa watuletee fedha za kigeni na nchi iende mbele. Tuongeze ajira, tuongeze mchango wa sekta hii kwenye uchumi na hii hali itakuwa ni nzuri sana. Kwa hiyo, ninaomba tuongeze uwekezaji kwenye matangazo ya vivutio vyetu na sisi tutashirikiana bega kwa bega na Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya, tunataka tuongeze mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja na ninawapongeza sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hasunga ahsante sana kwa mchango wako.

Nilimwita Mheshimiwa Bakari Bakari Shingo, atafuatiwa na Mheshimiwa Rashid Mohamed Mtima na Mheshimiwa Magreth Ezekiel Baraka ajiandae.

**MHE. BAKARI B. SHINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia tena Wizara yetu hii muhimu sana ya Maliasili na Utalii. Sipo mbali sana na Wabunge wenzangu kwa pongezi nyingi sana zinazotoka kwa

Serikali yetu, hususani kwa Waziri mwenye dhamana, Katibu Mkuu na Watendaji wake. Ninakubaliana kwamba, wanafanya kazi vizuri sana na ni haki yao kupigiwa makofi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyojua, binadamu hatuna ukamilifu, ninaamini kwamba, kuna mambo ambayo yanahitaji yaboreshwe kwa maslahi mapana ya Taifa letu. Kuna hii kadhia ya baadhi ya wafugaji wanaporuhusu mifugo yao kuingia kwenye mashamba ya wakulima. Kwa kawaida baada ya kuingia, Afisa Kilimo huenda kufanya tathmini ya hasara iliyopatikana kisha kumwambia mkulima au mfugaji alipe ile fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi fidia inakuwa ni ndogo, lakini udogo ule haufanani na pale ambapo mifugo ya Serikali, mifugo ya Kitaifa, kama tembo na kadhalika wanavamia kwenye mashamba ya wakulima. Pia, anapovamia kwenye makazi huleta hasara kubwa ya mazao, pamoja na majeruhi kwa wananadamu, sambamba na vifo vyao. Kumekuwa hakuna utaratibu maalum au mzuri unaoweza kuonesha kuguswa kwa Taifa juu ya kupotelewa kwa mwanadamu kutokana na majeraha ama kuuliwa na wanyama hao wakali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba Mheshimiwa Waziri aangalie hilo kwa jicho la pili kwamba, kuna haja ya kuangalia thamani ya utu kuliko ilivyo sasa. Kwamba, mazao ya mkulima yakiliwa na mnyama anayetokana na mkulima na mfugaji basi, mathalani anapigwa faini pengine shilingi 500,000, lakini binadamu akiuliwa na tembo anaweza akalipwa pengine shilingi 1,000,000 kwa usumbufu ama kwa karaha kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba paangaliwe hapo, ili pia, pafanane na thamani. Hatusemi kwamba, kuwalipa labda 10,000,000 au 20,000,000 sawa na uanadamu, hapana, lakini angalau wale wanaokuwa katika matanga yale na wale waliobaki pale wametokewa na msiba huu kwa ghafla, waweze kupata vitu vya kujiandaa, hasa ukizingatia kwamba, mtegemezi wao anakuwa ameondoka ghafla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, ninarudi kwenye suala la Jimbo letu la Ukonga. Tuna shetani, tuna mzimu

ambao sasa hivi unakwenda zaidi ya miaka 10, kuhusiana na Msitu wetu wa Kazimzumbwi. Ninaendelea kusema na nitaendelea kuikumbusha Serikali na kumwomba Waziri mwenye dhamana kwamba, ifikie mahali sasa tumalize.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila shaka Tanzania ni ya kwetu, Waziri ni wa kwetu, Serikali ni ya kwetu, misitu ni ya kwetu na Watanzania ndiyo sisi. Hakuna sababu ya suala la Msitu wa Kazimzumbi kuendelea kula miaka na miaka mjadala Bungeni. Watangulizi wangu walizungumza hilo, nimefika na mimi ninazungumza hilo. Ninaomba sasa tufikie mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Msitu wetu wa Kazimzumbwi suala lilipofika sasa hivi ni dogo sana na bahati nzuri Mheshimiwa Waziri Mkuu ametoa maelekezo akimweleza Waziri mwenye dhamana sasa liishe. Toka Mheshimiwa Waziri Mkuu atoe maelekezo leo ni zaidi ya wiki tatu; mimi kama Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Ukonga, lakini pia, mwakilishi wa wakulima wale, sijaona hatua madhubuti ama ya makusudi ya kuweza kufikia mwisho wa suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri mwenye dhamana ameniambia niwasiliane na Katibu Tawala wa Mkoa; nilitarajia kwa sababu, ipo Dar es Salaam na eneo hili lipo Dar es Salaam, umbali usiozidi kilometa 20, basi tungekuwa tumefikia hatua fulani. Leo hii niko hapa mjengoni, hapa Bungeni, wananchi wakulima wameenda kwa Katibu Tawala, lakini hadi sasa hakuna majibu yaliyonyooka. Hii hali siyo nzuri, haitii matumaini kwa Watanzania wenzetu. Kwa hiyo, ipo haja sasa ya watendaji twende sambamba na wimbo tunaoimba kumsifia Mheshimiwa Rais kwa kazi anazozifanya, sambamba na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ujumbe na harakati alizozifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama watendaji, wasaidizi wa Mheshimiwa Rais, wasaidizi wa Waziri Mkuu, hawataenda sambamba na kauli za viongozi wetu, tutakuwa tunatwanga maji kwenye kinu. Msitu wa Kazimzumbi hatua iliyobaki ni ya kwenda kuhakiki mipaka, kilichofanyika ni, msitu ule umepakana na Wilaya ya Kisarawe na Wilaya ya Ilala, katika upimaji wao watu wa

Maliasili wameenda wakaweka mahali mapipa, kama alama ya kuonesha mwisho wa mipaka yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kama wamehamisha mipaka kutoka upande ambao ndiyo umevamiwa, upande wa Wilaya ya Kisarawe, mipaka ile wakaleta Wilaya ya Ilala, kitu ambacho kimesababisha wakulima wa Kata ya Zingiziwa, Chanika na Buyuni kuishi maisha magumu sana. Kwa hiyo, ninaomba hapa tulipo, Mheshimiwa Waziri, nikiwa niko Bungeni ninawawakilisha wananchi, hili ni jambo ambalo limechukua miaka mingi, zaidi ya 15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu Waingereza, waliotutawala, waliacha wamemaliza huu mgogoro toka mwaka 1954, lakini pia, waliacha wamepima ramani. Hatuna sababu ya kuhangaika, kama wageni waliona umuhimu wa kuchora ramani, waliona umuhimu wa kupima ile ardhi, tunashindwa wapi? Tunakwama wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo tunavyokuwa tunakwama ndiyo yanasababisha sasa baadhi ya wananchi wanasema kuna watu wana maslahi binafsi kwa sababu, kama Taifa ni la kwetu, ardhi ni ya kwetu, wanaolalamika ni Watanzania. Waziri Mkuu ni wa kwetu, Rais wa kwetu, Waziri mwenye dhamana wa kwetu, Mkuu wa Mkoa wa kwetu, Katibu Tawala wa kwetu, tunashindwa wapi? Tumerogwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba, kama tumerogwa, basi ninatumia nafasi hii kujirogoroa. Sasa tuwe Watanzania, tuwe watu tulio huru zaidi. Ninaomba sana Waziri mwenye dhamana anihakikishie tu kwamba, sasa tunakwenda kumaliza suala hili ndani ya mwezi mmoja kwa sababu, kilichobaki ni kupima na siyo kuchora tena michoro mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa nafasi uliyonipa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bakari Bakari Shingo, ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Rashid Mohamed Mtima, atafuatiwa

na Mheshimiwa Magreth Baraka Ezekiel na Mheshimiwa Dkt. Neema Peter Majule, ajiandae.

**MHE. RASHID M. MTIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ninachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na kunifanya leo niwepo hapa. Ninakushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaanza kumpongeza Mheshimiwa Rais. Ninampongeza Rais, katika kipindi hiki cha Awamu ya Sita alivyochukua hatua ya kuifanya Wizara hii iweze kufanya vizuri; kwanza kwa maelekezo yake na kuelekeza kwa vitendo kwa kufanya *Royal Tour,* ambayo imeleta matokeo makubwa sana katika sekta ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na *Management* yote ya Wizara kwa sababu, kwa kipindi hiki ambacho wao wamekuwepo katika utendaji wa kazi tumeona mabadiliko. Ukisoma katika hotuba au taarifa ya bajeti yote ya Wizara, wameonesha maeneo mbalimbali ya mafanikio. Tumepata tuzo katika maeneo mbalimbali, kuna utekelezaji wa maeneo mbalimbali ya miradi ambao umekwenda vizuri, ambao tunatarajia baada ya muda utatoa matokeo mazuri katika sekta hii ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maeneo tunatakiwa tuweke nguvu zaidi. Maeneo ambayo sisi tunatakiwa kushauri kama Bunge, ili tuweze kufanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nianze kuchangia eneo la kwanza, lile ambalo Mheshimiwa Rais mwenyewe amefanya. Rais amefanya *Royal Tour,* kwa maana ya kutuelekeza kwa vitendo. Inawezekana alikuwa anaona haja kabisa kusema, jamani tangazeni utalii, lakini amefanya kwa vitendo, ili sisi tupite pale tuchukue alipofanya yeye tuendeleze zaidi. Sasa katika eneo hili naishauri Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokiona mimi, Wizara hii ili iende kwenye *pace* ambayo Rais anataka ni kuhakikisha kwanza

Bodi ya Utalii inafanya kazi vizuri. Bodi ya Utalii ni chombo ambacho, kama nchi, tumesema ndiyo *leading* na *coordinating institute* kwenda kutangaza utalii wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama suala la muundo wa taasisi yenyewe, twende tuifanyie kazi, ili dhamira yetu ya kufanya chombo cha kutangaza utalii itimie. Kama ni miundo ya taasisi zingine zilizoko kwenye sekta hii ya utalii inafanya taasisi hii, ambayo tumeiunda maalum kwa shughuli hii, kutofanya kazi twende tukafanye mabadiliko, ili muundo wake uwezeshe kufanya lile ambalo tumelilenga. Twende tukaijengee uwezo wa *manpower* na kuipa fedha ili iende ikatangaze utalii kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo watu wa Ngorongoro wakitoka inawezekana wanaenda wakiisemea Ngorongoro tu. Watu wa *TANAPA* wanaenda kutangaza taasisi yao, lakini tukiiwekea taasisi hii nguvu yote, maana yake ni tunautangaza utalii kwa ujumla wake, ambao unatengeneza *package* nyingi zinazogusa taasisi na vivutio vilivyoko kwenye taasisi nyingi, hivyo kuvutia watu wengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imezungumzwa hapa na watu wengi sana, Tanzania tunavyo vivutio vya asili, ambavyo huwezi kupata nchi yoyote. Mlima Kilimanjaro huwezi kuupata kwingine kokote, Ngorongoro huwezi kuipata sehemu nyingine yoyote. Ndiyo maana Rais akatuambia kilichobaki ni sisi kwenda kutangaza, ili kuwavuta watu. Kwa hiyo, eneo hili ninaomba Wizara iwekeze nguvu kuifanya *TTB* ifanye kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, ambalo ninatamani kuchangia ni mwingiliano wa wanyamapori na binadamu. Eneo hili limezungumziwa sana, lakini ukisoma katika taarifa tulikuwa na mkakati wa kushughulikia suala hili, wa miaka mitano iliyopita, ambao mwaka jana ulikuwa wa mwisho na tathmini imefanyika. Ninachotaka kujiuliza ni je, tathmini imetupa nini? Ziko namna mbalimbali au tumetumia nyenzo mbalimbali kukabiliana na suala hili? Je, tumeweza kulipunguza? Je, katika hizi nyenzo tunazotumia, ipi ni bora zaidi kwa kutafuta ufumbuzi wa muda mfupi na kwa kutafuta ufumbuzi wa muda mrefu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndipo sasa tuone tunatokaje hapa. Haiwezekani sisi Watanzania tumepewa dhamana, lakini kila mwaka suala hili linakuwa la kuzungumzwa. Kila Mbunge akisimama, anazungumzia wanyamapori. Tuseme hatuwezi kulinganisha na chochote kwenye uhai wa mwanadamu kwa sababu, hata hao wanyama tunawalinda, ili ikiwezekana tupate utalii uje kusaidia wananchi hao. Sasa leo wanaondoka, hata kama akiwa mmoja mmoja, kwa hiyo, eneo hili tuliwekee nguvu. Ninachoomba hapa ni Wizara ifanye tathmini na kama imefanya kwa mkakati wa miaka mitano uliopita, waone sasa ni maeneo gani ya kufanya, ili ikija awamu nyingine tupate taarifa kwamba, matukio haya yamepungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kukaa hapa tunajinasibu tu kwamba, mwaka jana tulilipa watu 2,000, mwaka huu tumelipa watu 3000. Maana yake ni nini? Ninaona wanaongezeka. Tuseme, mwaka jana tumelipa 2,000, mwaka huu tumelipa 500 tu kwa sababu, tumetengeneza *effective strategies* kwenye kudhibiti, kwa hiyo, ninaomba tuweke nguvu katika suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ninataka nichangie ni malikale. Nimeona kwenye taarifa masuala mengi yanafanyika kwenye malikale; kanuni zimetengenezwa za Mwaka 2025 na miongozo mbalimbali imetengenezwa. Mikakati ya kuandaa maeneo ya hifadhi na usimamizi wa malikale, hivyo vimefanywa. Hapa, ninataka nichangie kidogo na hasa katika eneo la kusini. Ukiangalia maeneo ya malikale Kusini, unaona suala la Eneo la Vita vya Maji Maji, lakini miongoni mwa maeneo ya malikale ni utawala ambao nchi yetu imepitia toka utawala wa asili, wa kikoloni mpaka uliopo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Mtwara, ukaenda Mikindani, tumeona kuna vitu vinafanyika na *Trade Aid,* ambayo ni *Old* Boma ya Mjerumani. Huwezi kuacha na *Old* Boma ya Newala, ambako kuko kimya, yale majengo yanaoza tu. Hatuwezi kukarabati yale majengo tukaweza kuonesha tulikotoka na tulipo sasa? Tukaweka vivutio na watu wakatembelea maeneo yale?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Wizara iangalie namna ya kupanua suala la malikale kule Kusini, ikihusisha na Boma la

Mjerumani la pale Newala Mjini. Hata Magereza ya Newala ilijengwa na Mjerumani, lakini ukienda hata *quarter* za polisi zile zilijengwa na Mjerumani. Suala la utawala pale, wa Mjerumani mpaka Mwingereza, ni suala ambalo ni la kihistoria katika eneo la Newala. Twende tukaoneshe vizazi vyetu vya leo tulikopita mpaka leo tulipofikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hilo la utawala pia tuoneshe waasisi wetu. Ukienda kule Newala ukimzungumza Lawi Nangwanda Sijaona na *TANU* ni mtu ambaye amepambana sana. Kule Newala wakoloni waliweka mfumo ambao viongozi wetu wa mila, maliwali walikuwa wanafanya nao kazi kwa karibu sana. Kwa hiyo walikuwa hawawezi kuingia kwenye shughuli za ukombozi moja kwa moja, lakini akina Liwali Manzi walimchukua Lawi Nangwanda Sijaona kwenda kumweka Lipalwe kule nje ya mji kabisa ili aendelee kutoa kadi za *TANU* ili nchi yetu iweze kupata ukombozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapi leo Nangwanda anaonekana, ambaye ndiye Mbunge wa kwanza wa Jimbo la Kusini? Nenda Lindi anaonekana? Nenda Mtwara anaonekana? kwenye uwanja tu wa Nangwanda Sijaona? Ni mambo gani tunaweza tukayafanya kuonesha kwamba hata vijana wetu wanaozaliwa leo wakiona historia ya Liwali Sijaona, basi watakuwa na uzalendo, kwamba uko wakati unasamehe yako binafsi unasimamia ya Taifa hili, hicho ndicho walichokifanya akina Lawi Nangwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wasingesamehe ya kwao kuacha utumishi kwa ajili ya Taifa hili tusingefika huku! Watoto wetu wanatakiwa wajue hilo, kwamba inafika muda unasamehe ya kwako kwa ajili ya nchi, tusiweke ya kwetu kwanza. Pamoja na kufundisha darasani, twende tukawaoneshe katika maeneo ambayo hawa waasisi wamefanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mtima kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, nilimwita Mheshimiwa Magreth Baraka Ezekiel, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Neema Peter Majule na Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, ajiandae.

**MHE. MAGRETH B. EZEKIEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunipa nafasi hii adhimu ya kusimama tena katika Bunge lako Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru na ninapenda kwa kuanza kumshukuru Rais wangu, kipenzi changu, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutunza hazina na chanzo kikuu cha utalii cha nchi yetu ambacho ni amani. Amani kwa tafsiri ya nje inaonekana kama ni kitu chepesi sana, lakini kwa tafsiri ya ndani ni kitu kigumu sana, kwanza kukitunza, kukienzi na kukiheshimu. Nasi tunaona umuhimu na maana halisi ya amani katika uchumi wa Taifa lolote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaangalia wenzetu wa Dubai, Nchi za Umoja wa Falme za Kiarabu, tunaona tangu vita ya Iran na Israel imeanza wamepoteza kwa kila siku kutokana na takwimu za *World Trade and Tourism Council*, kila siku iliyokuwa inapita walikuwa wanapoteza Dola za Kimarekani 600,000,000. Kwa hiyo hii inatuonesha haijalishi utakuwa na vitu vingapi vizuri, pale ambapo hapatakuwa na amani hakuna mtu atapenda kuja kwenye Taifa lako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda vilevile kumshukuru Makamu wa Rais, Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi kwa kuendelea kuweka umuhimu katika mazingira na Muungano wa Taifa letu kati ya Tanzania Bara na Zanzibar. Muungano vilevile unaonekana kama ni kitu ambacho ni chepesi sana, lakini ni kigumu sana. Kuna mataifa mengi ambayo yamewahi kuwa na muungano, lakini mpaka leo hii Muungano wetu kihistoria ni muungano unaodumu zaidi ya miaka na miaka na hilo ni jambo la kuendelea kupongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira yetu, tunaishi katika dunia yenye mabadiliko makubwa ya tabianchi, tunaishi kwenye dunia ambayo kuna ukame, tunaishi kwenye dunia ambayo hata

hawa wanyama tunaojaribu kuwalinda, wana athari ya kupotea na kutoweka katika uso wa dunia pale ambapo athari za tabianchi zitaendelea kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda vilevile kumpongeza Waziri Mkuu, Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba kwa kuendelea kusikiliza kero za wananchi wa Tanzania na kwa muktadha huu anaendelea kuleta Taifa lenye umoja na ujumuishi, lakini zaidi anaendelea kuyaheshimu maono ya Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan la kuleta tabasamu, furaha na utu katika uso wa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda vilevile kumpongeza Waziri wa Utalii, Dkt. Ashatu Kijaji kwa matumizi mazuri ya *TEHAMA* na kuelewa kwamba dunia haipo pale ilipokuwa miaka iliyopita. Bila kuwekeza katika teknolojia, bila kuwekeza katika ubunifu wa kufanya mambo kwa utofauti, basi hatutoweza kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Wizara nzima ya Utalii kwa kuendelea kuweka vipaumbele muhimu katika kulitangaza Taifa letu, lakini kama nilivyogusia awali, tafsiri na baadhi ya vitu ambavyo vinaonekana si utalii, lakini ni utalii katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa Taifa letu lina makabila 127 na hiki ni kichocheo pekee cha kuleta watu kuonesha utamaduni wetu, asili yetu na sisi Watanzania ni kina nani. Kuna nchi nyingi sana zina makabila mengine mawili, mengine matatu, lakini mpaka leo kuna vita na kuna *genocide* zinazoendelea, lakini sisi tuna makabila 127 na si vile tu ni nchi ambayo tupo kwenye Muungano na si vile tu, ni nchi ambayo ina dini mbalimbali kwa Watanzania na watu wake. Ni muhimu sana kulifahamu hili kwani kuna mataifa mengine yenye dini nyingi ni ngumu sana kupata umoja na mshikamano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kwa kuanza kutafsiri nini maana ya utalii. Utalii ni kitendo, shughuli ya kusafiri kutoka sehemu moja hadi nyingine nje au ndani ya nchi, kwa lengo la kujifunza, kupumzika, burudani au shughuli za biashara bila nia ya kuhamia au kufanya kazi ya kudumu kwa eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu inajivunia kuwa na *UNESCO World Heritages* saba duniani, ambacho si kitu cha kawaida kukipata katika eneo moja, vilevile sisi tuna sehemu inaitwa Olduvai *Gorge*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Olduvai *Gorge* ni *the cradle of humankind*, ndiyo pale binadamu wa kwanza alipotokea, vivyo hivyo, ni muhimu sana kwa Watanzania wote kuelewa rasilimali zilizobebwa na nchi yetu na zina maana gani kwa dunia. Sasa hivi tunaingia kwenye *world of super intelligence*, lakini *there is no AI*, hakuna *AI* wala *super intelligence* bila Tanzania. Kwa sababu Tanzania ndiyo nchi pekee inayoweza kuonyesha uthibitisho wa binadamu. Mheshimiwa mmoja alisema kuanzia *Zinjanthropus*, *Homo erectus, Homo habilis* na hivi vyote ukitembea pale Ngorongoro kidogo tu unapata ushahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuhoji, kwa wale Watanzania na watalii wanaoingia ndani ya nchi yetu, je, tunafahamu wanatumia shilingi ngapi? Kwa sababu tunafahamu idadi ya watalii wanaoingia, tunafahamu idadi pengine kwa kiasi mapato ya ndani, hela ambazo wanachangia kwenye uchumi wetu katika kutoa na kulipia vitu. Je, tumewahi kujihoji kwamba wale watalii wanaokuja, wana *disposable income* kiasi gani? Yaani wana pesa kiasi gani ya akiba ambayo wangeweza kuwekeza kwenye nchi yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninahoji hii kwa sababu ukiangalia wenzetu wa Dubai, hakuna cha ajabu walichokifanya duniani. Kwa sababu kipindi Dubai inajenga *Airport* ya Dubai, walikuwa wametoka kwenye ukoloni. Wakaulizwa ninyi mnajenga *Airport* kubwa ambayo haijawahi kuonekana duniani, mnajenga ya nini? Hakuna mtu atakuja, wakakaa kimya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dubai wakaanza ujenzi wa pili wakajenga *The Burj Al Khalifa*, wakawaambia ninyi mnajenga *the largest and tallest building in the world* ya nini, mnapoteza pesa nani atakuja? Wakakaa kimya vilevile, wakaendelea kujenga *Mall of Emirates* wakajenga na vitu vingine, lakini hii inalenga katika nini? Hii inalenga katika uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji na utalii sasa hivi si kile unachokiona, uwekezaji na utalii ni kile unachoweza kukitengeneza kwa kutumia kile ulichonacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba jambo moja tu, sisi kama Watanzania, tuwekeze katika kutengeneza miji ya kitalii tofauti na ile tunayoifahamu, kwa sababu leo tunapokwenda kubuni *the Tanzanian*, *Tanzanite City for World Travel*, inamaanisha nini? Inamaanisha kwa kila mtalii anayeingia katika Taifa letu, tunaweka lengo ya *mega and giga projects* ambazo tutazijenga ambazo zitakuwa za mfano. Kupitia hili na kupitia hii *Tanzanite visa* ambayo ninasema, hawa watalii hatutawatumia tu kwa kupiga picha wanyama wetu na kuwapeleka, lakini tutawatumia wao kujenga *infrastructure* yetu ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama vile ambavyo tunajenga *special economic zones* kwa ajili ya uwekezaji wa *cement*, chuma, vilevile tunapaswa kujenga *special economic tourism zones*, ambazo zinaenda kututofautisha sisi na wenzetu kwa sababu, kusema kwamba tuna simba, ndovu, tuna hiki, tuna hiki, wenzetu vilevile wanavyo, lakini sisi tunapaswa kutafiti zaidi dunia inaelekea wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wa China kule Chengdu wamejenga mji ambao treni zenyewe zinapita mita 200 juu, kuna treni inaingia hadi kwenye makazi na nyumba ya watu. Kuna *apartments* zimefungamana na *aquariums*. Kwa hiyo, sisi vilevile kwa jiografia ya nchi yetu na umuhimu wake na utofauti wake, tuna nafasi kubwa sana ya siku moja kusema kwamba *Tanzania is the world's destination for tourism* na siyo utalii wa wanyama, hata utalii wa teknolojia. Sasa hivi kuna mataifa hayana wanyama hata mmoja lakini wana teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, mimi ningependelea kusema mambo yafuatayo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sekta zetu muhimu ambazo zinapaswa kufungamana na sekta ya utalii na sekta yetu mojawapo ni sekta ya michezo na *entertainment*, kwa sababu siku hizi watu hawasafiri kuona vitu, watu wanasafiri ku-

*experience* vitu. Kuna mtu anafahamu kwamba nikienda Indonesia, nikienda Bali au nikienda Cancún, kwamba kule ninakwenda kutafuta nini. Kama Ibiza, Ibiza watu wanaenda kufanya starehe tu, hakuna lingine. Kwa hiyo sisi, tuna nafasi, tuna visiwa vingi sana. Siyo mbaya hata kidogo tukivitenga vingine kwa ajili ya mambo fulani na sisi vilevile tukaji-*rebrand*, siyo lazima kila siku Tanzania tuwe *the same* Tanzania, *we have a chance to rebrand our country*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante ninapenda kukushukuru na vilevile ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Magreth Baraka Ezekiel kwa mchango wako, ndiyo maana tunahitaji *more Gen-Z's* kwenye hili Bunge. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nilimwita Dkt. Neema Peter Majule atafuatiwa na Mheshimiwa Anna Richard Lupembe na Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo ajiandae. Endelea Mheshimiwa Majule.

**MHE. DKT. NEEMA P. MAJULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye Wizara hii muhimu ya Maliasili na Utalii. Kweli kabisa hii ni Wizara ambayo inatuingizia fedha za kigeni, hivyo tunaiangalia kwa jicho la tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwa moja nianze kwa kumpongeza sana na kumshukuru Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye amenyanyua utalii kwa kiasi kikubwa yeye mwenyewe alipoamua kufanya kwa vitendo kupitia filamu ya *Royal Tour*. Haikuwa kitu rahisi kwa Rais mwenyewe kuigiza. Mimi sijawahi kusikia Rais anafanya igizo, yaani anaingia kwenye filamu akiwa *sterling*, aliweza kufanya hivyo na imepandisha idadi ya watalii kutoka 2,000,000 mpaka milioni 5.9 haya ni mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila Mbunge ambaye angesimama hapa asingeacha kusema hilo, lakini sisi ambao tumepata nafasi ya kuchangia moja kwa moja, Rais ajue Tanzania nzima tunampongeza sana na tunamuunga mkono katika jambo hilo.

Hiyo imepita *phase one,* tunamwomba tena kwa *phase two*, sasa ile ilikuwa ya kwanza ya safari hii sasa iwe-*planned* vizuri zaidi ili iweze kuleta *impact* kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona Wizara imesema kwa mipango yake mwaka 2030 watafikisha watalii milioni nane. Mimi ninasema inaweza kwenda mpaka milioni 10, ikichangia hii *second phase* ya *Royal Tour,* lakini pia na mashindano ya *AFCON*. Mashindano ya *AFCON* yatakuja nchini kwetu, kwa hiyo hivyo ni utalii wa kutosha wa kutangaza vivutio vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu Watanzania tuna vivutio vingi ikiwepo maziwa makubwa matatu kwenye nchi yetu. Yaani mimi nikiangalia Afrika hivi halafu nikaona nchi yangu ilipokaa, ninaona Ziwa kubwa la Victoria, ambalo linalisha Misri yote, ninaona Ziwa la Tanganyika limejikita hivi, limechukua karibu eneo zima, ninakuta Ziwa Nyasa, ninakuta mito inavyopita, misitu na vitu vingine vyote, hivi ni vivutio vikubwa sana vya nchi yetu, watu wanaitamani nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo zaidi ya misitu, bado tuna mbuga za wanyama ambazo zimekuwa kivutio kikubwa cha watu kuja kuona. Kwa hiyo, vitu hivi tuendelee kuvitangaza na vitaweza kuleta matunda makubwa hasa kuongeza mapato ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisisahau moja kwa moja niweze kushukuru Wizara hii ya Maliasili na Utalii, nikimuenzi Mbunge wa Kondoa ambaye ni Waziri wa Utalii, hongera sana Dkt. Ashatu Kijaji, lakini pamoja na Naibu Waziri, pamoja na Katibu Mkuu na watendaji wengine, wanafanya kazi nzuri ndiyo maana tumeweza kuyaona haya matokeo. Sasa ninaomba nichangie machache ambayo ningetamani kuyachangia kwenye hii Wizara, nisirudie yale ambayo wengine wengi wamesema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niseme kwamba, zile jamii zinazozunguka, zipate mahitaji muhimu, kwa sababu kwanza wanatulindia hifadhi zetu, lakini pia wanaweza kutangaza hifadhi zetu. Siyo hivyo tu, ni watu bora kabisa ambao wanaweza

wakafanya kazi nzuri zaidi hata kuchukua mambo ya *tour guide* wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanaokaa karibu na hifadhi zetu, niseme tu kwanza wanajua mpaka lugha za Wanyama, lakini wanajua *behaviour* za wanyama. Watu hawa wakiwa *trained* kuwa *tour guide* watafanya vizuri zaidi kuliko mtu ambaye hakai karibu na hizi hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, niombe hata Wizara ya Elimu iweze ku-*integrate some topics* ambazo hawa watu wanaokaa karibu na hifadhi zetu waweze kujifunza kuanzia watoto wadogo wakiwa shule za *primary*, baadaye sekondari, vyuoni mpaka vyuo vikuu ili kama tunataka kitu kiwe *sustainable*, utalii uwe *sustainable*, basi tuuingize moja kwa moja kwenye mitaala yetu ili vijana wetu waweze kujifunza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niseme kwa kufahamu mali tulizonazo na rasilimali tulizonazo, moja kwa moja tunajenga uzalendo. Vijana wetu wataipenda nchi yao, wakijua ni nchi bora kuliko nchi zote, nchi ambayo Mungu ameikirimia vitu vyote hivi wajifunze wafahamu na wenyewe ndiyo wachukue nafasi sasa ya kutangaza hifadhi zetu na waweze kutangaza mbuga zetu za wanyama na vitu vingine. Kwa hiyo ninaomba *integration* ya *syllabus* katika vitu hivi ambavyo tunataka viendelee kutoka kwenye *generation* moja hadi *generation* nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ningetamani kulisema ni kwamba kila mkoa una vivutio vyake, mimi moja kwa moja nimsifie sana Mkuu wangu wa Mkoa, Dada Rosemary Senyamule akishirikiana vizuri na watendaji wa Serikali, lakini pia akishirikiana na Chama Cha Mapinduzi, Mwenyekiti wangu wa Mkoa Alhaj Adam Kimbisa, siwezi kumsahau, Katibu wetu wa Mkoa, Pili Agustino, watu hawa kwa pamoja wameweza kupanua utalii hapa Dodoma, tumepata watalii wengi kwa mwaka huu mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka huu mmoja watalii wa nje, kutoka 171 mpaka 12,031 lakini watalii wa ndani, kutoka 2,313 mpaka 35,694 wamejitahidi na vitu wanavyokuja kuviangalia

Dodoma pia tunavyo. Sisi tuna Pori la Swagaswaga, hiyo ni *National Reserve* tunayo, pia tuna Pori la Mkungunero, tuna michoro ya asili ambayo dunia nzima hakuna, ipo pale Kolo lakini siyo hivyo tu tuna vitu vingi, tuna misitu Kondoa, tuna misitu ya Chemba ambayo inafuga nyuki sana, tuna misitu Kongwa, tuna misitu Mpwapwa, kwa hiyo watu wanakuja kuangalia vitu hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, Mkuu wangu wa Mkoa amekuwa mbunifu sana, hata watalii wengine wanakuja kuangalia *UDOM*. *UDOM* hata ninyi hapa Wabunge wageni tupo karibu 63%, *University of Dodoma* ni mahali pazuri pa kwenda kutembea. Huwezi kuona *faculty* moja mpaka *faculty* nyingine unasafiri kwa basi, yaani huwezi kutembea kwa miguu ku-*join Education Faculty* kwenda kwenye *Science Faculty* au kwenda kwenye *Social Faculty,* unapaswa kupanda gari. Kwa hiyo ni sehemu nzuri ya kwenda kutalii. Wabunge wasiondoke bila kwenda *UDOM*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Mji wa Serikali pia, ulisemwa na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kutoka mwaka 1973, utajengwa, Marais wote wamepitia mchakato, sasa mji huo umejengwa ni dhambi kabisa kuondoka Dodoma bila kwenda Mtumba kuangalia Mji wa Serikali, maghorofa yameota kama uyoga, Rais amefanya, amejenga Mji wa Serikali kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, hapa Dodoma pia sisi tembo wa kwanza alididimia hapa Dodoma, hata hili jina la "Dodoma" limetokana na neno la Kigogo "Idodomya". Yaani hapa palikuwa ni mahali tifutifu. Kwa hiyo tembo aliweza kudidimia hapa Kikuyu. Pale ninaomba Waziri wa Utalii, tujenge *remarkable thing*, hata jengo au mnara kuonyesha ndiyo asili ya neno Dodoma, ambayo sasa hivi ndiyo Makao Makuu yamekuwa Dodoma. Pale ndiyo tuweke *remarkable thing* kwa ajili ya kuenzi neno hili Dodoma pale Kikuyu Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, tuna vivutio vingine vingi ambavyo tunavyo hapa, *TFS* wametupa mizinga 18,000, tumeweza kuzalisha asali kilo 135. Kwa hiyo tumepanda miti pia Dodoma, tumepanda miti 9,840,000, Dodoma hii ambayo ilikuwa kavu inaenda kubadilika kabisa. Hivyo, kila mkoa uangalie vivutio

vyake tuweze kuongeza idadi ya watalii, watalii wa ndani lakini pia watalii wa nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema maneno haya ambayo nimeyasema, ninaomba tuyazingatie ili tuongeze idadi ya watalii. Ninaomba kabisa kuunga mkono hoja ya Wizara hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Majule. Nimwite sasa Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo atafuata na Mheshimiwa Neto Paul Kapalata, ajiandae.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili nami nichangie Wizara yetu ya Maliasili na Utalii. Ninaomba nimshukuru Mungu ambaye ametupa uzima na uhai tupo muda huu, wakati huu tukipumua kwa ajili ya uhai wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa kwa sekta hii ya utalii. Mheshimiwa Rais kazi ameifanya kubwa ya kulitangaza na kuhakikisha kuwa Taifa letu linapata mapato na kuongeza watalii katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi kubwa ambayo wanaendelea kuifanya kwa ajili ya kusimamia sekta ya utalii. Nimpongeze Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu, nao wameendelea kusimamia vizuri. Niwapongeze Makamishna wote pamoja na Wakurugenzi wote wanaosimamia wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu Waheshimiwa Wabunge wa majimbo wamezungumza; ninaomba nizungumzie kuhusu tembo. Katika kata zangu mbili, Kata ya Katumba na Kata ya Litapunga katika Vijiji vya Kalungu, Iwimbi, Tambazi A na B, Mtambo, pamoja na Kijiji cha Kambuzi A na B, hivi ninavyoongea sasa hivi tembo wapo na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni janga kwa sababu Waheshimiwa Wabunge wengi wamesimama, wamezungumzia kuhusu tembo ambao wameleta athari kubwa sana kwa wananchi. Katika jimbo langu hizo kata mbili mazao yote yameliwa na tembo, wananchi hawana kabisa mazao, hawatoki na wala hawatembei. Hivi ninavyoongea hapa kule wananchi wamejifungia, tembo wapo kwenye mashamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Serikali ituangalie na itoe tamko rasmi kwa ajili ya hawa tembo. Alikuwa ananiambia Mheshimiwa Kadogosa kwamba yeye kwenye jimbo lake jana tembo amemuua mama, amefariki, wamemzika jana ile ile. Sasa hili limekuwa janga, tunaiomba Serikali, athari hii ni kubwa. Ukiangalia wananchi sasa hivi hawana chakula, mazao yote yameliwa na tembo na wapo katika maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tembo wamezidi watafute mikakati, sijui watuongeze nini, mimi hata sielewi. Maana mimi ninavyosema kila Mbunge ambaye yupo katika maeneo yao kuna athari ya tembo. Sasa sijui wamezaliana sana? Mimi hata sielewi, sijui wametokea wapi? Kwa sababu ni janga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tembo ni janga; katika vijiji hivyo nilivyovitaja wamepata athari kubwa sana. Tunaiomba Serikali itusaidie, hata basi kutoa kifuta jasho kwa wananchi ambao wamepata athari kubwa na tembo, kwa sababu hawana kitu. Tunaiomba Serikali yetu sikivu itaona jinsi gani ya kuweza kutusaidia kuhusu hawa tembo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niipongeze sana *TAWA,* nimpongeze Kamishna wa *TAWA*, amekuwa rafiki na wananchi wangu wa Kata ya Ugara, Kijiji cha Katambike, Kitongoji cha Kamini; wameanza kuwajengea zahanati. Ninaomba niwapongeze sana *TAWA* na niwashukuru na niseme ahsanteni sana *TAWA* kwa kazi kubwa. Wameanza, ninaomba wasiishie hapo, wahakikishe zahanati ile inakwisha kwa sababu wameungana na kuwa marafiki na wananchi wa Kijiji cha Katambike, Kitongoji cha Kamini. Basi huo urafiki kwa sababu wanafanya kazi nao ninaomba basi ile zahanati iishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa unyenyekevu mkubwa sana ninaomba niwashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpongeze Kamishna wa *TFS* kwa sababu jimbo langu mimi ni jimbo la hifadhi. 30% tu wanakaa wanadamu, lakini 70% ni misitu. Sasa nina *TAWA,* nina *TFS* na nina *TANAPA*. Ninampongeza Kamishna wa *TFS,* amejitahidi sana kuja mpaka jimboni kwangu, amepita na ameangalia uhalisia. Hata hivyo, ninaomba niseme, amepita na ameangalia uhalisia, ninaomba, alitoa maagizo kuwa waje kuhakikisha kwamba wanaweka mipaka kati ya vijiji na vitongoji vya wananchi na *TFS*. Kazi hiyo bado haijafanyika, wale vijana waliokuwa kule kazini wanaendelea kuwapiga wananchi wangu, wanawapiga na wanakatakata mazao yao. Ninaomba sana *TFS* waje waangalie mipaka ya vijiji vyetu pamoja na vitongoji vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nishauri hapa hapa; *TFS* wana misitu, lakini kule kwangu wanavuna sana. Sasa hivi ile misitu ninaomba nitoe ushauri, waingie kwenye *carbon* kwa sababu wana misitu mikubwa sana katika Jimbo la Nsimbo. Kuliko kukata na kuvuna waingie kwenye *carbon*, watapata manufaa zaidi. Kwa sababu wao wanavyovuna na wananchi nao wanakatakata, wanachoma mkaa. Sasa ina maana kuwa uhifadhi wa mazingira unakuwa haupo tena, kwa sababu wanasema mbona *TFS* wanakata mbao? Ninaomba *TFS* tuingie kwenye *carbon,* tutunze mazingira ili basi na hawa wananchi waone mfano huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TFS* vile vile wanatoa mizinga ya asali, Jimbo la Nsimbo bado hawajanufaika ingawa wanailindia misitu yetu, lakini bado hawajawaletea mizinga kuhakikisha na wao vijana, ili waendelee kuhakikisha wanaiweka hifadhi vizuri, basi tunaomba mizinga ya asali ili vijana wa Jimbo la Nsimbo waweze kutundika mizinga ya asali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *TANAPA;* Mheshimiwa Rais ameitangaza *Royal Tour,* tunategemea, kuwa Mheshimiwa Rais alionesha mfano, lakini *TANAPA* katika jimbo langu kuna Mbuga ya Wanyama ya Katavi, hawaitangazi. Hii huwa ninaisema mara nyingi, kwamba, Mbuga ya Katavi, ambayo ni mbuga kubwa na

yenye wanyama wakubwa na kwamba ndiyo yenye twiga mweupe na tembo hao wakubwa wapo katika Mbuga ya Katavi ambako ndiko jimboni kwangu; hawaitangazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wao *TANAPA* vile vile wapo na wananchi, tembo wanatoka kwenye hifadhi wanaenda kula mazao ya wananchi, hata fidia hawalipi. Ni miaka mitatu sasa hivi wananchi wangu wa Stalike hawajalipwa. Ninaomba waje, wafanye tathmini, wawalipe fidia kwa sababu sisi tunalea wale wanyama, tunawatunza, lakini wanafanya uharibifu mkubwa. Sasa kama wanafanya uharibu mkubwa, tunaomba kifuta jasho. Waje watulipe kifuta jasho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANAPA* hawa hawa tunaomba tena waje waangalie mipaka ya *TANAPA* na mipaka ya wananchi, kwa sababu nao, *TANAPA,* wananchi wakifika mtoni wanasema mmetuingilia, wanawapiga. Sasa ninaomba, ili tusipigane, tuoneshane mipaka. Mipaka yetu hii hapa, Watanzania wasiingie huko na wenyewe watulindie wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana kwa kipindi hiki Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumza; tumepata bahati Mheshimiwa Rais ametuletea *AFCON* katika nchi yetu. Ninawaomba *TANAPA* kupitia *AFCON* hii ya 2027, nao sasa waitangaze Mbuga ya Katavi ili watakaokuja kwenye utalii wakatembezwe. Kwa sababu ndani ya Katavi tuna uwanja mzuri wa ndege. Vilevile mle ndani kwenye mbuga zetu kuna uwanja wa ndege ili watalii watakaokuja kwenye *AFCON* wafike mpaka kwenye Mbuga ya Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nisisitize, kifuta jasho *TANAPA*, tunaomba wananchi wa Kata ya Stalike, wale ambao mazao yao yameliwa walipwe kifutia jasho. Muda mrefu sasa umeshapita, miaka takribani mitatu hawajalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niunge mkono hoja. Ahsante sana na Mungu akubariki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Anna Richard Lupembe. Nilimwita Mheshimiwa Taska Restuta Mbogo,

Mheshimiwa Neto Paul Kapalata atafuatia, Mheshimiwa Dkt. Regina Christopher Malima ajiandae.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi jioni hii ya kuchangia bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Kwanza kabisa ninapenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutujaalia uhai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda nitumie muda huu kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi alivyoitangaza Nchi yetu ya Tanzania kwenye filamu ya *Royal Tour* na kusababisha watalii wengi kuja kwenye Nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda nitumie nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii pamoja na Naibu wake, Mheshimiwa Chande na watendaji wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii kwenye taasisi zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, ninayo mambo ya kuchangia kwenye Wizara ya Maliasili na Utalii na nikiwa kama Mjumbe wa Kamati, basi ninaomba nitoe mawazo yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ninaomba nianzie na suala la Serikali. Serikali ilifanya marekebisho ya Sheria ya Fedha Na. 8 ya Mwaka 2020; na kupitia Sheria ya Fedha Na. 11 ya Mwaka 2025, Serikali iliruhusu Taasisi za *TANAPA* na *Ngorongoro (NCAA)* kurejeshewa 51% ya mapato ambazo huwekwa kwenye akaunti za taasisi zilizopo Benki Kuu na kupatiwa idhini ya matumizi na Mlipaji Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nia ya hoja yangu kuisema hapa ni kutaka kuliambia Bunge hili Tukufu kwamba siyo kwamba Serikali inachukua mapato yote ya *TANAPA* na Ngorongoro bali inarejesha 51% kwa ajili ya mishahara na miradi ya maendeleo kadri mipango ya bajeti ilivyoidhinishwa. Uratibu huu umeongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya hifadhi na kuboresha miundombinu ya utalii na kuimarisha huduma za maendeleo ya hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini ninasema hivi? Ninasema hivi kwa sababu kuna picha imeonekana ya kwamba Serikali inakusanya mapato yote, hapana, taasisi hizi zinarejeshewa 51%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali ya 51% mnamo mwaka 2013 Serikali ilianzisha tozo ya *TDL*. Katika tozo hii kuna makusanyo ambayo wanapata zaidi ya zile 51%. *TDL* maana yake ni *tourist development levy*. Tozo hii ni ya asilimia tisa; asilimia sita inakwenda *TDL* na asilimia tatu inakwenda kwenye Mfuko wa Wanyamapori. Nini maana yake? Maana yake ni kwamba mbali ya ile 51% ambayo Serikali inarejesha kwenye taasisi hizi, kuna asilimia tisa...

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mzungumzaji anazungumza vizuri, lakini ninadhani amelisahau Azimio la Bunge. Azimio la Bunge lilikuwa, hizi Taasisi za *TANAPA*, *TAWA* na *TFS* wakusanye fedha, halafu wawagawie Serikali, lakini hali ilivyo ni kwamba Serikali inapokea hela, inawaletea. Sasa sisi tunaoathirika na tembo hela hii ikienda Dar es Salaam Hazina ije irudi, tembo wameshatumaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Taska Restuta Mbogo, unaipokea Taarifa hiyo?

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei taarifa ya msemaji aliyepita kwa sababu Serikali inarejesha 51%; lakini mbali ya 51% kuna fedha za *TDL* asilimia tisa ambazo huwa zinagawanywa kwenye taasisi hizi; asilimia sita na asilimia tatu inakwenda kwenye Mfuko wa Wanyamapori. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niendelee na unilindie dakika ambazo amezitumia Mheshimiwa Getere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za *TDL* ambazo ni asilimia sita. Jukumu la fedha hizi za *TDL* ni kuendeleza utalii, lakini kuendeleza mambo ya miundombinu kwenye hifadhi, kufanya utafiti kwenye hifadhi zetu na kuhakikisha kwamba watalii wanakuja kwa wingi. Kwa hiyo, fedha hizi nazo zina akaunti yake ambayo imefunguliwa Benki Kuu. Taasisi hizi zina uhuru wa kwenda kuzichukua zile fedha na kuzitumia kadri ambavyo wameweka bajeti yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalizo kwenye fedha hizo za *TDL;* kwa sababu kuna ile 51% ambayo inarudishwa na Serikali, lakini kuna *extra money* ya fedha za *TDL* ambazo zinakwenda kwenye taasisi. Basi ningeomba Serikali iangalie utaratibu wa mgawanyo wa fedha hizi za *TDL,* kwa sababu kunakuwa na mchanganyiko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ile 51% kuna fedha za maendeleo, lakini pia kuna hiyo asilimia tisa ambapo asilimia sita inakwenda kwenye *TDL* na asilimia tatu kwenye Mfuko wa Wanyamapori. Hizi zote ni mifuko, pesa hizi za *TDL* ninataka niunge mkono Taarifa ya Kamati yangu ya Ardhi, Maliasili na Utalii iliyosomwa hapa Bungeni ya kusema kwamba, fedha za *TDL* zinatakiwa ziwekewe utaratibu ambao unatakiwa ueleweke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini maana yake? Maana yake ni kwamba fedha hizo zinatakiwa zikaboreshe miundombinu na vilevile zikafanye utafiti; lakini *suppose* zile pesa huko zinakokwenda kwenye taasisi zisipokwenda kufanya hiyo kazi nani ana-*monitor* hizi fedha? Kwa sababu zinagawiwa Wizarani, hazigawiwi Serikalini, wanazi-*monitor* wenyewe, wanakusanya wenyewe, wanaweka kwenye akaunti ambayo ipo Benki Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niendelee kwenye suala la malazi nchini kwetu Tanzania. Kwenye Nchi yetu ya Tanzania siyo kwamba sisi tulikuwa maskini wa uhaba wa hoteli. Sisi tulikuwa na hoteli ambazo zilikuwa chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii, lakini Serikali kupitia urekebishaji wa sheria mwaka 1992,

ilibinafsisha hoteli 23 Nchini Tanzania ambazo zilikuwa kwenye mbuga zetu za wanyawa ambazo ni hoteli pamoja na *lodge*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maliasili na Utalii ilikuwa inamiliki hoteli 17; ilikuwa na hoteli kule Manyara, Ngorongoro na Serengeti; lakini Wizara hii ilizibinafsisha hoteli hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho ninataka kukisema hapa, tuliwahi kumwita *TR* kwenye Kamati mwaka 2021 tarehe 24 Januari, tukamwita tena *TR* tarehe 21 Januari, 2025, lakini tukaleta Azimio la Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba Serikali izichukue hizi hoteli, izirudishe kwa sababu sasa hivi tuna uhitaji wa hoteli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu wale waliobinafsishiwa hizo hoteli wamevunja masharti ya ubinafsishaji, ipo haja ya Serikali kuzirudisha hizo hoteli. Ninatoa mfano kidogo, *Embassy Hotel* Dar es Salaam, haijawahi kufanya kazi toka mwaka 2008. Hoteli zimekufa, nyingine popo wanazaliana. Ipo haja ya kuzirudisha hizi hoteli Serikalini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba dakika moja au nusu dakika niweze kuchangia *TTB*…

**MWENYEKITI:** Malizia, sawa malizia dakika mbili.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninaomba kuongelea suala la *TTB* ambayo ni Bodi ya Utalii nchini Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi hii ukisoma kwenye Taarifa ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, ndiyo ambayo imepewa pesa nyingi (shilingi 20,000,000,000), angalia Taarifa ukurasa wa 126 kama sijakosea. Ipo haja ya hii Bodi kuangalia *human capacity* na kuangalia *technical how*, nikiwa na maana iajiri watu wenye uzoefu wa biashara, lakini pia iajiri watu ambao watacheza na hii mifumo. *TTB* ina mfumo unaitwa kutangaza, imejenga mfumo pale Dar es Salaam wa kutangaza utalii kidijiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo huo tulienda kuutembelea mwaka 2023, mpaka ninavyoongea hapa mfumo una hadithi nyingi. Nimesoma kwenye Taarifa ya Mheshimiwa Waziri anasema unataka sijui kuongezewa pesa ili uweze kufanya kazi. Ninaona haja ya *TTB* kuongezewa wataalamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza tukawa tunajilaumu kwamba *TTB* haifanyi kazi, *TTB* sijui imefanya nini, lakini ninaona pia kwamba *TTB* inahitaji kusaidiwa kuongeza wataalamu ambao watacheza na kompyuta kuitangaza nchi yetu nje ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanajenga mfumo mwingine ambao unaitwa '*Travel Companion*' ambao utakuwa unazungumza kwa lugha 56 za dunia hii ili mtalii atakapokuwa yuko huko, watatumia akili mnemba ili mtalii atakapokuwa yuko huko aweze kuji-*book* mwenyewe kwenye hoteli, usafiri na jinsi ya kuja nchini kwetu Tanzania.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako mzuri. Ninamwita sasa Mheshimiwa Neto Paul Kapalata, Mheshimiwa Dkt. Regina Malima atafuata, Mheshimiwa Patrick Adkin Mwalunenge ajiandae.

**MHE. NETO P. KAPALATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii kuweza kuchangia jioni ya leo. Awali ya yote, ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kuweza kupata fursa hii kupitia wewe katika Kiti ulichokalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hoja yangu, nitakuwa na utangulizi wa hoja na nitaenda kujikita kwenye Maliasili na Utalii peke yake na halafu nitajielekeza kutoa ushauri katika hizo sekta mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mbunge wa Jimbo la Nzega Vijijini, ninatokana na Mkoa wa Tabora. Mkoa wa Tabora tuna kilio kikubwa cha maeneo ya kufanyia shughuli za maendeleo ya makazi pamoja na uchumi. Mkoa wa Tabora una mapori ya Hifadhi ya Misitu pamoja na wanyamapori yasiyopungua 12. Mkoa wa Tabora una eneo la kilometa za mraba 76,000 na ushee, lakini katika Mkoa wa Tabora, Hifadhi za Misitu na Wanyamapori ni 46% ya hayo mapori yaliyotengwa na 22% ni kwa ajili ya wanyamapori tu peke yake ambao ni tofauti na misitu ambayo ina wanyamapori wengi ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inabakia 32% kwa ajili ya maendeleo ya makazi pamoja na shughuli za uchumi. Sasa ninaomba kujielekeza kwenye hoja yangu. Kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye amekuwa ni kiongozi mbunifu, sisi wote tumeona na tunaenda kuelekea kwenye Dira ya 2050, ninataka kusema, katika Jimbo langu la Nzega Vijijini na Jimbo la Uyui na Jimbo la Bukene lina-*host* hifadhi inaitwa *Ilomero Hills* ambapo kuna Kijiji kikubwa cha Ipala ambacho siyo kijiji rasmi. Sisi tulikaa na Serikali ya Kijiji kutathmini kwa sababu sisi wengi wetu ni wakulima na wafugaji katika eneo hilo mkabala na hifadhi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *square kilometer* 405 ambazo ni za hifadhi hiyo. Katika Uongozi wa Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, wale Waheshimiwa Mawaziri Nane walikuja kujionea adha ya kukosa maeneo ya maendeleo ya makazi na shughuli za kiuchumi, wakaridhia likatengwa eneo la hekta 1,667.8 kwa ajili ya maendeleo ya makazi na shughuli za kiuchumi katika hifadhi yenye kilometa za mraba 405 ambalo hilo ni eneo dogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kukudokeza kitu. Pale katika Kijiji cha Ipala ambacho kiko katika Hifadhi ya Ilomero kipindi cha ukoloni kulikuwa kuna kampuni inaitwa *Tanganyika Packers* ikifanya shughuli za kilimo. Sasa hivi kampuni hiyo haifanyi shughuli za kilimo ambalo ni eneo hilo hilo mkabala na hifadhi. Kijiji cha Ipala ambacho siyo rasmi kiko ndani ya Kijiji cha Ugembe II. Kijiji cha Ugembe II ukienda hicho Kitongoji cha Ipala ambacho siyo rasmi, kina kaya zaidi ya 1,300 na wananchi zaidi ya 12,000

ambao wengi wao wote ni wapiga kura wa Chama Cha Mapinduzi, hakuna mpiga kura wa chama cha upinzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kusema kitu, kutokana na ukweli kwamba eneo lile shughuli kubwa ni kilimo na ufugaji na pamekuwa na uhaba wa mapori ambayo wanyama hao wanakula nyasi tu hawali miti, lile eneo limejaa. Kwa kuthibitisha kwamba pale *there is life*, hata *TRC* imekwenda kujenga kituo cha stesheni katika hiyo hiyo Hifadhi ya Ipala ikiwa ni kana kwamba imekubali *there is life*, wale watu wa pale lazima waendelee na shughuli za kiuchumi na kuendeleza makazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hoja hiyo, tulikaa na uongozi wa Tarafa na uongozi wa Wlilaya ya Nzega, tukaanza kurasimu kwa nini wananchi hawa wasikae raha mustarehe, wasipate bugudha pamoja na askari wanaokuja wa *TSF* na kadha wa kadha? Tukakubaliana tutakwenda TAMISEMI kutengeneza kurasimu Kijiji cha Ipala kwa sababu kuna vitongoji vinne visivyo rasmi, vina uongozi usio rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitongoji hivyo kwa majina ni Masoradi, Sengerema, Ipala Kati pamoja na Sengerema Juu. Sasa ninataka kusema kitu, ushauri wangu katika Wizara upande wa misitu, sheria zilizotenga mapori miaka ile, huenda zikawa zimepitwa na wakati kwa sababu watu wameongezeka, ubunifu umeongezeka na watu wamekuwa wabunifu wa kuangalia shughuli za uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Wizara ya Maliasili na zile Wizara wanaotoka wale Waheshimiwa Mawaziri Nane, zikae chini kupitia sheria ya kutenga mapori ya hifadhi kama ni misitu na wanyamapori kulingana na *population* iliyokuwa ili sisi sasa tuweze kuratibu vizuri kutokana na mahitaji ya makazi na ya kiuchumi katika Nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninakwenda kwenye hoja ya utalii. Jamani Serengeti ni *one of the seven wonders of the world,* lakini Sekta ya Utalii imeingiliwa, tunaua *a safari feel*, tunaua *a feeling of you being in a wildlife area*. Sasa hivi ongezeko la hoteli za kitalii, wanyama wanaletwa wakiwa wamefungiwa kwenye

*cage,* watu wanajaribu kumshika hadi simba sharubu, wanyama wanalishwa chakula ambacho siyo *wild* ambacho siyo *ecological* kwa wale wanyama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba kupendekeza, hizi hoteli na vitu vya namna hiyo tujaribu kuzi-*regulate* ili sisi na ile Serengeti yetu na hifadhi nyingine, watu waje wa-*experience a safari feel,* waende kule kwenye maeneo kwenye mbuga waone wanyama, tuzuie kufanya *artificial safaris.* Watalii watashindwa kwenda mbugani, wataishia hotelini, watarudi *airport*, watapanda ndege wataondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi huwa siyo msemaji sana. Ninaomba Mheshimiwa Waziri akisimama hapo, atupe mpangokazi wake kutokana na ushauri wangu jinsi ya kukaa na zile Wizara nyingine nane ku-*regulate* kutokana na *population* hizi hifadhi ambazo ni nyingi kwa sababu sisi wananchi wa Mkoa wa Tabora kweli tunajiona tuna mkosi, *(twadye dagwa)*. Ninataka kusema, tena aje na mpangokazi wa hiyo *artificial safari* ikomeshwe, kuwe kuna *a real safari* kwenda kwenye *wild reserve areas*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa fursa na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kabla hujakaa Mheshimiwa hebu, maana ya hilo neno ni nini? Kwa ajili ya *Hansard*, hilo la kilugha ulilotaja.

**MHE. NETO P. KAPALATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, aah! Tunaonekana tunadharaulika; ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya tunaendelea. Nilimwita Mheshimiwa Dkt. Regina Christopher Malima, atafuatiwa na Mheshimiwa Patrick Adkin Mwalunenge na Mheshimiwa Naibu Waziri ajiandae.

**MHE. DKT. REGINA C. MALIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ninamshukuru Mungu kwa kutupatia uhai na sote kuwa mahali hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua fursa hii ya pekee sana kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo ameendelea ku-*promote* sekta ya utalii nchini na haya yote yanajidhihirisha wazi katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050. Pia, tumeliona hili katika Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. Kama hii haitoshi tumeendelea kuliona kwa Mheshimiwa Rais wakati akilihutubia Bunge la Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, Bunge la Kumi na Tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ameendelea kutoa mkazo na msisitizo katika kupanua wigo wa utalii kwa kuangalia uwekezaji katika maeneo tofauti tofauti mbali na yale ambayo yamekuwa yakizoeleka kama Serengeti, Mlima Kilimanjaro na hata Zanzibar. Nitaelezea baadaye kwa nini ninasema hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua fursa hii pia kuipongeza Wizara yetu. Ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri Dkt. Ashatu Kijaji, lakini Naibu Waziri - Mheshimiwa Chande, Katibu Mkuu na timu yote ya wataalamu wa Wizara hii kwa kutengeneza *document* ambayo ni nzuri na ambayo imeendelea kutupatia mwelekeo kama Watanzania kujua tuko wapi katika sekta ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapongeza sana, mimi kama Mheshimiwa Mbunge wa Kundi la Vyuo na Vyuo Vikuu, nimeona dhamira ya dhati ya Serikali yetu ku-*support* wanafunzi ambao wako katika hifadhi ambao wanaishi katika mazingira ya hifadhi. Takribani wanafunzi 978 katika ngazi ya sekondari, vyuo na vyuo vikuu watanufaika na uwezeshaji ambao utafanywa na Serikali yetu. Hongereni sana kwa kutambua hili kwa sababu tunapowekeza katika elimu, tunawekeza katika maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kupanua wigo wa uwekezaji na utalii nchini siyo suala dogo. Tumeendelea kuona Wizara ikija sasa na *Tourism Master Plan* ya Taifa letu. Ni jambo zuri sana na ninasema tu ya kwamba tulikuwa tumechelewa, lakini bado ni jambo jema ambalo litatoa mwanga wa namna ambavyo Sekta ya Utalii inaenda kuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *Tourism Master Plan* ninasema tu ya kwamba ni mpango wa muda mrefu. Ninaomba Wizara, kutoka katika hii *master plan,* andaeni *Tourism Strategic Plan* kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge tofauti tofauti wameongea hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vivutio vingi katika Taifa letu, bila kuwa na *strategic plan* ambayo ita-*identify* maeneo haya, hakika tutakuwa hatuna vipaumbele ni nini ambacho tunapaswa kufanya. Kwa hiyo, ninawaomba waandae *strategic plan* ya miaka mitano yenye malengo maalum, namna ya kuyafikia, nani atafanya nini kwa sababu wana taasisi nyingi zilizopo chini ya Wizara yao. Lakini pia tujue muda wa utekelezaji, bajeti na hata kuandaa *KPI's (Key Performance Indicators)* kwa ajili ya tathmini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivutio ni vingi na leo ninaomba kuongea kitu cha pekee ambacho wengi yumkini hawajawahi kusikia. Tumeona namna ambavyo Wizara inaenda sasa katika utalii katika Ziwa Victoria. Kuna kisiwa kinaitwa Kisiwa cha Ukerewe, *Ukerewe Island* ni kisiwa cha pekee sana. Waheshimiwa Wabunge wasiofahamu kisiwa hiki kina visiwa 38 ndani yake kitu ambacho duniani hakipo. Kwa nini kisiwe ni miongoni mwa vivutio katika Taifa hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kisiwa hiki ni cha kwanza barani Afrika kwa ukubwa, Kisiwa hiki ni cha tano duniani kwa ukubwa, lakini kina fukwe zenye mchanga tofauti tofauti nikiwa na maana ya kwamba mchanga wenye rangi tofauti tukiwa na fukwe za Ukara, Rubya, Hamiebe na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kisiwa hiki, ukiwa katika maeneo 10 tofauti unapata kuona namna ambavyo jua linazama (kwa lugha nyingine tunaita *sunset)* kitu ambacho ni *very rare* katika maeneo mengi katika Tanzania na dunia, lakini hii unaipata katika Kisiwa cha cha Ukerewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni katika kisiwa cha Ukerewe tuna mwandishi wa kwanza kutunga kitabu, kuandika na kuchapisha. Hii ni historia ya pekee ambayo haiko katika mikoa mingine katika Taifa letu na huyu siyo mwingine alikuwa anaitwa Anicet Kiteleza.

Kisiwa hiki kina jiwe linalocheza, wakitaka waone wafike wataliona namna linavyocheza. Pia, kina *ginnery* ya kwanza ya pamba kujengwa katika Tanganyika mwaka 1906 na ikazinduliwa na *Sir* Edward mwaka 1920.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *ginnery* hii bado ipo, zile *machines* bado zipo. Kwa nini Wizara isiende kuangalia *richness* ya utamaduni na historia ambayo iko katika kisiwa hiki? Kisiwa hiki kina ghorofa ya kwanza kujengwa na Chifu mwafrika kama hamfahamu. Chifu huyu huyu ndiye wa kwanza Tanzania au Tanganyika wakati ule kununua gari. Nani alinunua gari katika Tanzania hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea kuwatia moyo Waheshimiwa Wabunge, wafike katika kisiwa hiki chenye utajiri wa kutosha. Ni katika Kisiwa hiki tunapata Padri wa kwanza wa Kanisa Katoliki ambaye ndiye alipata upadrisho. Katika Kisiwa hiki tuna Shule ya Sekondari Kagunguli, shule ambayo amesoma mama Maria Nyerere, mke wa Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Kisiwa hiki mama yetu Getrude Mongela amesoma katika shule hii. Kama mnavyofahamu mama Getrude Mongela amekuwa ni Rais wa Kwanza wa Bunge la Afrika, lakini pia alishiriki au ali-*participate* kwenye ule mkutano wa Beijing. Kisiwa kimejaa vivutio vingi, vingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anapofanya mahitimisho ya Wizara yake, ninaomba kisiwa hiki badala ya kusubiri kutafuta namna ambavyo tunataka kupata maeneo mengine ya uwekezaji, Ukerewe iwe ni miongoni mwa vivutio katika Taifa letu kwa sababu imejaa na imesheheni mambo ambayo hayapatikani katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninasoma *criteria* ili eneo lipate kuwa katika Vivutio vya Taifa ni nini? Mkiangalia ile *Tourism Act* nafikiri ni ya tatu mtaona pale lazima kuwe na *uniqueness;* sasa eneo gani lina *uniqueness* siyo lingine ni Kisiwa cha Ukerewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapomalizia ninaomba kama tunatafuta Zanzibar katika kisiwa, katika Ziwa Victoria, Zanzibar inapatikana katika Kisiwa cha Ukerewe ndani ya Ziwa Victoria. Kisiwa hiki kikiwekezwa vizuri kitakuwa ni Zanzibar ndani ya Ziwa Victoria, njooni muone dhahabu iliyofichika ndani ya Ziwa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itasaidia kuongeza Uchumi na ajira kwa vijana na wanawake. Baada ya kusema hayo niwaombe njooni Kisiwa cha Ukerewe, kisiwa cha maajabu ndani ya Taifa letu ahsante sana ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Malima, ahsante sana kwa mchango wako, nimwite sasa Mheshimiwa Patrick Adkin Mwalunenge aweze kutoa mchango wake.

**MHE. PATRICK A. MWALUNENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa fursa hii nami niweze kuchangia kutoa mawazo yangu kwenye hii Wizara ya Maliasili na Utalii. Awali ya yote namshukuru sana Mheshimiwa Rais na kumpongeza kwa kazi kubwa aliyoifanya, mageuzi makubwa aliyoyafanya kwenye Wizara hii na yeye mwenyewe kuwa mstari wa mbele kwa kucheza ile filamu ya *Royal Tour.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio tumeyaona watalii wameongezeka sana kwa hiyo, tumpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa ile Filamu yake na naamini viongozi sasa wa maliasili na utalii waige huo mfano wa Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili natokea Mbeya, Jimbo la Mbeya Mjini kwa maana ya Mkoa wa Mbeya. Mkoa wa Mbeya una vivutio vingi sana vya utalii kwa Nyanda za Juu Kusini lakini haujatangazwa ipasavyo. Kwa hiyo, ninamuomba Waziri atakapokuja ku-*wind up* atueleze mipango aliyonayo ni nini kitaweza kufanyika kutusaidia kuutangaza Mkoa wa Mbeya ili kuweza kutangaza vivutio vilivyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo Milima ya Kawetele, zile kona za Mkoa ukipanda pale juu unaiona Mbeya yote na ni panauwanda mzuri sana, hali ya hewa nzuri ambapo naamini watu wanaweza wakatoka sehemu mbalimbali na kwenda

kufurahia pale na kuingiza pesa. Mapato mengi yataingia kwenye Mkoa wetu wa Mbeya na watu wataenda kufurahia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunayo mito inayotiririsha maji tunayo madaraja, tunayo mabwawa lakini pia tuna Maziwa madogo madogo ambayo yapo juu ya milima. Mengine yanatoa maji ya moto kama vile Bwawa la Ngosi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia siyo hiyo tu Mkoa wa Mbeya, tunayo milima mingi ambayo pia ni kivutio sana na tunaweza tukafanya Mkoa wa Mbeya ukawa ni kitovu cha utalii kwa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri mtusaidie Mkoa wa Arusha wamefanikiwa sana kwa sababu wana vitu vingi wenzetu. Kwanza wana hizo Mbuga lakini na sisi mbuga pia zipo, ukienda kule Kitulo utaiona mbuga iko kule, kuna wanyama, kuna vipepeo, kuna maua ambayo hayapatikani maeneo yote lakini kama nilivyosema hatujatangaza vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninamuomba Mheshimiwa Waziri atusaidie Mkoa wetu wa Mbeya ili tuweze kuutangaza Mkoa wa Mbeya. Moja tujenge, mtusaidie kupata Ukumbi wa Mikutano ya Kimataifa ili tuweze kuvutia wageni wengi pale, kwa sababu tunao Uwanja wa Ndege wa Kimataifa, ambapo ndege za aina yoyote zinaweza zikatua pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sasa hivi tupate ukumbi pale na hoteli ya nyota tano ili tuweze kuwavutia wageni waweze kufanyia mikutano na mwisho wa siku watakwenda kwenye maeneo yetu ya vivutio vya utalii na mapato yataweza kuongeza kwa kiasi kikubwa na watu wetu kwenye Mkoa wa Mbeya watapata ajira nyingi na kuweza kusaidia vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine naongea na watu wa *TFS,* nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri. *TFS* kwenye Mkoa wangu wa Mbeya hasa Jimbo la Mbeya Mjini walikuwa kama ni mwiba pale Mbeya, walikuwa wanakamata vijana wetu wale wanaobeba mikaa na walizuia pikipiki karibu 120 za vijana wetu ambao wao walikuwa wanabeba mikaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikawa najiuliza mimi hawa vijana mpaka wanasomba hiyo mikaa, mkaa ili uweze kuchomwa unakatwa kwanza mti, unaparuliwa linajengwa tanuri na tanuri likichomwa moto maana yake moshi unafuka. Maana yake hata *TFS* wanaweza wakaona kwamba kuna eneo fulani mkaa unachomwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hiyo *process* yote hawaendi kumkamata yule anayechoma mkaa mle ndani, wanakuja kumkamata kijana anayebeba mkaa barabarani. Tena wanakimbizwa kwa namna ya ukatili inafikia hatua pikipiki inaanguka yule kijana anaweza akaumia na kwenda hospitali wanamnyang'anya ile pikipiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile pikipiki unakuta ni ya mkataba, ameingia mkataba na mwalimu ambaye amekopa pikipiki. Pikipiki inanyang'anywa na mwisho wa siku sheria inavyosema ni kwamba pikipiki itaifishwe iuzwe sasa mazingira kama hayo mimi nasema hii Sheria ya *TFS* tumeitunga ni sisi Wabunge au imetungwa na nani? Na sisi kama ni Wabunge ndiyo tunawawakilisha wananchi nadhani sasa imekuwa ni kero hiyo sheria kwa wananchi ambao ni wananchi wetu vijijini kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashauri *TFS* badilikeni na kupitia Waziri *TFS* wabadilike wafanye, wabadilike waanze kufikiria kibiashara zaidi. Ile Misitu ya Kabwetere iliyozunguka vijiji nimesikia wachangiaji wenzangu wamezungumza hapa huwa inatolewa mitaji kwa ajili ya kutengeneza mizinga ya nyuki basi na sisi badala ya vijana kuwakamata wabeba mkaa waletewe hizo fedha ili waweze kufuga nyuki kwenye ile Misitu ya Kawetele na maeneo mengine ya Mkoa wa Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni nini? Wale vijana wao wenyewe ndiyo wataulinda msitu sasa badala ya kuchoma mkaa. Kwa sababu watapata pesa kupitia asali na watajenga viwanda vidogo vidogo kwa ajili ya kuchakata ile asali na mwisho wa siku kupeleka kwenye soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lazima tuwe na majawabu mbadala badala ya kila siku kukamata. Niliwauliza watu wa *TFS* kwa hiyo, mkishakamata hizi pikipiki zinazobeba mkaa ina maana ni kwamba uchomaji wa mkaa ndiyo umekwisha? Lakini unakuta mkaa bado uko mjini unauzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namshukuru sana Naibu Waziri alinisaidia kuongea na watu wa TFS japo lilikuwa ni jambo gumu sana. Niliingilia kati mimi mwenyewe wale vijana walirudishiwa pikipiki lakini wale vijana wako zaidi ya 300 kwenye kile kikundi chao wapo tayari kubadilika wasibebe tena mkaa wapewe fedha ili wakafuge nyuki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana wapewe mizinga ya kufuga nyuki ili mwisho wa siku wao ndiyo walinzi wa msitu na wako tayari kuulinda msitu usikatwe miti ili wao wakafuge nyuki na kupata asali mle ndani. Kwa hiyo hilo Mheshimiwa Waziri naliomba wakati una *wind up* utuambie ni jinsi gani vijana wetu wale wako zaidi ya 300 na wameishajiunga kikundi ili waweze kupata hizo fedha wakafuge nyuki na mwisho wa siku wao ndiyo watakuwa walinzi namba moja kuhakikisha kwamba ule msitu haukatwi miti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili upande wa *TANAPA* na *TAWA*, hapa namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu watu wa *TANAPA* mimi nashangaa kule Mbarali kuna eneo limetengwa kwa ajili ya hifadhi eneo Oevu, wananchi walilima mpunga heka karibu 4,000 mpunga umeshaota bado miezi miwili kuvuna maana yake ulikuwa unataka uvunwe huu mwezi wa tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa *TANAPA* wamechukua magari yao na madumu ya madawa yale ya kuua nyasi wamepakia kwenye hiyo gari. Maana yake wanatumia fedha za Serikali kwenda kuuchoma ule mpunga wa wananchi zaidi ya heka 4,000. Sasa mimi nashindwa kuelewa hii sheria tunaitunga ni kwa ajili ya wananchi au ni kwa ajili ya nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii sheria siyo inatuchonganisha sisi, mnamchonganisha Mheshimiwa Rais na wananchi wale mabwana na nilimpigia Naibu Waziri yuko pale ndugu yangu

Chande walikataa walikaidi amri ya Waziri, Naibu Waziri. Lakini hadi Mkuu wa Wilaya ameongea nao pale wamekaidi *TANAPA* hao mpaka nilipochukua jukumu la kumpigia Waziri Mkuu ndiyo akawazuia msichome chakula cha wananchi lakini sababu ni moja; ni kweli hakuna mtu anayetaka wananchi walime kwenye maeneo oevu maeneo ya hifadhi hakuna anayepinga hilo jambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini leo hii ukienda Mbarali maeneo mengi yamejaa maji yana mafuriko na ule mpunga ukikaa miezi mitatu tu wanauvuna siyo zao la kudumu lakini mtu anaenda kuchoma mpunga kesho kutwa wale watu wakishapata njaa maana yake Serikali inatakiwa tena ipeleke chakula cha msaada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, yule mtu amekopa mbolea, amekopa fedha lakini amepewa mbolea ya ruzuku ya Serikali ambayo inatoa fedha kulipia ruzuku ya mbolea lakini mtu wa *TANAPA* haya yote yeye hayafikirii anaenda kuchoma mpunga. Hili jambo naliomba maelezo kwa kweli Mheshimiwa Waziri anapokuja atueleze hawa watu wa *TANAPA* wanapata wapi hicho kiburi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mkuu wa Wilaya anashindwa kuzuia, Naibu Waziri ameshindwa kuzuia, nikachukua jukumu mimi la kumpigia Waziri Mkuu tena ilikuwa Jumapili, naomba tumpigie makofi sana Waziri Mkuu. Jumapili ndiyo akachukua jukumu la kuwapigia wale watu ndiyo wakazuia kwenda kuchoma mpunga wa watu lakini heka 18 walikuwa wameshaziunguza tayari na hiyo dawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale ni wananchi wadogo, maskini wenye heka moja moja maana yake hawana chakula na kama walikopa fedha za riba maana yake hawawezi kurudisha. Sasa tumekaa hapa sisi kwa ajili ya nini kwenye hili Bunge hapa ndani? Kama wananchi tunaowaongoza tunawafanyia vitu vya kikatili vya aina hiyo. Kama ni sheria tumeitunga sisi basi ije hapa tuirekebishe kwa sababu kama ni sheria inaenda kuwaonea watu ina faida gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine *TFS* hawa hawa pia mwananchi analima mahindi wanamwangalia, mahindi yamekua mpaka imefika kuvuna baadaye anakwenda kwenye *operation* anakwenda kufyeka, kesho kutwa yule mwananchi akipata njaa kwenye Serikali hii hii ya Mheshimiwa Dkt. Samia anaenda kumpa chakula, unashindwa nini kumvumilia huyo mtu akavuna hayo mahindi halafu kesho ukaenda kumwelimisha ili asiende tena kuendelea kulima hayo mahindi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mambo tuyaelewe vizuri hawa watu kweli hizi sheria tumezitengeneza sisi wenyewe. Kama ni sheria ambazo zinaenda kuwakandamiza watu wetu ambao ni wananchi wa chini zije hapa tuzirekebishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini elimu ni muhimu sana kwa wananchi wetu hakuna anayekataa kulinda mazingira au watu wakalime kwenye hifadhi lakini lazima elimu itumike ili kuwaelimisha wale watu hawakatai lakini lazima tuwaelimishe. Lakini kwenda kukamata mazao siyo jambo la kiubinadamu na wala haliruhusu kabisa mazingira, hata uungwana tu siyo jambo jema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako. Waheshimiwa kabla hatujaendelea, sijamwita Naibu Waziri tuwatambue baadhi ya Wageni. Tuna mgeni wa Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Mbunge na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii huyu ni ndugu Mariamu Juma ambaye ni mke wake karibu sana, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya Mafunzo, hawa ni Wanafunzi 100 na Walimu saba kutoka Shule ya Awali na Msingi Canossa ya Jijini Dar es Salaam nadhani wamekaa kwenye Ukumbi wetu mkubwa kule tunawakaribisha sana nikiamini kwamba wananisikia. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea nimwite sasa Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Naibu Waziri, Maliasili na Utalii baada ya hapo Mtoa Hoja ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa fursa hii naomba nianze kwa jina la Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema mwenye kurehemu. Tumshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye tangu Ijumaa mpaka leo tunajadili jambo letu hili muhimu sana, adhimu na adimu sana. Namuomba Mwenyezi Mungu atujalie tumalize kwa salama na amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ninaomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mbeba maono ya Watanzania, mama mwenye ujasiri, uweledi na ufanisi mkubwa sana wa kutafsiri sera kwa vitendo. Hata hivyo, niendelee kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba unipe fursa hii kushukuru Kamati yetu ya Ardhi, Maliasili na Utalii, Wajumbe wote wakiongozwa na Mwenyekiti wetu ndugu yangu Mheshimiwa Mnzava nawapongeza sana kwa kazi nzuri, maelekezo yao na maoni yao na nikuhakikishie kwamba ushauri, maelekezo na maoni yao tunaenda kuyafanyia kazi kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwapongeze na kuwashukuru sana Wabunge wote ambao wamechangia kwa maandishi, kwa kuongea na wale ambao hawakuchangia. Kwani michango yao imekuwa ni mizuri sana, ninataka niwaahidi Waheshimiwa Wabunge mbele yako kwamba maoni yao na ushauri wao tumeyapokea na tunaenda kufanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru sana na nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii kwa namna anavyofanya kazi mashirikiano yake, maelekezo yake kwetu sisi na kufanya kazi kwa ufanisi na nimuombe tu Mheshimiwa Waziri hizi ndogo ndogo ambazo zinatokea na hata makubwa lawama na nini azipokee kwa sababu Waswahili wanasema “mwenda hidimani ndiye mkosa” *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukishakuwa wewe unafanya kazi lazima utalaumiwa kama umekaa tu hatokei mtu wa wa kukulaumu mfano anaweza kusema hata Mheshimiwa kwamba pale Chama alikuwa asitoe pasi apige shuti. Lakini mwenzako yeye yuko pale anavuja jasho lakini lazima alaumiwe kwa sababu yuko hidimani. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nikutie moyo kwamba kwa kuwa wewe ni mwenda hidimani lazima zitatokea zile lawama na maelekezo pengine kwa hisia tofauti tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niwapongeze sana Wataalam wetu wa Wizara yetu ya Maliasili na Utalii kwa kazi nzuri, mashirikiano mazuri na kwa kweli wanafanya kazi kwa uweledi na ufanisi mkubwa sana wakiongozwa na Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Makamishna na Watendaji wote, naomba niwaombee Mungu nao awabariki sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba uniruhusu niishukuru sana familia yangu, niwashukuru wake zangu, nishukuru watoto wangu kwa kazi nzuri ninavyokaa nao na namna wanavyonishauri vizuri. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nielekee kwenye hoja niseme tu kwamba hoja zile na maoni ambayo yametolewa na Kamati tumeyapokea na tunaenda kuyafanyia kazi. Lakini hatutoongea sana mimi na Mheshimiwa Waziri wangu kwa sababu yaliyotoka ni maelekezo kinachotakiwa ni kwenda kuyafanyia kazi na Wahenga wanasema "ada ya mja hunena muungwana ni vitendo" sisi tunaenda kutenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo hoja ambayo imetolewa na Waheshimiwa Wabunge kwamba tuhakikishe wale ambao waliathirika kifuta jasho na kifuta machozi kimetoka kwa wakati. Serikali imechukua hatua kubwa zaidi ya kuanzisha mfumo unaotambulika kwa jina la *payees*, mfumo huu umerahisisha sana kupokea na kuchakata taarifa mbalimbali na umeiwezesha Serikali kulipa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fikiria kutoka Januari mpaka Mei 17 Serikali imeishalipa bilioni 9.58 ukilinganisha na mwaka uliopita kipindi kama hicho tumelipa bilioni 5.6. Kwa hiyo, nikusema

kwamba mfumo huu unatusaidia sana sana katika kuboresha na kufanya utekelezaji wa ulipaji wa kifuta jasho na machozi kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru sana sana Mheshimiwa Rais kwa maelekezo yake na kutupa ridhaa kuanzisha mfumo huu ambao unatuletea tija kubwa sana kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tu nataka nitoe wito kwa Wakurugenzi wetu kule kwenye halmashauri zetu wawe wanajitahidi kuleta taarifa kwa wakati kuingiza kwenye Mfumo ili tusiwaweke wale watu ambao wamepata athari, ikifika tu taarifa kwa wakati basi na Serikali inaenda kulipa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ni maelekezo ambayo hata dini zipo dini zinasema kwamba ni vyema sana kumlipa mtu kazi yake aliyofanya au aliyokutananayo kabla jasho lake halijakauka kwenye mwili wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niende hoja ya pili ambayo imezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi sana akiwemo ndugu yangu Mheshimiwa Kampala na wengine kuhusu changamoto na kadhia ambazo wanazipata huko chini kwa baadhi ya watendaji wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninawatia moyo watendaji wetu, wanafanya kazi nzuri sana ya kiuzalendo, tena wanajitoa kwa maslahi ya Taifa letu katika uhifadhi. Ni lazima kwenye kiunga huwezi kukosa pofu. Inawezekana wako ambao wamekiuka maadili. Ninaomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, Serikali haitokuwa na muhali kwa yeyote yule ambaye anaenda kinyume na sheria, anaenda kinyume na taratibu na kanuni zilizowekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nikwambie Pamoja na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, ushahidi wa hilo ndani ya mwaka huu wa fedha 2025/2026, Serikali imechukua hatua kubwa sana za kuwasimamisha watendaji 17, akiwemo hata wa ndugu yangu Mheshimiwa Asenga kule Kilombero. Yule amesimamishwa.

Kwa hiyo, ninamtia moyo Mheshimiwa Asenga na Waheshimiwa wengine ambao wamepata kadhia kama hiyo, Serikali imechukua hatua. Wamesimamishwa kazi na wako wengine wameshushwa vyeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninakuahidi, Serikali haitomvumilia mtu yeyote yule. Kwa sababu ni lazima, kwa kuwa moja ambalo nilikuwa ninataka niliseme, sisi bahati nzuri tulioko mbele mimi na Mheshimiwa Waziri, wote ni wenye duka halafu ni wauza duka, tunauza wenyewe. Sijui umenisoma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, duka ni la kwetu na tunauza wenyewe. Maana yake sisi ni viongozi katika chama, hatutokuwa tayari kuona mwananchi yeyote huko anapata shida. Kwa hiyo, ninataka kuwahakikishia watu wetu hawa tunawapa maelekezo ya siku zote kwamba kama *slogan* (falsafa) ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inavyosema fanyeni kazi na utu; 'Kazi na Utu'. Kwa hiyo, tunasema fanya kazi na utu, uishi vyema na watu, uwatambue watu, uthamini utu wa mtu ili na wewe uwe mtu mbele za watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo imezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge ni suala la malikale. Ni kweli, ninaomba nikiri kwamba yako baadhi ya maeneo hatujayafikia, lakini Serikali imefanya kazi kubwa sana sana ya kupitia vivutio vya malikale katika sehemu mbalimbali, lakini ni kweli baadhi ya nyingine hatujazifikia. Serikali imeandaa timu maalum ambayo inapita kila sehemu kufanya utafiti. Hata ya ndugu yangu Rashid Mtima, wataalamu wameshafika na tukimaliza tu hili, tutapeleka watalaamu wengine ili kusudi kwenda kubaini vivutio hivyo ambavyo Wabunge wamevitaja vya malikale na vyenyewe vitaingizwa kwenye *list*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Regina dada yangu, ni kweli ameizungumzia Ukerewe vizuri na ameainisha vizuri, lakini ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Dkt. Regina kwamba, sisi Serikali, wataalamu wetu pamoja na yeye tutaambatana kwenda kuona maeneo hayo na ninamhakikishia na Ukerewe nayo itaingia kwenye *list* kama ni kivutio cha utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa muda hautoshi na mimi hapa kazi yangu leo ni kuweka tu nyalio, Mheshimiwa Waziri yupo atakuja kujibu hoja kwa ukamilifu mkubwa sana na kwa wakati mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Nimwite sasa mtoa hoja, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji, Waziri wa Maliasili na Utalii.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote kabisa, nitoe shukrani kwa Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kuniwezesha leo hii kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kwa ajili ya kuhitimisha hoja tuliyoiwasilisha tarehe 15 ya Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa jinsi ambavyo mmeendesha mjadala wa siku hizi mbili kuhusu hoja ambayo tuliweka mezani. Ninawashukuru sana, tukiongozwa na Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru pia Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa jinsi ambavyo wametoa maoni yao kwenye hoja yetu hii. Tunawashukuru sana, mimi na wenzangu ndani ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana kwa dhati ya moyo wangu Mheshimiwa Timotheo Mnzava, Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, pamoja na Wajumbe wa Kamati yetu kwa kazi kubwa waliyoifanya kwenye kujadili utekelezaji wa Bajeti ya Wizara yetu kwa mwaka wa fedha 2025/2026, lakini pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenyekiti wetu wa Kamati ni mtu muungwana sana tangu nilipomfahamu ametuongoza vyema sana, kuanzia kwenye Kamati, lakini hata alipowasilisha taarifa

yake, aliiwasilisha vyema kabisa. Mheshimiwa Mwenyekiti, mdogo wangu Mheshimiwa Mnzava ninamshukuru sana kwa kazi yake njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yetu imepokea na kuchambua maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge 63 na kati ya hawa Wabunge 51 wamechangia kwa kuzungumza na Wabunge 12 wamechangia kwa maandishi. Ninawashukuru sana. Hii inaonesha utayari wao kwenye kuona maliasili zetu zinaendelea kuchangia vyema kwenye uchumi wa Taifa letu, lakini watu wetu pia waendelee kunufaika na maliasili zetu. Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kulithibitishia Bunge lako Tukufu kwamba, maoni na ushauri wa Kamati pamoja na hoja zote za Waheshimiwa Wabunge waliochangia kama ambavyo nimewataja, tutayazingatia katika utekelezaji wa mpango na bajeti yetu kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Hoja na ushauri huo wa Waheshimiwa Wabunge umejikita katika maeneo mbalimbali kama ambavyo tumesikia kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi, nikisema nijibu moja moja tutafika kesho asubuhi. Kwa hiyo, ninaomba Wabunge wanikubalie tuseme machache na mengine kama nilivyoahidi tutayazingatia kwenye utekelezaji wa mpango na bajeti, lakini tutajibu pia kwa maandishi. Kama ambavyo nimetangulia kumpongeza Mwenyekiti wetu wa Kamati, nina uhakika atasimamia vyema kuona hoja zote zikiijibiwa. Ninaomba hilo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya ombi hilo, ninaomba sasa niseme machache kati ya mengi ambayo mmeyasema. Kwanza kabisa na mimi niungane nanyi Waheshimiwa Wabunge kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi yake kubwa aliyoifanya kwenye kuitangaza nchi yetu na vivutio vyake. Pale alipotoka ofisini akaenda kuigiza Filamu ya *The Royal Tour* pamoja na *Amazing Tanzania*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu tunazozitaja za kuongezeka kwa idadi ya watalii ni majibu ya kazi yake nzuri aliyoifanya. Hatujawahi kupata watalii wengi kutoka Nchi ya China kama ambavyo tumepata mwaka huu na wanaendelea kuja. Ni kwa sababu ya ile Filamu ya *Amazing Tanzania* ambayo tulienda kuizindua kwenye miji miwili tu na sasa tuna mpango mkubwa wa kuipeleka kwenye miji mingine ndani ya Nchi ya China pamoja na majirani zake ambao wanaongea Kichina. Nina uhakika tutaendelea kuwapokea wengi zaidi. Hivyo, ninawashukuru kwa pongezi hizi kwa Mheshimiwa Rais wetu na sisi tunawaahidi hatutomwangusha Mheshimiwa Rais wetu kwenye eneo hili la utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hoja ambayo imeguswa karibu na kila Mbunge aliyesimama na kusema tukitanguliwa na ushauri wa Kamati yetu, ilikuwa ni hoja ya kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu. Nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri amesema wapi tupo na mimi nitaongezea kule tunakoelekea. Yeye amesema vyema kwa mapenzi mema ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana Waheshimiwa Wabunge walitupitishia bajeti ya shilingi bilioni 12.3 kwa ajili ya kulipa kifuta jasho na kifuta machozi. Mheshimiwa Naibu Waziri amesema tayari tumeshalipa shilingi 9,000,000,000 na Ijumaa iliyopita tumepokea shilingi 2,000,000,000 nyingine ili tuendelee kulipa. Ninashukuru Mheshimiwa Mbunge mmoja alisema anaona wananchi wake sasa wako kimya. Tumeanza kulipa kuanzia *weekend*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru pia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameelekeza tuongezewe shilingi 6,000,000,000, ili wale wote ambao hawakulipwa kuanzia mwaka 2023, wote walipwe au angalau tufike 70% ya kuwashika mkono ndugu zetu walioathirika na wanyamapori wakali na waharibifu. Dhamira ya Serikali yetu ni njema. Ninaomba sana sana waliridhie hilo, tutaendelea kuwalipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfumo alioutaja Mheshimiwa Naibu Waziri nina uhakika ilikuwa inatuchukua muda mrefu sana.

Watumishi wa Wizara watoke wasafiri kwenda kwenye halmashauri zote nchini, ilikuwa kazi kubwa na fedha nyingine zilikuwa zinaishia njiani. Kwa mfumo sasa tunalipa moja kwa moja kwenye akaunti ya mwananchi aliyeathirika au kwenye namba yake ya simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwenu Waheshimiwa Wabunge, zipo akaunti tulizopokea ni akaunti mfu, malipo yanagoma kwenda. Ninawaomba sana kwenye majimbo yetu tuwashajihishe wananchi wetu ili wanapoandika akaunti iwe ni akaunti ambayo inafanya kazi.  Lipo tatizo la pili, nalo ni namba za simu. Namba ya simu iliyoandikwa na jina la anayelipwa hazifanani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua kulikuwa na michezo huko nyuma na lengo la Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan lilikuwa ni kuhakikisha kila mwananchi anapata haki yake. Kwa hiyo, tumepata pia changamoto ya namba ya simu ambayo imeletwa haifanani na jina la anayetakiwa kulipwa, mfumo unagoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninawaomba pia tuwaambie wapigakura wetu, wananchi wetu, kupitia mfumo huu hakuna kupokeleana. Kila mmoja aandike namba yake ya simu na aweze kulipwa yeye mwenyewe. Hiyo pia ni changamoto nyingine tuliyokumbana nayo. Unakuta mwananchi anasema wenzangu wote wamelipwa kasoro mimi. Ninamwambia ninaomba nitumie namba yako ya simu uliyotuletea ili tukulipe. Unaikuta ile namba haifanani. Kwa hiyo, ninaomba sana hilo pia tuwafikishie wananchi wetu ili tufanikiwe kuwafikishia kifuta jasho chao pamoja na kifuta machozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge kwenye eneo hili wameenda mbele na wakasema, ni muhimu tuwe na utafiti wa kina nini kimetokea? Kwa nini wanyamapori wakali na waharibifu wanatoka wanakuja kwenye maeneo ya wananchi? Tulifanya utafiti na matokeo niliyasema kwenye hotuba yangu ya bajeti, lakini nimeona kiu ya Waheshimiwa Wabunge, ninawaahidi. Tunayo taasisi yetu mahususi kwa kazi hiyo, *TAWIRI*. watakwenda kufanya tena utafiti mwingine tuendelee kujiridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tukisema kama ni idadi ya tembo imeongezeka, sensa tuliyoikamilisha mwaka jana inagoma. Mwaka 1961 wakati tunapata uhuru tulikuwa na tembo 300,000 kwenye nchi yetu. Leo kwa sensa iliyofanyika mwaka jana tuna tembo 66,000. Kwa hiyo, kitaalamu inagoma kusema wameongezeka. Utafiti ule pia ukatuambia ni kweli idadi ya watu wa mwaka 1961 na wa leo hatufanani, tumeongezeka. Katika kuongezeka kwetu tumejikuta tunasogelea hifadhi zetu na hapa nimepokea maombi mengi ya Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mmoja akisimama anasema tunaomba tukatiwe pale kwenye hifadhi, tukatiwe pale kwenye msitu. Kule kukatiwakatiwa tunawasogelea hao wanyama. Kwa hiyo, tutajikuta sisi tumesogea na hatimaye kuwaonjesha matikiti maji, kwa sababu tutakuwa tumewasogelea na kwenda kulima, wamekula matikiti maji wameyapenda. Baadaye wataanza kuyatafuta mpaka ndani. Kule kwangu Kondoa pale Mkungunero tembo alienda kuchukua tikiti maji uani. Kikubwa Mwenyezi Mungu ametuambia kwenye vitabu vyote Vitukufu, amemuumba mwanadamu katika mfano wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa wale Waislamu Mwenyezi Mungu akasema: "*Laqad khalaqnal insaana fii ahsani taqweem.*" Amemuumba mwanadamu katika umbo lililo bora akiwa na uwezo wa kutafakari. Maana yake nini? Sisi tunaweza kumwona tembo anakuja tukakimbia. Sisi tunaweza kujua tumemsogelea tukasema turudi nyuma. Tembo yeye amependa tikiti maji atalitafuta popote, kwa sababu hana tafakuri, hana utashi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania sasa tuko zaidi ya 60,000,000. Ni kweli, ndiyo maana Waheshimiwa Wabunge wanasema tufanye utafiti wa kina na hapa utafiti wa kina ni wa njia za kuwazuia ili wasiingie kwenye maeneo yetu. Kwa sababu, *finding* ya kwanza tumeshaiona. Wao wako pungufu sisi tuko wengi, bado tunahitaji maeneo zaidi. Sasa, ni kutafuta mbinu za kisayansi, nini tunafanya ili waweze kubaki kule hifadhini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndipo tulipokuja na mkakati wetu mpya wa miaka 10 wa jinsi ya kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu, ambao tunaanza kuutekeleza mwaka huu wa fedha

2026/2027 mpaka mwaka wa fedha 2036/2037. Kwenye mkakati huu ambao bado ni rasimu, sisi, Wizara, tutaufikisha kwenye Kamati yetu ya Ardhi, Maliasili na Utalii, ili tuweze kuona yale ambayo yamependekezwa na wataalamu wetu, pamoja na wadau wetu na wawakilishi wa wananchi, wanasema nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaufikisha, tutajadili kwa pamoja na ninaamini kabla hatujamaliza Bunge hili la Bajeti tutauleta kwa Waheshimiwa Wabunge pia, ili tuwasilishe mwanzo mpaka mwisho. Miongoni mwa machache ambayo yametokana na utafiti uliofanyika, yaliyomo ndani ya mkakati huu, moja ndiyo hili ambalo Waheshimiwa Wabunge wamesema. Tuongeze kasi ya kuweka *fence* za umeme kwenye hifadhi zetu, ili kuwazuia hao wanyama wakali na waharibifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameendelea kutupatia fedha na tumeleta leo bajeti yetu Bungeni, tunawaomba watupitishie, ili tukaendeleze kazi hii ambayo tumeianza. Ni wazi kwa sababu ya bajeti hatuwezi kuweka kwenye hifadhi zote 21, mapori yote sitini na ngapi! hatuwezi ndugu zangu, lazima twende hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo lipo kwenye mkakati huu ni kwamba, tuweze kupata *helicopter* nne kwenye taasisi zetu zote za uhifadhi, ili kuwe na urahisi wa kuwarejesha nyuma hao wanyama wakali na waharibifu pale wanaposogelea maeneo ya wananchi wetu. Ndani ya kipindi hiki cha utekelezaji wa mkakati tunaona hili linawezekana na kupitia bajeti yetu hii tunayoitekeleza. Bajeti hii tunayoileta leo tunawaomba watupitishie, tumeleta *helicopter* mbili, ili *TANAPA* wawe na ya kwao na Ngorongoro wawe na ya kwao; tuliona tuanze nazo hizo, ili tuweze kuwarejesha wanyamapori hao wakali na waharibifu mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajuaje kwamba wamesogea, ili tuwarejeshe? Tumeanza kuwafunga mikanda tembo na mwaka huu, ninalishukuru sana Bunge lako, limeturuhusu kununua mikanda 50, lakini kwa dhamira njema ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha Watanzania wanakuwa salama,

tumenunua mikanda 76 na tumewafunga tembo viongozi 76. Hawa viongozi ndiyo watakuwa wanatuwezesha kwa sababu tuna uwezo wa kuwa-*monitor* kwamba sasa amesogea, amekaribia kijiji fulani, ili tuweze kuwarejesha tutakapokuwa tumepata *helicopter* zetu. Kwa sasa tunatumia ndege nyuki ambazo kwa mwaka huu tumenunua 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sasa hivi tunatumia hizo teknolojia, ndivyo utafiti ambao tumefanya unatuambia. Tofauti na hapo tutadanganyana. Kwa hiyo, katika eneo hili tutafanya hayo, lakini tumeanza pia kuchimba mabwawa, ikiwa sababu ya hawa wanyamapori kutoka kule hifadhini ni maji, waweze kuyapata kulekule hifadhini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeanza kuchimba mabwawa na katika bajeti yetu ya mwaka huu tumelileta pia, tunawaomba watupitishie, ili tuendelee kuchimba hayo mabwawa, wanyama wetu wanywe maji kulekule, wasitoke kuja kuyatafuta huku nje. Eneo hili ni la mkakati, kama nilivyosema, tutaleta rasimu yetu kwenye semina ya Wabunge wote ili tuijadili kwa pamoja na tukubaliane tutoke kama Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo ninatamani niseme na limechangiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi, ni eneo la utendaji kazi wa Bodi yetu ya Utalii *(TTB)*. Waheshimiwa Wabunge wengi wamesema, Kamati yetu imesema na niruhusu niendelee kumshukuru Mwenyekiti wetu wa Kamati, amefanya jitihada kadhaa ya kutuita sisi Wizara pamoja na bodi; hapa nieleweke, maana yake hii ni Bodi ya Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenyekiti kaiita Bodi ya Utalii, pamoja na sisi Wizara, tuje kwenye Kamati yake. Tumekaa, tumesema kwa pamoja na wao wamesema vyema. Ni wazi tunakiri, ipo changamoto na tumeanza kuifanyia kazi. Kamati yetu imependekeza tuangalie muundo na Waheshimiwa Wabunge wamependekeza tuangalie muundo; tuna Muundo wa Mwaka 2022, Muundo ambao umeanza kufanya kazi Mwaka 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaonekana ipo haja ya kuendelea kuuangalia mfumo na muundo huu wa Bodi yetu ya Utalii, lakini

kamati yetu ikaenda mbele ikasema inawezekana isiwe muundo, ikawa ni watendaji waliopo ndani ya Bodi yetu ya Utalii. Waheshimiwa Wabunge wamesema kwa uchungu sana na hata sisi Wizara tunaliona. Niwaombe sana; moja, waniruhusu nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa sababu aliridhia kuuangalia huo muundo, kama ambavyo Bunge lilielekeza. Pili, Mheshimiwa Rais wetu ametupatia fedha kwenye Bodi yetu ya Taifa ya Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kwamba hakuna fedha, hapana! Hili ninaomba niseme, Wabunge wamesema na niwape mifano michache. Tukiangalia kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Bodi yetu ya Taifa ya Utalii iliidhinishiwa jumla ya shilingi 23,238,461,059. Mpaka tunamaliza mwaka Bodi ya Taifa ya Utalii ilikuwa imepokea shilingi 16,893,119,975 sawa na 92% ya fedha zilizopitishwa na Bunge. Tukienda mwaka huu wa fedha, ambapo Waheshimiwa Wabunge wamesema, walituidhinishia, Bodi ya Taifa ya Utalii ilipewa shilingi 33,267,764,600 na mpaka Aprili hii, Bodi ya Taifa ya Utalii tumewapa 77.2% shilingi bilioni ishirini na moja na milioni mia tano na kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwenye hoja ya Wabunge ya kuwaongezea fedha, sisi tumeanza kupata shida, kama Wizara. Sisi, kama Wizara, tumeanza kufanyia kazi, kama nilivyosema, pamoja na Kamati yetu ya Kisekta. Tunakwenda mbele zaidi tujue tatizo ni nini, ili utangazaji wa utalii uweze kuleta tija. Ninaomba niwaahidi, watuamini, tutarekebisha utendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitamani niseme hili la Bodi ya Taifa ya Utalii na niwashukuru kwamba wanatuamini. Watuachie tulifanyie kazi, ninaamini ndani ya kipindi cha miezi sita tutakuwa tunaongea lugha nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuja hoja ambayo kidogo nimeona kama imechafua Taifa. Ninaomba nikiri wazi imetuumiza sisi, hoja imesema kwamba, idadi ya watalii 5,935,000 tunaosema siyo sahihi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba, hili ni Taifa letu sote. Kwa kazi kubwa aliyoifanya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu

Hassan, watalii tunaowaona wanaingia kwenye viwanja vyetu vya ndege, watalii tunaowaona hifadhini. Hili sisi limetuumiza, tukasema, hapana, ni muhimu nalo hili nikalisema; Waheshimiwa Wabunge, takwimu hizi siyo za kwetu ni za Shirika la Utalii Duniani la Umoja wa Mataifa ambao wameweka vigezo vyao. Wao wanakusanya kila mwezi na mwisho wa mwaka wanatupatia, kwa mwaka huu Tanzania mmekuwa wangapi na watalii wenu waliowatembelea ni kiasi hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hoja ile aliyosema ni muhimu tukawa na *Gen' Z* wengi humu ndani, nilisema pia, kwenye hotuba yangu. Taifa letu limekuwa la tatu kama Taifa ambalo watalii wakija wanatumia fedha nyingi kuliko mataifa mengine. Kwa hiyo, tunajua wakija wana-*spend* kiasi gani, tunajua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili ninasema Serikali yetu hutumia viwango na Miongozo ya Kimataifa inayotambuliwa na Shirika la Utalii Duniani la Umoja wa Mataifa ambalo Mwongozo wake ni wa Mwaka 2008. Kwa hiyo, hatuhesabu tu; amekuja mchuuzi wa nyanya, tunasema ni mtalii, hapana! Hao wachuuzi wa nyanya nitamwachia mdogo wangu Mheshimiwa Judith Kapinga, Waziri wa Biashara, hao wa kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuna vigezo vya kuja na namba hii. Ninapenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali yetu itaendelea kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Utalii kwenye kazi hii na hii yote ni kumwambia Mheshimiwa Dkt. Samia, ahsante kwa kazi nzuri uliyoifanya ya kuinua sekta yetu ya utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo ambalo limesemewa kwa nguvu pia na Waheshimiwa Wabunge wengi ni *AFCON* 2027. Waheshimiwa Wabunge, ninapenda kuwaambia na wamesema vyema sana, *AFCON* 2027 ni *multisectoral*, ni ya sekta zote, siyo ya Maliasili na Utalii peke yake. Ninamwona kaka yangu Mheshimiwa Ulega yumo kwenye barabara na anafanya kazi nzuri, ninamwona Waziri wa Nishati yumo anafanya kazi nzuri, ninawaona Mawaziri wote wanafanya kazi nzuri kwenye

maandalizi, tukiratibiwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu, ambaye naye anaifanya kazi yake vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwetu sisi, nimesema kwenye hotuba yangu na ninaomba niwahakikishie; sisi kama Wizara, tunao mkakati mahususi wa jinsi gani tunaiendea *AFCON* 2027. Jambo la kwanza ni mafunzo kwa wadau wetu wote wa utalii, ambapo tumeanza na waongoza utalii zaidi ya 2,000, tumemaliza kuwapa mafunzo hayo. Tuna mpango wa kuendelea na wadau wengine wote kwa makundi yao, ambao wanahusika na Sekta ya Utalii, zikiwemo hoteli, ikiwemo hoja ile waliyosema ya kugeuza nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku moja nilikuwa pale Arusha, Mji wa Utalii, wakaniambia hapa Arusha na pale Moshi kuna nyumba nyingi za wastaafu ambao watoto wao wameondoka, wanatamani wazigeuze kuwa *Airbnb*. Sisi huo mkakati tunao, wiki ijayo tutakuwa na mkutano na akina mama wa Arusha ambao wanatamani nyumba zao ziwe *Airbnb* ili sisi tuwape viwango vya Kimataifa, tunataka nini kwa ajili ya wageni wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utapokea watalii, utawapeleka Serengeti, pamechoka, miundombinu imechoka! Tumesema tunawekeza kwenye miundombinu yetu, kwenye hifadhi zetu zote na ninamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipopata tatizo la mvua kubwa Serengeti, nilienda kumwomba; mama ninaomba shilingi bilioni 8.1, kanipa zote ndani ya siku mbili, sasa hivi Serengeti wanatengeneza barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetamani tuiunganishe reli yetu ya kisasa na Hifadhi yetu ya Taifa ya Mikumi. Mheshimiwa Rais katupatia shilingi 4,000,000,000, tunajenga geti la kisasa pale Kilosa, ili wakiteremka pale Mikumi, pale Kilosa, iwe ni dakika 20 wameingia hifadhini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka kufanya nini? Tunachotaka kukifanya ni siku za mapumziko, ambazo hakuna mechi, tuwachukue mashabiki wote waliopo Dar es Salaam,

mashabiki waliopo Zanzibar, tuwaweke kwenye *SGR* wateremke Kilosa, waingie Mikumi. Ndiyo mkakati tulionao, pamoja na mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kengele ya pili imegonga. Ninaomba nikushukuru sana kwa hili, lakini ninaomba niwaahidi hatupo tayari kuona tunapoteza fursa ya *AFCON*. Sisi, Wizara ya Maliasili na Utalii tupo tayari, mimi na wenzangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea nina tangazo. Ninaomba niwatangazie kwamba, Waheshimiwa Wabunge wote na watumishi wa Ofisi ya Bunge mnakumbushwa kwamba, Wataalamu wa Afya kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na *Ocean Road* wanaendelea na kliniki maalum ya uchunguzi wa magonjwa ya kike, kiume, njia ya mkojo, afya ya moyo, *cancer*, mifupa, magonjwa ya ajali, masikio, pua na koo, pamoja na huduma za ushauri wa afya. Shughuli hii itahitimishwa tarehe 22 Mei. Waheshimiwa Wabunge mnaombwa na mnakaribishwa sana kupata huduma hiyo.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

*Hapa Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**FUNGU 69 - WIZARA YA MALIASILI NA UTALII**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*…………*Sh*. 7,252,929,550

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Kifungu hiki kina mshahara wa Waziri, nina majina hapa takribani tisa na ninajua wengine watarudia yale yale, ninawaomba na ninawakumbusha Kanuni yetu ni kuhusu sera, ukizungumzia tembo siyo tembo wa Ilala peke yake, ninawaomba sana.

Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Mheshimiwa Bahati Ndingo.

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Ninahitaji nipate ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Tunafahamu kwa mujibu wa Katiba yetu, Ibara ya 24…

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, samahani, ninaongeza muda mpaka hapo tutakapomaliza shughuli yetu. Endelea.

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na ninaomba ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Tunafahamu kwa mujibu wa Katiba yetu Ibara ya 24 inaeleza utaratibu wa namna ambavyo Serikali itatoa maeneo kutoka kwa wananchi, lakini tunazo sheria ambazo Bunge lako Tukufu lilishazitunga. Tunayo Sheria ya Ardhi, Namba 4 ya mwaka 1999, lakini pia tunayo Sheria ya Ardhi ya Vijiji Namba 5 ya mwaka 1999 na sheria nyinginezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na utaratibu wa maeneo ambayo tunatambua nchi yetu hifadhi zinatanuliwa kwenda kwenye maeneo ya wananchi, lakini kumekuwa na

utaratibu ambao *TANAPA* wamekuwa wakiufanya kuwazuia wananchi kutumia maeneo yale hasa maeneo ya uzalishaji. Hali hiyo kwanza imepelekea wananchi kuwa maskini na benki kufilisiwa. Tukiangalia Katavi wanayo changamoto hiyo, Arumeru wanayo changamoto hiyo, Mbarali wanayo changamoto hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninahitaji kauli ya Mheshimiwa Waziri kuhusiana na kuwakataza watu kutumia maeneo kabla ya Serikali kuwalipa fidia, hususan maeneo ya uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba majibu na ninakusudia kushika shilingi yake nisipopata majibu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na ninampongeza Mheshimiwa Bahati kwa hoja hii aliyoizungumzia wakati anachangia, nilitamani nijibu wakati ninatoa ufafanuzi, muda ukawa mchache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kumekuwa na maeneo mbalimbali ya nchi yetu yanaonekana aidha kwa sababu ya uhitaji wa ikolojia zetu au kutokana na mabadiliko ya tabianchi. Nikichukulia mfano wa eneo lile la Mbarali, lilichukuliwa baada ya kuonekana Mto Ruaha ulikuwa unaathirika kwa kiwango kikubwa, hivyo Serikali ikaona ipo sababu ya kuyalinda na kuyahifadhi maeneo yale kwa ajili ya usalama wa Mto Ruaha ambao unaleta maji kwenye mabwawa yetu matatu yanayozalisha umeme hapa nchini, likiwemo Bwawa la Mwalimu Nyerere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Serikali kuona hivyo na maelekezo kutolewa Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia *TANAPA* ilipewa jukumu la kuyalinda maeneo yale. Wizara ya Ardhi ilipewa jukumu la kufanya tathmini ili Serikali iweze kulipa. Tunakiri Wizara ya Ardhi haijamaliza tathmini na itakapomaliza tathmini tu, basi tutaweza kulipa fedha hizo kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo hayo yanachukuliwa kwa sababu ya maslahi mapana ya Taifa letu. Tunasubiri tu tumalize

tathmini hiyo na tuweze kuwalipa wananchi wetu. Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bahati.

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni takribani miaka mitatu, sasa tunaenda wa nne, wananchi walikuwa wanatumia mashamba yale kama *collateral* kwenye benki. Hivi ninavyokwambia wananchi wale nyumba zao zimeuzwa, mali zao zimeuzwa. Sasa kama Serikali haikujipanga kuwalipa wananchi wale kwa nini wasisimamishwe kufanya uzalishaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati upande mwingine wa ng'ambo, wananchi wameelekezwa kwamba walime umbali fulani wa mto na hawatumii maji ya Mto Ruaha, wanatumia wakati wa mvua peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni adha kubwa kwa sababu linagusa maisha ya watu. Wananchi wa Mbarali wanatia huruma, shamba lile la hekta zaidi ya 10,000 limepoteza ajira za watu zaidi ya 100,000 wanaolima pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitoe hoja, Waheshimiwa Wabunge wenzangu waniunge mkono, jambo hili ni gumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja.

*(Hoja ilitolewa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Upande wa Serikali msimame vilevile. Mheshimiwa Taska, Mheshimiwa Waitara, Mheshimiwa Tabasam, Mheshimiwa Ulega na Mheshimiwa Reuben. Tunaanza na Mheshimiwa Mnzava.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Bahati na ukisoma taarifa ya Kamati jambo hili tumelieleza kwa kina na kama alivyosema Mheshimiwa Bahati jambo hili lipo kwenye maeneo mengi na ni kweli jambo hili ni la muda mrefu. Sheria zinaeleza utaratibu wa kufuata ukisoma Sheria ya Utwaaji wa Ardhi kwa maana ya *Land Acquisition Act*. Ni kweli wananchi wanaathirika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili tumelifanyia kazi kwenye Bunge lako kwa muda mrefu, ninachokielewa na ninachokiona hapa, jambo hili linahusisha Wizara zaidi ya moja, kwa maana ya Wizara ya Maliasili, lakini wenzetu wa Wizara ya Ardhi ambayo ndiyo ina jukumu la kisheria la kufanya uthamini, pia Wizara ya Fedha ambayo pia ina jukumu la kutoa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwa sababu wale wananchi wanaolima kwenye baadhi ya maeneo likiwemo lile la Mbarali si kwa maeneo yote, wana wataalam ambao wanaweza kuwasaidia kuwaelewesha namna gani ya kufanya hii kazi, tuombe Serikali namna ya kulegeza masharti kwenye jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Bahati na kwa maelekezo yako, kwa sababu Bunge letu bado lipo na kwa sasa jambo hili linahusisha Wizara nyingi. Ninadhani tunayo haja sasa ya kukaa vikao mahsusi kwa ajili ya jambo hili ili tukutanishe Wizara zote zinazohusika na jambo hili tuone namna ya kufikia mwisho wa jambo hili ili wananchi wasiendelee kupata shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaweza kuona namna ya kuwapa angalau ahueni hawa wananchi kwa kipindi hiki, lakini kwa maelekezo ya Bunge lako tutamwomba Mheshimiwa Bahati mwishoni amrudishie Mheshimiwa Waziri shilingi ili bajeti ipite lakini kwa maelekezo ya Bunge lako na kwa maelekezo ya Kiti chako Mwenyekiti tukae vikao mahsusi vya kamati yako pamoja na Wizara hizi tutafute mwarobaini wa jambo hili ili wananchi

wasiendelee kuteseka, waendelee kunufaika na kufurahia kuwa kwenye nchi yao. Ninakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kabudi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, URATIBU NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ambayo imewasilishwa hapa ni hoja muhimu sana. Kwanza inagusa maisha ya Watanzania, pili inagusa uhai na uchumi wa Watanzania. Bwawa la Mtera, Bwawa la Kidatu, Bwawa la Mwalimu Nyerere yanategemea hayo maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina wajibu wa kuhakikisha wananchi wake wanaendelea na maisha yao na wanapata riziki yao, Serikali ina wajibu na Taifa lina wajibu wa kuhakikisha lina umeme na uzalishaji unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tunalichukua suala hili, Ofisi ya Waziri Mkuu ndiyo yenye jukumu la uratibu. Tutaita Wizara zote za kisekta zinazohusika kesho ili kulijadili jambo hili na kulipatia mwafaka na mwafaka wa kwanza mkubwa ni kukamilisha tathmini ili wananchi walipwe fidia kama ambavyo Mbunge wa Mbarali ameeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatoa *commitment* kwamba sasa italichukua jambo hilo na kuhakikisha tathmini imekamilika ili wananchi walipwe fidia. Pia itachukua hatua nyingine ambazo zitashauriwa kitaalamu zitakazohakikisha wananchi wanaendelea kupata riziki yao bila kuhatarisha usalama wa nishati katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaahidi kulifanya jambo hilo kwa haraka na sisi kama Serikali tutakutana wote tunaohusika, yaani sekta zote zinazohusika na jambo hili, kuanzia kesho ili tupate ufumbuzi wa haraka. Wizara ya Ardhi tutahakikisha tunakamilisha tathmini haraka iwezekanavyo kwa mtindo wa dharura ili wananchi hawa waweze kupata fidia yao na waweze kuendelea na maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndiyo *commitment* ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bahati.

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na ninaiamini Serikali yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni aidha watafikia hatua ya kuongea na wale watu au kufanya hata tathmini ndogo kwa sababu ni eneo kubwa, tathmini ndogo ya maeneo yale ambayo ni *sensitive* kwa Taifa au kuwapa maeneo mbadala ya kufanyia kazi zao. Isifike msimu mwingine wa kilimo kabla hatujapata majibu haya, niombe sana wamekaa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, ninasubiri hiyo kesho tupate hayo mambo, tuweze kulimaliza jambo hili ili wananchi wapate haki yao, kama alivyosema Mheshimiwa Profesa Kabudi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musa Godfrey Mbuga.

**MHE. MUSA G. MBUGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kwa suala la wafugaji ambao ng'ombe, mbuzi na punda wao walikamatwa katika maeneo mbalimbali wakataifishwa na baadaye wakaenda mahakamani na wakashinda kesi na kuamriwa warudishiwe mifugo yao, walipwe na hivyo vitu vyao vyote. Suala hili limekuwa la muda mrefu lilipelekwa Wizara ya Katiba na Sheria, likarudishwa Wizara ya Mifugo, likarudishwa tena Wizara ya Maliasili na baadaye likapelekwa Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka sasa nipate ufafanuzi wa Serikali na Wizara ni lini hawa wafugaji watalipwa ng'ombe wao au mifugo yao kwa ujumla. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru na nimpongeze sana Mheshimiwa Musa Godfrey Mbuga amefuatilia sana hili jambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hali hiyo ilitokea na tayari tathmini imekamilika ambapo wananchi hawa wanastahili

kulipwa shilingi bilioni 2.926, tayari tumeshakaa na Wizara ya Fedha na walitoa *commitment* kwamba, kabla mwaka huu wa fedha haujakwisha, pesa hizi zitakuwa zimetoka.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mbuga, kwa sababu hukutoa hoja ya shilingi, hoja yako imeshajibiwa tunaendelea na Mheshimiwa Kampala.

**MHE. THOMAS K. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakubaliana wote hakuna mtu ambaye anapinga uhifadhi kwenye nchi yetu na hakuna mtu anayepinga au kubeza sheria za uhifadhi kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli ulio wazi kwamba kumekuwa na changamoto na unyanyasaji mkubwa wa askari wa *TAWA* na *TFS* kwa wananchi kwenye mikoa mingi kwenye nchi yetu. Mikoa iliyoathirika sana ni Mikoa ya Katavi, Kigoma, Tabora, Simiyu na maeneo mengine. Mfano mdogo kwenye Jimbo la Katavi, Waziri Mkuu alifanya ziara na akatoa maelekezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelekezo aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri Mkuu alipofika kwenye ziara alikutana na hoja ya wananchi ambao kwa bahati mbaya waliingia kwenye eneo ambalo linadhaniwa ni la hifadhi na wakalima. Wale wananchi walilima mazao, sasa kinachotuchanganya sisi ni kwamba wameingia, askari wa *TAWA* wanawaona, wanaweka mbolea askari wa *TAWA* na *TFS* wanawaona. Imefika saa mazao yamekomaa kila wanapotaka kwenda kuingia kuvuna askari wa *TAWA* na *TFS* wanawazuia. Matokeo yake, katika maeneo yote kumetokea mabishano makubwa na malumbano makubwa, hali hiyo imepelekea mpaka vifo kutokea katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba *commitment* ya Serikali na kauli ya Serikali. Nini kauli ya Serikali kwa wananchi wale ambao tayari mazao yamekomaa na wale wananchi ambao kama ambavyo ameongea Mbunge aliyepita, mifugo yao imekamatwa na haijulikani ilipo? Nisipopata majibu ya kuridhisha nitakamata shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba majibu ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana. Jambo hili pia tumelifanyia kazi sana na Mheshimiwa Thomas Kampala na tukakubaliana na tayari tumeshatoa maelekezo kwamba, wananchi ambao mazao yao yamekomaa waachiwe wavune.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo ndiyo tutajua na sisi tunashughulika vipi na watumishi wetu wachache ambao wanatenda ndivyo sivyo kwenye eneo hilo. Kwa hiyo, tumeshakubaliana na tumetoa maelekezo wananchi waachiwe waweze kuvuna mazao yao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kampala.

**MHE. THOMAS K. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kushukuru na sikuwa na mashaka na Mheshimiwa Waziri. Kinachonipa mashaka ni namna ambavyo viongozi wanatoa maelekezo na hayatiliwi maanani. Mfano mdogo ni katika Jimbo la Kasulu Vijijini hivi tunavyoongea alikwenda Mbunge na Naibu Waziri wa Ardhi…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kampala kipindi hiki unatakiwa ueleze kama unataka kuendelea kushika shilingi au umeridhika na maelezo ya Mheshimiwa Waziri?

**MHE. THOMAS K. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti… *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Naona umeridhika!

**MHE. THOMAS K. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaridhika na maelezo ya Waziri, kwa sababu hivi tunavyoongea Kasulu watu wanazuiliwa kuvuna mazao yao. Ninaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu wenye matatizo kama yangu waniunge mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja tujadili jambo hili.

**MWENYEKITI:** Hoja haijaungwa mkono, mmechelewa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi. Kumekuwa na migogoro mikubwa hasa ya mipaka ya ardhi kati ya wananchi na Hifadhi ya Taifa ya Serengeti *TANAPA* na *SENAPA*. Jambo hili limeleta madhara makubwa sana kwa wananchi na limechukua muda mrefu kiasi kwamba kila wakati ni mgongano kati ya wananchi na askari wa hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nipate maelezo ya Mheshimiwa Waziri ya mkakati alionao wa kuhakikisha kwamba mipaka hii kati ya wananchi na hifadhi zetu inaangaliwa katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija Mkoa wa Mara, nenda pale Simiyu, amesema mwenzangu pia Katavi na maeneo mengine ni jambo kubwa ambalo kila wakati wa bajeti watu wanalalamikia mahusiano yaliyopo kati ya wananchi wetu na hifadhi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Waziri atueleze mpango alionao wa kupitia mipaka hii. Kuna maeneo mengine wameweka *beacon* za mipaka bila kushirikisha wananchi wenyewe, kuna maeneo mengine wamesogeza mipaka kuja kwa wananchi. Kwa hiyo kuna mambo ambayo kwa kweli tungetamani kama Taifa tujadili na Waziri atueleze amejipangaje ili jambo hili lifikie mwisho na watu waishi kwa amani na kuleta mahusiano ya kuunga mkono utalii kupitia sekta ya maliasili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisiporidhika na majibu nitaomba Wabunge wenzangu waniunge mkono na wawahi kusimama kabla ya muda ili tujadili jambo hili kwa maslahi mapana, wasichelewechelewe kuniunga mkono. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Serikali kwa dhamira njema ilitoa maelekezo kwa Mawaziri Nane wa Kisekta na wakazunguka nchi nzima na 98% ya migogoro katika vijiji 975 vilivyokuwa na kero hii imetatuliwa na mipaka imewekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ambayo imebaki mbele na ambayo tunaihitimisha ni sasa Serikali kwenda kutoa tamko la mipaka hiyo kwenye maeneo yote ya vijiji 975 ambayo kazi imekamilika. Nimwombe sana Mheshimiwa Waitara atupe nafasi tuweze kukamilisha kazi hii ambayo imebaki kidogo, kwa sababu kazi kubwa tayari imeshafanyika nchi nzima kwenye vijiji vyetu vyote 975.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikia Mheshimiwa Waziri. Ni kweli Mawaziri walikwenda tangu mwaka 2021 wakazunguka baadhi ya maeneo, nami nilikuwepo, kwa hali halisi kwa Tarime Vijijini kuna vijiji saba katika Kata ya Kwihancha, Gorong'a na Nyanungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi halikuwa shirikishi, kwa sababu watu wa hifadhi na Mawaziri ndiyo walikuwa wanaelekezana *beacon*, kulikuwa na ubishi mkubwa katika maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili siyo jambo la afya kwa Taifa letu, kila mwaka wa bajeti kujadili migogoro iliyopo pale. Kwa nini inakuwa ngumu kuwasikiliza wananchi? Unakuja kuniambia mimi sikai hapa, lakini nimezaliwa hapa, ulitokea ubishi, pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Waziri ambaye ninamwamini sana, ninatamani jambo hili tupate *test* ya maeneo mbalimbali halafu aone ukubwa wa shida hii, namna ambavyo inasumbua wananchi wale na katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba jambo hili lijadiliwe, tupate maelezo kwa maeneo mbalimbali, aone uzito wake, ninatamani kama yeye angekuwa ni Mbunge wa eneo kama Tarime Vijijini, maeneo ambayo watu hawakushirikishwa kabisa. Kwa hiyo, maelezo yake nimeyasikia, lakini tujadili kama Taifa na tumshauri namna ya kwenda mbele ili jambo hili hata mwaka wa fedha ujao lisije kwa namna ambavyo linajitokeza hapa. Tutengeneze mahusiano na watu wetu, zoezi liwe shirikishi, mipaka iangaliwe upya, *beacon* zijulikane na tukubaliane kama Taifa namna ya kwenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba wenzangu waniunge mkono ili hili jambo tulijadili kwa upana wake.

**MWENYEKITI:** Watu watatu, wanne, mechi ya leo imekwisha.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kutumia vipaza sauti)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana, wapo wengi.

**MWENYEKITI:** Haya moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nane. Imekwisha, hamna kitu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Daniel Awack. Mheshimiwa Waitara, ukitaka jambo lako jipange kama ulivyojipanga kwenye mambo mengine. Mheshimiwa Awack.

**MHE. DANIEL A. TLEMAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Sote tunajua kwamba hifadhi zetu zinaleta fedha nyingi za kigeni katika nchi yetu. Pamoja na kuleta fedha nyingi na kukuza uchumi wa nchi yetu, lakini utaifishaji wa mifugo ya wananchi wetu imetokea mara nyingi sana katika mbuga zetu ndani ya hifadhi katika nchi hii. Katika Mbuga ya Burigi Chato, Serengeti, katika eneo la Mikumi na katika eneo la Manyara. Ninataka ufafanuzi kuhusu utaifishaji wa mifugo ya wananchi wetu katika maeneo yetu katika nchi hii katika mbuga zetu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Awack, hili swali lilishaulizwa na Mheshimiwa Mussa na limetolewa majibu na wewe hukuomba kushika shilingi. Kwa hiyo, majibu yale yale ya mwanzo ya Mheshimiwa Waziri ndiyo hayo hayo ambayo yatakwenda kufanya kazi na kwako.

Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Mchungahela.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nimesimama kwa jambo la mwingiliano hasi wa majukumu kati ya Hifadhi na *TTB*, kwa maana ya bodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Utalii Ssura Na. 65; hali kadhalika Sheria ya Bodi ile iliyofanyiwa marekebisho Sura Namba 364; sheria hizi zote zimetoa maelekezo ya wazi kabisa jinsi ya majukumu yanavyotakiwa yawe katika taasisi hizo tofauti mbili. Miongoni mwa jukumu mojawapo muhimu kabisa kwa *TTB* ni la utangazaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kumejitokeza changamoto ya taasisi hizi kuwa zimejitokeza katika mazingira ya kutaka kupoka majukumu yale ya *TTB*. Kwa hiyo, ningetaka kupata ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kwa hali halisi ilivyo mpaka sasa hivi, maana sijapata majibu yoyote kuhusiana au sijasikia mpango wowote ukizungumzia suala hili la mwingiliano wa haya majukumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba majibu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Kama hayatakuwa yameniridhisha nitaomba wenzangu waniunge mkono.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti ninakushukuru. Nimemsikiliza Mheshimiwa Mchungahela na ameiweka vyema Sheria, Sura ya 364. Mwenye jukumu la kuratibu na kutangaza utalii wa Taifa letu, kui-*brand* nchi yetu ni Bodi yetu ya Taifa ya Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ana jukumu la kutangaza na kuratibu. Yeye anawaratibu pia wadau mbalimbali wanaoshughulika na shughuli za utalii ndani ya Taifa letu. Kwa hiyo, kwenye jambo hili Bodi yetu ya Taifa ya Utalii imekuwa ikilifanya jambo hili kwa miaka yote na hakuna mtu ambaye ameshapoka jukumu lake hili la kutangaza na kuratibu. Kwa hiyo, wapo wadau wa utalii wa sekta binafsi, wapo wadau wa utalii hata kampuni zilizopo ndani ya Serikali ambao nao pia hushiriki kwenda kutangaza vivutio mbalimbali vya utalii walivyonavyo, wakiratibiwa na Bodi yetu ya Taifa ya Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mchungahela kwamba jambo hili linaendelea kufanywa kiukamilifu na Bodi yetu ya Taifa ya Utalii na pia kwa maelekezo ya Bunge lako Tukufu na kwa utayari wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Hata yale ambayo yaliyokuwa yanafanywa na idara yetu ya utalii ndani ya wizara, ikiwemo kuainisha vivutio mbalimbali, sasa sheria inarekebishwa kama alivyosema yeye na tupo hatua za mwisho. Ninaamini hata haya majukumu mengine pia yatarejeshwa kwenda Bodi ya Taifa ya Utalii na sisi kama Wizara tutabaki kuwa kwenye sekta na tuweze kuwasimamia ili tuone *destination* Tanzania ikifika duniani kwenye maeneo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuongezea baada ya kuwa nimefuatilia mjadala. Zimejitokeza hoja nyingi, hata zile ambazo kwa mujibu wa kanuni zinajirudia zilikuwa zinatupa ujumbe mmoja tu kwamba kuna mambo ambayo wawakilishi hawa wa wananchi wanakutana nayo kule majimboni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge kwa kuonesha kwamba wao ni Wabunge wanaowajibika kwa Watanzania waliowachagua. Serikali hii inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan pia ni Serikali inayowajibika kwa Watanzania. Kwa hoja hizi ambazo

zimejitokeza zote kwa ujumla, kuanzia kwenye michango na hizi ambazo zimekuja kujitokeza katika kipindi hiki ambacho Bunge lako limekaa kama Kamati, tumezipokea; tukianza na hoja ambayo *Chief Whip* ametoka kuisemea pamoja na hizi ambazo zimejirudia rudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais tayari alikwishaelekeza Wizara ya Maliasili na Utalii kushirikiana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wizara ya Katiba na Sheria kuyaangalia upya haya masuala ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyapazia sauti hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaenda kupitia upya Sheria Namba 111 na 116 inayoongelea masuala ya kutaifisha. Tutaenda kuangalia upya masuala yanayohusiana na hii mipaka, hasa ambapo baadhi ya maeneo haijulikani hasa mpaka ni upi. Baada ya ile taarifa ambayo tumepewa hapa ambayo ilishakamilika, tutaenda kuifanya hiyo kazi ili wananchi wajue hasa mpaka ni wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, tutaenda kufanyia kazi hili jambo la mahusiano katika maeneo yetu. Sheria zetu ambazo zilikuwepo kwenye haya masuala ya hifadhi, adhabu ziko zinaendana. Mwenye mkaa na aliyebeba meno ya tembo wote wanapata adhabu inayofanana; yule aliyelima mazao yake na yule anayefanya ujangili zote zinafanana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Rais ameelekeza sheria hiyo iangaliwe upya, niwaombe Waheshimiwa Wabunge watoe nafasi kwa Serikali ili tukaangalie haya yote kwa ajili ya ustawi wa maisha ya Watanzania, lakini pia na ustawi na uendelevu wa uhifadhi na utalii ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe Waheshimiwa Wabunge waridhie ili tukafanyie kazi haya yote waliyochangia kuhusiana na hoja hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Getere, Mheshimiwa Kinyoma na Mheshimiwa Mgore Miraji Kigera, mtaonana na Waziri Mkuu ili kumpa hoja zenu ambazo zitachukuliwa kwa pamoja ili ziende zikafanyiwe kazi. *(Makofi/Kicheko)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts Unit*…………....Sh.1,205,133,000
Kifungu 1003 - *Policy and Planning Unit*……………...Sh.1,864,482,501
Kifungu 1004 - *Government Communication Unit*……………………….………….……….Sh.663,806,988
Kifungu 1005 - *Internal Audit Unit*……..……………..…..Sh.861,114,000
Kifungu 1006 - *Procurement Management Unit*……………………….…………..Sh.813,052,780
Kifungu 1007 - *Legal Services Unit*……………………....Sh.833,928,500
Kifungu 1008 - *Management Information Systems Unit*………………...……….Sh.1,070,888,000
Kifungu 1009 - *Research and Training Unit*.............Sh.37,660,075,441
Kifungu 1010 - *Paramilitary Coordination Unit*………………..………………..….Sh.1,303,303,036
Kifungu 1011 - *Monitoring and Evaluation Unit*……….………………………………..Sh.694,600,000
Kifungu 2001 – *Wildlife*……………………....…....Sh.120,495,199,316
Kifungu 3001 - *Forestry and Beekeeping*…………......Sh.70,425,539,596
Kifungu 4001 – *Tourism*…………………….........…...Sh.14,776,117,677
Kifungu 4002 - *Antiquities Unit*………………………....Sh.12,124,254,615

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba Kamati yako ijielekeze kwenye Kitabu cha Nne, Miradi ya Maendeleo, kwenye vishikwambi ni ukurasa wa 291, Fungu 69.

## KITABU CHA NNE

## MIPANGO YA MAENDELEO

## FUNGU 69 – WIZARA YA MALIASILI NA UTALII

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts Unit*…………..….Sh.57,476,764
Kifungu 1003 - *Policy and Planning Unit*……………...Sh.9,341,280,593
Kifungu 2001 - *Wildlife*………………..…...……….…Sh.36,664,470,117
Kifungu 3001 - *Forestry and Beekeeping*….………..Sh.12,674,643,002
Kifungu 4001 - *Tourism*………………..……………..…Sh.2,563,574,524
Kifungu 4002 - *Antiquities Unit*………………………....Sh.1,000,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Mtoa hoja.

## T A A R I F A

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 126(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, ninaomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi zake, ninaomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba niwahoji kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Waheshimiwa Wabunge, walioafiki wameshinda. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 Yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Nichukue nafasi hii kukushukuru Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri uliyoifanya wewe na Naibu wako na watendaji wenu, lakini hasa Waheshimiwa Wabunge; hizi ndizo kazi za Kibunge. Mmesimamia wananchi wenu na Serikali imetoa majibu; na *commitment* ya Waziri Mkuu ndiyo *commitment* ya mwisho ndani ya Bunge letu.

Sasa ni kufuatilia *commitment*. Kikao kifanyike tukubaliane, tunajenga nchi moja. Kuchafua mazingira ni kuua Taifa. Unaweza ukaokoa kisehemu kidogo, lakini nchi nzima ikafa. Kwa hiyo, mazingira yetu ni muhimu. Hata hivyo, dhuluma bado zinafanywa na baadhi ya watu wabaya wanaoumiza wananchi. Hao Mheshimiwa Waziri Mkuu ni lazima ulale nao. Kwa kweli watu wanaumia sana. *(Makofi/Kicheko)*

Sina maana hiyo, samahani! Unajua maneno ya mjini nayo saa nyingine… *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, nikuombe sana, bado kuna watendaji. Wizari hii tukiweka *select committee* leo, kesho watu mtaondoka humu, *honestly*; kwa sababu dhuluma bado zinafanywa. Zinafanywa na tunaziona zinafanywa na hakuna hatua zinazochukuliwa.

Mheshimiwa Waziri, taasisi zako zifuatilie, wakati mwingine hawa wazee wanaumia kimoyo moyo. Wanaoumia zaidi ni watoto wao, na ndiyo maana wanaandamana. Wanajiunga na vikundi bila kujua kwa sababu ya uchungu wa kuona wazazi wao wanavyoteseka na mali zao. Mtu anaona kabisa hifadhi hii kuna

ng'ombe wanalisha hawaguswi, hapa mtu akipita na baiskeli anakamatwa. *This should not happen!* Mnanisikia makamanda huko. Tunaomba sana; kazi na utu – Tunasonga mbele. Lakini hapa utu hakuna, kazi zipo, utu hakuna.

Niombe sana Mheshimiwa Waziri, masuala ya tembo, mnajitahidi jitahidini zaidi. Kuna kitu kinaitwa *Human-Elephant Conflict,* ninafikiri mnaijua hiyo. Jitahidini zaidi na zaidi na zaidi kuhakikisha wanyama hawa hawaendelei kuharibu mali na hasa maisha ya watu.

Nimesikia mmezungumzia takwimu za 5,935,000 za watalii ni kweli, lakini hapa kwenye 2,294,000 ni wa nje, wa ndani ni zaidi. Tunataka watalii wa nje ndiyo wawe wengi zaidi, ili mapato mengi yapatikane, *and you can do it.* Mkishirikiana mnaweza mkafanya. Lakini Wizara moja huyu anafanya, mwingine anafanya, halafu hakuna mtu anajua *results* zinakuwa hatupati, ongezeni jitihada. Rais amejitolea akafanya ziara, akafanya *tour*, sisi tunafanya nini? Na sisi tuoneshe basi. Onesha Mheshimiwa Waziri, tunataka mwakani nyongeza ya bilioni tatu dola, ziko, utaleta. Mungu akujalie. *(Makofi)*

Waheshimiwa, kuna Mwongozo wa Spika ulioombwa na Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo kuhusu lugha iliyotumiwa na Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, tarehe 14 Mei 2026 katika Kikao cha 29 cha Mkutano wa Tatu wa Bunge la 13 Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo aliomba Mwongozo wa Spika. Mwongozo huo uliombwa chini ya Kanuni ya 79 ya Kanuni za Kudumu za Bunge 2025. Mheshimiwa Hokororo alitaka kujua iwapo lugha iliyotumiwa na Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga inaruhusiwa au hairuhusiwi. Awali Mheshimiwa Kiswaga aliyekuwa anachangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Kiti kiliahidi kupitia Kumbukumbu Rasmi za Bunge za siku hiyo, kisha kilieleza kwamba kitatoa mwongozo katika suala hilo.

Waheshimiwa Wabunge, nimepitia Kumbukumbu za Bunge za tarehe 14 Mei 2026 kuhusu mchango wa Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga, (Mb). Nimebaini kwamba Mheshimiwa Mbunge

alizungumza ifuatavyo: "*Mheshimiwa mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Bashiru. Amekuwa mjumbe wa kamati ya maji na mazingira, niliposikia amepewa uwaziri nilifurahi sana. Ndugu yangu Mheshimiwa Bashiru, umeingia mahali pana wahuni wengi na pahali pagumu, tukiwemo sisi wanasiasa na wafanyabiashara wengine walioko Serikalini.*"

Waheshimiwa Wabunge, maelezo hayo yalifanya Mheshimiwa Hokororo kuomba Mwongozo wa Spika. Katika maombi yake alitaka kujua iwapo maneno yaliyotumiwa na Mheshimiwa Kiswaga ni lugha inayoruhusiwa Bungeni. Hoja ya Mheshimiwa Hokororo ni kuwa tafsiri ya maneno ya Mheshimiwa Kiswaga inaudhi, inadhalilisha mtu mmoja mmoja au kundi la watu wengi na vilevile ni lugha isiyokubalika Bungeni kwa mujibu wa kanuni ya 74(k) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025.

Waheshimiwa Wabunge, suala linalohitaji Mwongozo wa Spika ni; je, maneno yaliyotumiwa na Mheshimiwa Kiswaga ni lugha inayokubalika katika mijadala ya Bunge?

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyoeleza, *Hansard* ya tarehe 14 Mei, 2026, inaonesha kwamba Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga alichangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ya mwaka wa fedha 2026/2027. Mheshimiwa huyo alieleza kuwa anaufahamu utendaji wa uaminifu wa Mheshimiwa Balozi Dkt. Bashiru, Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa sababu alikuwa ni mjumbe wa Kamati inayoongozwa na Mheshimiwa Kiswaga.

Kupitia mchango huo Mheshimiwa Kiswaga alimtahadharisha Mheshimiwa Balozi Dkt. Bashiru Kakurwa juu ya ugumu wa kuongoza Wizara ya Ardhi. Aidha, alisema kwamba, "*Mheshimiwa Waziri, umeingia mahali ambapo pana wahuni wengi wakiwemo wanasiasa na wafanyabiashara wengine walioko Serikalini.*" Hivyo, alimsihi aongoze na sayansi na utafiti ili uvuvi uwe endelevu kwa manufaa ya vizazi vijavyo.

Waheshimiwa Wabunge, katika maelezo yake Mheshimiwa Kiswaga alitumia *maneno "pana wahuni wengi, wakiwemo wanasiasa na wafanyabiashara wengine walioko Serikalini.*" Nimetafuta tafsiri ya neno wahuni kwenye Kamusi ya Kiswahili ya

Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), Toleo la Pili la 2017; neno muhuni limetafsiriwa kuwa ni: *"Mtu ambaye tabia yake siyo nzuri; mtu ambaye hajaoa wala kuolewa; mtu ambaye anapenda kukaa katika magenge ya watu na wala hana mahali maalum pa kuishi." (Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na kwamba mchango wa Mheshimiwa Kiswaga ni mzuri, maneno yake kwamba pana wahuni wengi katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi tukiwemo wanasiasa na wafanyabiashara wengine walioko Serikalini ni tuhuma zinazohitaji uthibitisho. Mheshimiwa Kiswaga alitumia maneno hayo bila kuwasilisha uthibitisho wowote ili kuyapa maelezo yake uzito.

Waheshimiwa Wabunge, lugha hiyo haikubaliki, maneno haya ni ya kuudhi na kudhalilisha, siyo tu kwa Wabunge bali pia watu wengine waliotajwa kwa ujumla kwenye mchango wa Mheshimiwa Kiswaga. Lugha hiyo haipaswi kutumiwa katika mijadala ya Bunge. Kanuni ya 74(1)(k) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025 inakataza kutumia lugha namna hiyo ifuatavyo: -

74._(1) Bila kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge-

(k) hatatumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine.

Kutokana na tafsiri ya Kamusi *BAKITA* na masharti ya Kanuni ya 74(1)(k) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, nimejiridhisha kwamba maneno ya Mheshimiwa Kiswaga ni maneno ya kuudhi na yanayodhalilisha.

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na kuwa Ibara ya 100 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inatupa Wabunge uhuru wa majadiliano Bungeni, tunao wajibu wa kuhakikisha lugha tunayotumia inalinda hadhi na heshima ya Bunge. Inatakiwa kuwa ni lugha fasaha, lugha inayoeleweka na isiyoudhi au kudhalilisha.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu hiyo, maneno haya hayapaswi kuwa sehemu katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge. Kwa mantiki hiyo, ninaelekeza kwamba maneno "sasa ndugu yangu Mheshimiwa Bashiru, umeingia mahali pana wahuni wengi na mahali pagumu, tukiwemo sisi wanasiasa na wafanyabiashara wengine walioko Serikalini" yafutwe kwenye *Hansard*. Uamuzi huu unatolewa kwa mujibu wa Kanuni ya 5(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge 2025. Huo ndiyo Mwongozo wa Spika. Umetolewa leo tarehe 18 Mei, 2026.

Waheshimiwa Wabunge baada ya maneno hayo ninawashukuru tena na kuwapongeza, lakini nipongeze Serikali kwa namna mnavyojibu na hasa Waziri Mkuu ku-*intervene* na kulifanyia kazi. Niwaombe sana; *Chief Whip* ametoa kauli ndani ya Bunge iko kwenye *Hansard*, kesho kikao kifanywe na mpate mwafaka na Waheshimiwa Wabunge ili wananchi wetu wawe na raha kwa kuwa wako Tanzania na mambo yao yanayotekelezwa na Serikali yao.

Baada ya maneno hayo, ninaahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 2.21 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 19 Mei, 2026 Saa Tatu Asubuhi)*